# ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA UTEUZI WA MSAMIATI: MFANO WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI

**NA**

**PAUL SANKALE SITO**

**C50/63461/2013**

**Tansnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi**

**2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi…………………………………………………Tarehe …………………………………

**Paul Sankale Sito**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Kiswahili.

Sahihi…………………………………………………Tarehe …………………………………

**Dkt. Ayub Mukhwana**

(Msimamizi)

Sahihi…………………………………………………Tarehe …………………………………

**Dkt. Iribe Mwangi**

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu ambao walinitia moyo katika safari hii. Kwa mama yangu mpendwa Ann Sito ambaye alijifunga kibwebwe na kujinyima kwa ajili ya elimu yangu. Mungu akubariki sana. Kwa marehemu baba yangu uliyetuacha 26.9.2013 Leyeyio Ole Sito, ambaye kwake hamna kilichokuwa kigumu. Mungu wa mbinguni akuhifadhi pema.

Nawatabarukia mke wangu mpendwa Elizabeth na wanangu Saiton Sito na Bramwel Letayian ambao hata nilipokuwa mjini Nairobi kwa ajili ya masomo yangu, walinihakikishia kusimama nami hadi mwisho wa elimu yangu. Upole na uvumilivu wenu umenipa nguvu nilizozihitaji katika utafiti huu. Kwa kaka na dada zangu wote kwa kunipa nafasi ya kusoma na kuhitimisha elimu yangu. Mungu awabariki nyote.

Kwa Francis Nkako uliyepanda mche wa elimu katika maisha yangu.

Kwa familia yote ya Sito kwa kuwa na imani na mtoto wenu. Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Safari ya kukamilisha tasnifu hii ilikuwa na pandashuka si haba, lakini nashukuru kwa ushauri, maelekezo na mawazo ya watu kadhaa. Mchango wao mkubwa ulipunguza uzito wa kazi hii. Natoa shukurani zangu kwa Maulana kwa kunipa afya nguvu na neema katika kipindi hiki cha shahada ya uzamili na kuniwezesha kuikamilisha. Namshukuru kwa kuwa si lazima kwamba ukianza jambo utalimaliza; wengi huanza safari ila hawafiki walikoazimia kufika.

Shukrani zangu za dhati na za moyo mkunjufu kwa wasimamizi wangu Dkt. Ayub Mukhwana na Dkt. Iribe Mwangi. Walijitolea kwa hali na mali kunielekeza kila nilipowahitaji. Nawashukuru sana kwa kuwa japo walikuwa na majukumu mengi ya kutekeleza waliweza kunihudumia. Mawaidha, tahakiki, ushauri na maelekezo ya kitaaluma ambayo walinifaa nayo yatabaki yamesitiriwa moyoni mwangu milele. Mchango wenu unanifanya kuwa mdeni wenu. Mungu awaongezee hekima.

Natoa shukrani za dhati kwa wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili, kwa ushauri wao na maelekezo yao katika kipindi cha usomi wangu katika Chuo Kikuu cha Nairobi tangu shahada ya kwanza hadi shahada hii ya uzamili. Nawashukuru wahadhiri wote walionifunza shahada ya kwanza kwa kunipa motisha ya kujiunga na uzamili. Shukurani zangu ziwaendee Dkt. Mbuthia, Dkt. Swaleh, Prof. Timammy, Dkt. Omboga, Bi. Mary Ndung'u, Bw. Walubengo, na Dkt. Mweri ambao walinipa msingi mzuri wakati wa shahada yangu ya kwanza. Nawashukuru pia Prof. Habwe, Prof wa Mutiso, Prof. Mbatiah na Ndugu Mungania.

Tasnifu hii haingekamilika bila mchango wa jumuiya ya shule za msingi na upili za Naikarra. Mlinitia moyo na kunielekeza kwa mashauri nasaha ambayo yamenipiga jeki pakubwa katika safari hii. Kwa mwalimu mkuu wa shule ya Naikarra Bw. Koileken Loontubu ambaye alinielewa kila nilipohitaji idhini ya kuwa nje ya shule kwa sababu ya utafiti huu. Kwenu nyote nasema Maulana awabariki walimu pamoja na wanafunzi wote, na awazidishie neema zake.

Basi hili la shahada ya uzamili tuliabiri pamoja na wanafunzi wenzangu ambao tulihimizana na kutiana moyo. Naomba Mola awaongoze katika jitihada zenu za kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Mola awabariki Mutahi Miricho, Peter Kilonzo, Hudson Nyandiwa, Edward Zani, Lawrence

Orenge, Timothy Mukaria, Dinah Sungu, Julita Wanjala, Evelyn Kanyange, Rose Nyamemba, Damarice Otuoma, Rose Mutunga, Lydiah Shaviya, Magdaline Yegon, Judy Kemunto, Queen Ndoni, Gladys Kinyua, na Flora Omosa.

Nawashukuru ndugu zangu Joel, Margaret, Simon, Jennifer na Eliza kwa kunipa moyo na wakati wenye amani na utulivu katika kipindi nilichokuwa ninafanya kazi hii. Namshukuru pia binamu yangu Catherine Nkere ambaye kila wakati tulipokutana au hata kuzungumza kwa simu, alizoea kuniuliza, "Na je, umefikisha wapi masomo yako?" Mungu akubariki.

Nawashukuru rafiki zangu ambao siwezi kuwataja wote ila baadhi: Ruth Binyanya, Getrude Mapenzi na Evans Mdamu ambao tulikuwa darasa moja katika shahada yetu ya kwanza, Lanoi Keton kwa kuhimizana na kutiana moyo katika bahari hii ya elimu, Benson Mwangangi kwa kunihimiza nizidishe bidii katika uwanja huu wa elimu.

Shukrani zangu za dhati pia zimwendee Bi. Christine Oyolo ambaye alipiga chapa baadhi ya sura za utafiti huu kwa haraka tena kwa moyo mkunjufu. Mungu akubariki.

Watu ambao ningependa kuwashukuru kwa kuwataja majina ni wengi lakini muda na nafasi haitoshi. Pokeeni shukrani zangu hata kama sikuwataja.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati. Tumetumia methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kama data ya uchanganuzi wetu. Utafiti huu una jumla ya sura tano. Tatizo letu la utafiti limetokana na ukweli kwamba hakuna maana moja inayojitokeza ili kueleza dhana ya methali. Wataalamu mbalimbali wamefafanua dhana ya methali kwa mujibu wa mkabala ambao wanaufasili. Ndiposa utafiti wetu umezamia suala la mazingira na mchango wake katika uteuzi wa msamiati katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini, msamiati ulioteuliwa hukusudiwa kuafikia malengo gani kwa jamii na jinsi msamiati ulioteuliwa unatusaidia kuelewa mahusiano na maafikiano ya watu katika jamii inayotumia lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu una madhumuni matatu: kufafanua sifa, tabia na maumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini, kueleza athari zinazotokana na matumizi ya methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii ambamo lugha ya Kiswahili hutumiwa, kuchunguza uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika mazingira mahsusi. Madhumuni yetu yametokana na nadharia tete zetu kuwa kunao viumbe wenye maumbile, sifa, na tabia mahsusi ambao kwa mujibu wa wanajamii hutumika katika methali za Kiswahili, na kwamba maumbile, sifa na tabia za viumbe hao zinafaa kwa matumizi ya methali mahsusi katika jamii ya Waswahili, athari zinazotokana na matumizi ya msamiati wa Kiswahili unaohusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini zinaonekana na kwamba methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini huwa na uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu fulani katika mazingira mahsusi. Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya mahusiano, ambapo dhana zake tatu za utambuzi, mawasiliano na uelewa zimetuongoza katika utafiti huu. Katika utafiti wetu tumetoa maelezo kuhusu dhana muhimu katika utafiti huu, na pia kuangazia methali kwa ujumla wake. Pia tumefanya ufafanuzi wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kwa kuangazia sifa, tabia na maumbile ya viumbe waliotumika katika methali hizo. Katika uchanganuzi wa data, utafiti wetu umethibitisha kuwa mazingira ni muhimu sana katika uteuzi wa msamiati. Msamiati ulioteuliwa na kutumika katika methali husika huwa na athari kwa wanajamii na kuwa methali hizo husika huwa na uamilifu wa majukumu katika jamii.

## YALIYOMO


Ungamo ........ ii

Tabaruku ........ iii

Shukrani ........ iv

Ikisiri ........ vi

**SURA YA KWANZA ........ 1**

1.0 Usuli Wa Mada Ya Utafiti ........ 1

1.1 Tatizo La Utafiti ........ 3

1.3 Madhumuni Ya Utafiti ........ 4

1.4 Nadharia Tete ........ 4

1.5 Sababu Za Kuchagua Mada ........ 4

1.6 Upeo Na Mipaka ........ 5

1.7 Msingi Wa Kinadharia ........ 6

1.7.1 Dhana Muhimu Katika Nadharia Ya Mahusiano ........ 8

1.7.2 Umuhimu Wa Nadharia Ya Mahusiano Katika Utafiti Huu ........ 15

1.8 . Yaliyoandikwa Kuhusiana Na Mada ........ 16

1.9 Mbinu Za Utafiti ........ 20

1.9.1 Mahali Pa Utafiti ........ 20

1.9.1.1 Uteuzi Wa Sampuli ........ 21

1.9.2 Ukusanyaji Data ........ 21

1.9.2.1. Uchanganuzi Wa Data ........ 21

1.9.3. Uwasilishaji Wa Data ........ 22

1.9.4 Walengwa ........ 22

**SURA YA PILI ........ 23**

**DHANA MUHIMU KATIKA TAALUMA YA METHALI ........ 23**

2.0 Utangulizi ........ 23

2.1 Dhana Ya Isimujamii ........ 23

2.2 Dhana Ya Jamii ........ 24

2.3 Dhana Ya Msamiati ........................................................................................................ 25
2.4 Methali ............................................................................................................................ 26
2.4.1 Sifa Za Methali .............................................................................................................. 27
2.4.1.1 Uwili .............................................................................................................................. 27
2.4.1.2 Mkato Na Ufupisho Wa Kimuundo .................................................................................. 27
2.4.1.3 Mbinu Ya Ushairi ........................................................................................................... 28
2.4.1.4 Matumizi Ya Tamathali Za Usemi ................................................................................... 29
2.4.1.5 Matumizi Ya Lahaja Na Msamiati Wa Kale...................................................................... 29
2.4.2 Mbinu Za Kuainisha Methali ............................................................................................ 30
2.4.2.1 Uanishaji Wa Kimaudhui.................................................................................................. 30
2.4.2.2 Uainishaji Wa Unaotegemea Sauti Za Kati Na Za Mwisho ............................................ 33
2.4.3 Uanishaji Katika Makundi Ya Nomino .............................................................................. 33
2.4.3.1 Methali Zonazorejelea Sehemu Za Mwili.......................................................................... 33
2.4.3.2 Methali Zinazorejelea Wanyama ...................................................................................... 33
2.4.3.3 Methali Zinazorejelea Ndege ............................................................................................ 34
2.4.3.4 Uanishaji Wa Methali Zinazorejelea Wadudu................................................................... 34
2.4.3.5 Methali Zinazorejelea Mimea Na Matunda ...................................................................... 34
2.4.3.5 Methali Zinazorejelea Hali ............................................................................................... 35
2.4.4 Methali Za Kiswahili ........................................................................................................ 35
2.5 Lugha Ya Kiswahili ............................................................................................................ 36
2.6 Hitimisho............................................................................................................................. 37
**SURA YA TATU .................................................................................................................. 38**
**UFAFANUZI WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI: SIFA, TABIA NA MAUMBILE YA VIUMBE WALIOTUMIKA KATIKA METHALI HIZO ............................................................................................................ 38**
3.0 Utangulizi............................................................................................................................ 38
1.Alaye Kitu Cha Mamba Asifike Majini................................................................................ 39
2. Ana Nchi Yake Simba Ana Maji Yake Mamba.................................................................... 40
3. Anayetaka Kufa Na Ala Bunju, Atazame Rehema Ya Mungu ............................................ 41

4. Atakaye Maji Mtoni Asimtukane Mamba ........ 41
5. Avumaye Baharini Papa Kumbe Wengine Wapo ........ 42
6. Binadamu Ni Ngamba Hawakosi La Kuamba ........ 43
7. Chafi Kandani Mwako Ni Chafi- Kiyenge ........ 44
8. Chafi Rasilmali Yake Utumbo (Matumbo) ........ 45
9. Chokochoko Kamchokoe Pweza, Binadamu Hutamweza ........ 45
10. Chombo Cha Samaki Hakiachi Kunuka Vumba ........ 46
11. Chombo Kilichopikiwa Samaki Hakiachi Kunuka Vumba ........ 46
12. Chura Akitupwa Majini Hafi ........ 47
13. Chura Hupenda Maji Lakini Si Maji Moto ........ 47
14. Chura Huweza Kumwua Tembo ........ 47
15. Chura (Hu)Mzuia Maji Ndovu Akiyatamani ........ 48
16. Dagaa Amemponza Ndobe ........ 48
17. Dunia Mwendo Wa Ngisi ........ 49
18. Ewe Mtuje, Kwamba Wali Tafi Ungalikuwaje? ........ 50
19. Hasira Ya Mkizi Tijara (Furaha) Ya Mvuvi ........ 51
20. Huna Mshipi, Huna Ngwe Kuomoa Tenga Ni Nini? ........ 52
21. Kaa Akiinua Gando Mambo Yamekatika ........ 53
22. Kaa Mkuu Ng'ombe Wa Maji Akiinua Gando Mwelemeze Nanda ........ 53
23. Kajigeuza Chachandu Kujipalia Makaa ........ 54
24. Kambare Mkunje Angali Mbichi ........ 55
25. Kangaja Simle, Mchuzi Kitoweo ........ 55
26. Kasirani Ya Mkizi Ni Furaha Kwa Mwenye Tando ........ 56
27. Kiboko Aliyepasha Habari Hapasui Mtumbwi ........ 56
28. Kila Kiboko Na Kivuko Chake ........ 57
29. Kila Mvuvi Wa Pweza Tutaonana Mwambani ........ 58
30. Kilichompata Ngwena Na Kiboko Ni Hicho ........ 58
31. Kitatange Hutia Chafi Lemani ........ 59
32. Kumla Nguru Si Kazi, Kazi Ni Kumwosha ........ 59

33. Kumla Nguru Si Kazi, Kazi Ni Kumtoa Magamba ........ 60
34. Kuvua Numbi Si Kazi, Kazi Ni Magawioni ........ 60
35. Maji Marefu Mwulize Chura ........ 61
36. Mamba Hutoka Majini Na Kulamba Umande ........ 62
37. Maskini Hajui Kula Na Mkwasi, Akianza Kula Samaki Huanza Kichwani ........ 63
38. Mbio Za Kasa Si Mbio Lakini Humfikisha Aendapo ........ 63
39. Mchagua Samaki Hupata Aliyechina ........ 64
40. Mtafitafi Hula Samaki (Nswi), Mtulivu Hula Nyama ........ 64
41. Mvuvi Ndiye Ajuaye Pweza Alipo ........ 65
42. Nguvu Ya Mamba Ni Maji ........ 66
43. Ngwena Na Mwenzake (Mwingine) Hawapatani ........ 66
44. Nyama Wote Wangawako, Mkuza Pezi Ni Papa ........ 67
45. Pono Mmoja Akioza Huoza Na Shazile ........ 67
46. Pweza Kamwambia Ngisi, 'Tusifanye Majilisi, Maji Yakipwa Tukisi' ........ 68
47. Samaki Akilia Machozi Yake Hupelekwa Na Maji ........ 69
48. Samaki Huanza Kuoza Kichwani ........ 70
49. Samaki Mkunje Angali Mbichi ........ 70
50. Samaki Mmoja Akioza, Huoza Wote ........ 70
51. Samaki Mmoja Akioza Ni Mtungo Pia ........ 71
52. Samaki Wote Hunuka Walimshuku Kambare ........ 71
53. Shuka Ya Maskini Ndiyo Itandiwayo Dagaa ........ 71
54. Taa Haachi Mwibawe ........ 72
55. Ukikaa Na Simba, Vaa Ngozi Ya Mamba ........ 72
56. Ulimwengu Umemshinda Kaa Endaye Upande Upande ........ 72
57. Umekuwa Nguva Huhimili Kishindo? ........ 73
58. Umeona Wapi Mnandi Kujenga Nyumba Machweoni ........ 73
59. Ungeenda Juu Kiboko Makazi Yako Pwani ........ 74
60. Usiku Kiza Mangazibwe Mtumbuu Huwa Papa ........ 74
61. Uso Wa Samaki Hausikii Viungo ........ 74

62. Wavu Utakaonasa Samaki Wengi Huanza Mapema ........ 75
63. Wavuvi Wa Pweza Hujuana Mwambani ........ 75
64. Zobe Na Msuwele Wote Ni Wamoja ........ 75
3.2 Hitimisho ........ 76
**SURA YA NNE ........ 77**
**ATHARI KWA JAMII PAMOJA NA UAMILIFU WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI KATIKA JAMII ........ 77**
4.1 Utangulizi ........ 77
4.2 Habari Ya Waliojaza Hojaji ........ 78
4.2.1 Umri Wa Waliojaza Hojaji ........ 78
4.2.2 Kituo Cha Kufanyia Kazi ........ 79
4.3 Msamiati Na Athari Zake Katika Mazingira Mahsusi Kwa Mwanajamii Au Wanajamii ........ 79
4.4 Athari Kwa Jamii Kutokana Na Methalizinazorejelea Viumbe Wa Majini ........ 81
1. Alaye Kitu Cha Mamba Asifike Mtoni ........ 81
2. Anayetaka Kufa Na Ala Bunju, Atazamerehema Za Mungu ........ 83
3. Avumaye Baharini Papa Kumbe Wengine Wapo ........ 84
4. Binadamu Ni Ngamba Hawakosi La Kuamba ........ 85
5. Chafi Kandani Mwako Ni Chafi- Kiyenge ........ 86
6. Chokochoko Kamchokoe Pweza, Binadamu Hutamweza ........ 87
7. Chombo Cha Samaki Hakiachi Kunuka Vumba ........ 88
8. Chura Akitupwa Majini Hafi ........ 89
9. Dagaa Amemponza Ndobe ........ 90
10. Dunia Mwendo Wa Ngisi ........ 91
11. Ewe Mtuje, Kwamba Wali Tafi Ungalikuwaje? ........ 92
12. Hasira Za Mkizi Tijara (Furaha) Ya Mvuvi ........ 93
13. Huna Mshipi, Huna Ngwe Kuomoa Tenga Ni Nini? ........ 94
14. Kaa Akiinua Gando Mambo Yamekatika ........ 95
15. Kajigeuza Chachandu Kujipalia Makaa ........ 96
16. Kambare Mkunje Angali Mbichi ........ 97

17. Kangaja Simle, Mchuzi Kitoweo ........ 98
18. Kiboko Aliyepasha Habari Hapasui Mtumbwi ........ 99
19. Kilichompata Ngwena Na Kiboko Ni Hicho ........ 100
20. Kitatange Hutia Chafi Lemani ........ 101
22. Kuvua Numbi Si Kazi, Kazi Magawiani ........ 103
23. Mbio Za Kasa Si Mbio Lakini Humfikisha Aendapo ........ 104
24. Pono Mmoja Akioza Huoza Na Shazile ........ 105
25. Pweza Kamwambia Ngisi, Tusifanye Majilisi, Maji Yakipwa Tukisi ........ 106
26. Shuka Ya Maskini Ndiyo Itandiwayo Dagaa ........ 107
27. Taa Haachi Mwibawe ........ 108
28. Ukikaa Na Simba, Vaa Ngozi Ya Mamba ........ 109
29. Umekuwa Nguva Huhimili Kishindo ........ 110
30. Umeona Wapi Mnandi Kujenga Nyumba Machweoni ........ 111
31. Usiku Kiza Mangazimbwe Mtumbuu Huwa Papa ........ 112
32. Zobe Na Msuwele Wote Ni Wamoja ........ 113
4.5 Uamilifu Wa Methali Za Kiswahili Zinazorejelea Viumbe Wa Majini ........ 114
4.5.1 Kurahisisha Mawasiliano ........ 114
4.5.2 Kubadili Mada ........ 116
4.5.3 Kutenga Kundi Fulani Katika Mawasiliano ........ 118
4.5.4 Kuonya ........ 119
4.5.5 Kuburudisha Na Kupumbaza ........ 121
4.5.6 Kufunza Na Kuasa ........ 122
4.5.7 Kutia Moyo ........ 125
4.5.8 Kukashifu ........ 126
4.5.9 Kutahadharisha ........ 128
4.5.10 Kushauri ........ 130
4.6 Hitimisho ........ 132

**SURA YA TANO ........................................................................................................ 134**
**MUHTASARI, HITIMISHO, CHANGAMOTO ZA UTAFITI NA MAPENDEKEZO .. 134**
5.0 Utangulizi........................................................................................................ 134
5.1 Muhtasari ........................................................................................................ 134
5.2 Hitimisho........................................................................................................ 135
5.3 Changamoto Za Utafiti ...................................................................................... 136
5.4 Mapendekezo .................................................................................................... 136
Marejeleo: ............................................................................................................ 138
Kiambatisho “A”........................................................................................................ i
Hojaji........................................................................................................................ i
Kiambatisho “B”.......................................................................................................v
Data Ya Uchanganuzi ...............................................................................................v
Methali Za Kiswahili Zinazorejelea Viumbe Wa Majini ..........................................v

# SURA YA KWANZA

## 1.0 USULI WA MADA YA UTAFITI

Utafiti huu unahusu athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati. Katika kushughulikia hili, tumejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumetumia nadharia ya mahusiano katika utafiti huu.

Utafiti wetu umejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini, ambapo, tumeangazia sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao katika mazingira ambayo methali zimelenga pamoja na umuhimu wa sifa, tabia na maumbile hayo kwa jamii ya binadamu.

Tumetafiti kuhusu uamilifu wa methali hizo husika katika utekelezaji wa majukumu katika jamii, ambamo lugha ya Kiswahili hutumika.

Mazingira ni sehemu muhimu sana katika maisha ya kiumbe yeyote yule duniani kote. Binadamu ni mmoja kati ya viumbe duniani. Binadamu na mazingira yake ni kama pande mbili za sarafu moja, hivyo hawawezi wakatenganishwa.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wakiwarejelea Buliba n.w (2006) wanasema kuwa lugha kama chombo amilifu humwezesha binadamu kuufafanua utamaduni wake kwa misingi ya mazingira aishimo. Katika maelezo haya, tunaona kuwa utamaduni wa jamii fulani huwa umefinyangwa kutoka kwa mazingira ambamo jamii inayozungumza lugha fulani huwa inapatikana. Asasi zote za jamii huchota malighafi yake kutoka kwa mazingira yake.Ndipo mawasiliano yatimie (yafaulu) mazingira ambamo lugha yenyewe huzungumzwa, huwa ni muhimu sana ili kuweza kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa.

Kauli hii inatiliwa nguvu na Kitula na Ndalu (1989) wanaosema haya kuhusu methali:

> …kama methali za lugha nyingine zozote, hurejelea sana maisha na mazingira ya nchini waishimo Waswahili na janibu zake.

Hivyo basi, mazingira huathiri sana lugha ya binadamu. Msamiati autumiao binadamu katika lugha yake hutoka katika mazingira yake. Hii ndiyo sababu kila jamii huchota msamiati wake kutoka kwa mazingira yake. Hali hii inabainika kutokana na ukweli kwamba kutokana na

mazingira fulani ambamo jamii husika hupatikana, utapata msamiati unaorejelea mazingira yake. Kwa mfano, jamii ya Wamaasai, wanaopatikana nchini Kenya na Tanzania wana msamiati wa maneno zaidi ya sita unaorejelea aina za nyasi. Jamii ya Waswahili nayo ina msamiati mpana unaohusishwa na maji na viumbe wa majini. Kutokana na maelezo haya, tunaelewa kuwa mazingira huchangia sana utamaduni wa jamii tumizi-lugha katika eneo fulani. Utafiti huu umelenga kueleza athari za mazingira katika uteuzi wa methali. Tumejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.

Kila kiumbe huwa na tabia fulani katika mazingira yake. Kiumbe yule anapotolewa kutoka kwa mazingira yake na kuwekwa katika mazingira tofauti, si ajabu kwa kiumbe huyo kuweza kubadilisha tabia zake za kawaida ili zioane na mazingira hayo mapya.

Methali ni sehemu muhimu ya fasihi ya jamii yoyote ile. Si ajabu basi kuwa methali hutumiwa na wanajamii katika mazungumzo yao ya kila siku katika shughuli zao mbalimbali. Joon (1992:7) anatuambia kuwa kinyume na tanzu nyingine za fasihi simulizi ambazo hasa zilikusudiwa kuburudisha, methali hunuiwa kurahisisha mawasiliano kwa sababu ya sifa yake ya ufupi. Ni kutokana na ukweli huu ndipo tunachunguza athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati.

Umuhimu wa methali katika jamii nyingi ulimwenguni hauwezi ukatiliwa shaka. Ni wazi kwamba methali ni mali ya jamii ambayo ina uamilifu mkubwa. Andambi (2005) anasema kuwa methali hutumika katika mawasiliano kuonya, kushurutisha, kutia moyo, kukashifu, kuelimisha miongoni mwa mambo mengine. Katika mawanda ya matumizi, methali hutumika katika dini, elimu, utamaduni, michezoni miongoni mwa mazingira mengine ya kijamii. Tunachunguza methali za Kiswahili kutokana na umuhimu ambao methali hutunukiwa na jamii.

Methali za Kiswahili hutumiwa na watu wengi katika eneo la Afrika Mashaiki na Kati. Hali hii inatokana na ukweli kwamba lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa kuliko lugha nyingine za Kiafrika. Kiswahili aidha ni lugha ya taifa, lugha rasmi au lugha ya kibiashara katika mataifa ya Afrika Mashariki. Si ajabu basi kuona kuwa kuna kamusi nyingi za methali za Kiswahili zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kuliko lugha nyingine yoyote ile ya Kiafrika.

Katika utafiti wetu, tumelenga kutoa ufafanuzi wa methali husika kwa kurejelea sifa, tabia na maumbile ya viumbe wa majini. Tumeeleza kama kiumbe aliyetumiwa katika methali husika yuko katika mazingira yake ya kawaida au la.

Utafiti wetu pia umelenga kubaini athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati. Ili tuweze kulishughulikia suala hili la uteuzi wa msamiati vilivyo, tumejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumeangazia athari za msamiati teule katika jamii.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Katika kueleza methali ni nini, utata unaibuka ili kuweza kupata maana moja ya dhana "methali."Wamitila (2001: xiii) anasema kuwa ni vigumu kutoa fasili ya neno methali kwa sababu methali, vitendawili na nahau, ni vipengele vya sanaa ya lugha ambavyo hatimaye vinakutana katika kapu moja linaloitwa "misemo." Utata huu unatokana na ile hali ya kuwepo kwa mshabihiano mkubwa kati ya methali na vipera vingine vya fasihi simulizi.

Naye Finnegan (1983: 393) kuhusu dhana ya methali anasema kuwa:

> Uhusiano wa karibu uliopo kati ya methali na tanzu nyingine za fasihi unazua tatizo. Je, ni kupitia njia ipi hususan ya fasihi simulizi tunaweza kuitofautisha methali kutoka kwa fani nyingine za sanaa simulizi? Au hata kwa mazungumzo ya kawaida na misemo, au semi nyingine zenye mahusiano lakini zenye kutumia mbinu tofauti kama kanuni? (Tafsiri yetu)

Kufuatia fasiri hizi kuhusu dhana ya methali, utafiti wetu umejitokeza na maswali yafuatayo kama tatizo la utafiti hasa kwa kuangazia mazingira na uteuzi wa msamiati utumikao katika kubainisha methali: je, mazingira huchangia vipi uteuzi wa msamiati katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini? Je, msamiati husika huwa umeteuliwa ili kuafikia malengo gani kwa jamii? Je, msamiati ulioteuliwa unatusaidia vipi kuelewa mahusiano na maafikiano ya watu katika jamii inayotumia lugha ya Kiswahili?

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti wetu yamekuwa haya:

i. Kufafanua sifa, tabia na maumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.
ii. Kueleza athari zinazotokana na matumizi ya methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii ambamo lugha ya Kiswahili hutumiwa.
iii. Kuchunguza uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika mazingira mahsusi.

## 1.4 NADHARIA TETE

Nadharia tete katika utafiti wetu zimekuwa hizi:

i. Kunao viumbe wenye maumbile, sifa, na tabia mahsusi ambao kwa mujibu wa wanajamii hutumika katika methali za Kiswahili, na kwamba maumbile, sifa na tabia za viumbe hao zinafaa kwa matumizi ya methali mahsusi katika jamii ya Waswahili.
ii. Athari zinazotokana na matumizi ya msamiati wa Kiswahili unaohusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini zinaonekana.
iii. Methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini huwa na uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu fulani katika mazingira mahsusi.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Lugha ya binadamu hubadilika kila uchao kutokana na maingiliano ya binadamu kutoka janibu mbalimbali. Haya mabadiliko ya lugha huathiri vilevile muonoulimwengu wa watumizi wa lugha. Jambo hili ni la kweli hasa kwa sasa, ambapo kuna athari nyingi kilugha kutokana na utandawazi. Kwa misingi hii, ni fikra zetu kuwa muanda wa methali za Kiswahili hasa zinazohusu viumbe wa majini umeathirika pia. Hili ndilo lengo la utafiti huu, ili kuweza kubaini mkondo ambao methali za Kiswahili zinazohusu viumbe wa majini zinachukua.

Tafiti nyingi kuhusu methali zimefanywa. Nyingi ya tafiti hizo zinabainisha jinsi lugha ya Kiswahili inavyozidi kupanuka katika mawanda ya matumizi yake. Baadhi ya kazi za utafiti wa methali ambazo zimekwisha kufanywa ni kama vile: Karama (1983), Ndalu (1989), Wamitila

(2001), Andambi (2005) King'ei (2008) na Arege (2011). Kadri utafiti unavyozidi kufanywa ndivyo idadi ya methali inavyozidi kuongezeka. Kwa mfano; Wamitila (2001) alikusanya jumla ya methali 2964(elfu mbili mia tisa na sitini na nne), naye Arege (2011) alikusanya methali 3539(elfu tatu mia tano thelathini na sita). Kazi hizi zinaonyesha wazi kuwa methali ni muhimu sana katika jamii na kwa hivyo methali zinapewa uamilifu mkubwa. Utafiti wetu ni muhimu maana utaongeza uhai katika methali za Kiswahili, hasa zinazorejelea viumbe wa majini kwa kuonyesha uhai wa lugha ya Kiswahili. Isitoshe, waandishi tuliowataja hapo juu walizungumzia suala la methali za Kiswahili kwa ujumla wake, kinyume na kazi hii ambayo imemega sehemu ya utamaduni wa Kiswahili na kutaka kuushughulikia kwa kuufungamanisha na methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Utamaduni huu unahusu mahusiano ya Waswahili waishio pwani na viumbe wa majini.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umejikita katika kutafiti methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Katika utafiti wenyewe tumeangalia hasa namna mazingira huathiri uteuzi wa msamiati katika methali hizi za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.

Mtafiti ni mwanafunzi wa Kiswahili ambaye amesomea Kiswahili kutoka darasa la kwanza katika shule ya msingi hadi chuo kikuu. Kutokana na hali hii, mtafiti amekumbana na methali nyingi za Kiswahili zikiwa vitabuni au zikiongewa hadharani. Kwa hiyo, mtafiti ametumia kipawa chake hiki alichojifunza kubaini kama ni ipi methali ya Kiswahili na ni ipi methali kutoka kwingine lakini ambayo imelazimishwa kuingia katika lugha ya Kiswahili kupitia tafsiri. Ni methali za Kiswahili pekee ambazo zimezingatiwa katika utafiti huu. Mtafiti anafahamu mawanda ya Kiswahili, kwa hivyo atatumia vielelezo vya methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kutoka lahaja zote za Kiswahili. Hii ni kwa sababu, methali za lugha yoyote ile hazijikiti katika usanifu wa lugha, bali hunuiwa kuwa mafumbo.

Utafiti wetu umejikita katika msamiati wa viumbe wa majini katika methali za Kiswahili. Hatujajikita katika viumbe vingine vya majini kama vile methali za Kiswahili zinazotumia msamiati wa mimea ya majini.

Kuna baadhi ya methali ambazo ni visawe lakini zinaanza kwa herufi tofauti za kialfabeti. Methali hiyo au hizo zitakuwa sawa na ile ambayo tayari tutakuwa tumeifafanua, ambayo ilitangulia kialfabeti, hivyo basi hatujaifafanua tena ili kuepukana na hali ya kujirudia. Methali kama hizo tumezitaja kisha tumemwelekeza msomaji katika kisawe cha methali hiyo ambayo tayari tulikuwa tumeshaishughulikia. Hali kadhalika, kuna methali zaidi ya moja ambazo zimemrejelea kiumbe fulani. Katika hali hii, hatujarudia kufafanua sifa, tabia na maumbile ya kiumbe huyo tena, bali tumemwelekeza msomaji katika methali ambayo imetumia msamiati wa kiumbe huyo na ambayo tayari tumeshaishughulikia.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Katika utafiti huu, nadharia ya mahusiano ndiyo imetuongoza. Nadharia hii imeasisiwa na Sperber na Wilson (1995). Hii ni nadharia ambayo hushughulika na ufasiri wa matamshi au maandishi ili kupata maana iliyokusudiwa. Tumeitumia nadharia hii katika uchanganuzi wa sifa, tabia na maumbile ya viumbe waliotumiwa katika methali za Kiswahili, athari za msamiati huo pamoja na dhima ya methali hizo zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii tumizi lugha ya Kiswahili.

Chimbuko la nadharia hii lilitokana na udhaifu wa kanuni ya uhusiano katika nadharia ya Grice (1975). Kwa mujibu wa Grice, msemaji ni muhimu katika uteuzi wa maana katika mchakato wa mawasiliano. Hivyo Kulingana na Grice, msikilizaji hutambua maana iliyokusudiwa na mnenaji. Kanuni ya uhusiano kwa kumrejelea msikilizaji katika ufanikishaji wa maana haikutiliwa maanani, ndiposa nadharia hii ya mahusiano ilizuka ili kulitatua tatizo hili.

Katika kutoa fasiri ya kazi neno mahusiano, tunasema kuwa mahusiano ni neno ambalo lina maana kuwa mtu, mnyama, mahali au kitu kina ukuruba wa karibu na mtu, mnyama, mahali au kitu kile anachozungumzia au anachofikiria. Katika misingi hii basi, tunaweza tukazungumza kuhusu mtu aliye na uhusiano fulani na mtu au kitu kingine, swali lililo na uhusiano na dhana fulani au hata hali iliyo na uhusiano fulani na wakati fulani. Kwa mfano, uhusiano uliopo kati ya mafuriko yanayoshuhudiwa mjini Narok na eneo ambalo mji wenyewe umejengwa, pamoja na uzibaji wa mitaro ya kupitisha majitaka.

Sperber na Wilson walinuia nadharia hii ifafanue na kuliweka wazi suala la mahusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Nadharia hii ilikusudia kufafanua kile ambacho hutokea kati ya mzungumzaji na msikilizaji katika mchakato wa mawasiliano.

Sperber na Wilson (2004) wanasema kuwa:

> Tamko lolote linaloelekezewa msikilizaji huwa linawasilisha lengo la mahusiano yake. (Tafsiriyetu).

Kauli hii inamaanisha kuwa mzungumzaji anapoongea, msikilizaji anaelewa lengo la kutumia maneno yaliyotumiwa. Hivyo basi, mahusiano yanakuwepo moja kwa moja kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

Katika nadharia ya mahusiano utambuzi ambao upo akilini mwa binadamu ni muhimu katika kuelewa lugha ya binadamu kupitia mawasiliano. Kwa mfano, msikilizaji anapotajiwa methali ya Kiswahili inayorejelea kiumbe wa majini akiwa kazini au nyumbani, ataichanganua methali hiyo kutegemea mazingira aliyomo kwa kujikita katika athari zake za kiutambuzi pamoja na uhusiano wake na mzungumzaji. Sperber na Wilson (1986 na 1995) wanasema kwamba lengo kuu la pragmatiki ni kufafanua kile ambacho msikilizaji husikia kutoka kwa kile ambacho mzungumzaji alikusudia kwa kujikita katika ushahidi uliopo.

Katika nadharia ya mahusiano, msikilizaji hukisia lengo la mzungumzaji kwa kujikita katika muktadha wa mawasiliano. Msikilizaji anapopata lengo la mzungumzaji habari ya kuwasiliana aliyokusudia mzungumzaji inakuwa rahisi kueleweka. Kutokana na maelezo haya kanuni ya uhusiano katika mchakato wa mawasiliano huwaongoza washiriki; yaani mzungumzaji na msikilizaji wake.

Hivyo basi, kama asemavyo Mang'eni (2008) kuwa katika mchakato wa mawasiliano, mzungumzaji hunuia kumfanya msikilizaji wake aelewe barabara kile anachokizungumzia. Hata hivyo, huenda lengo la mzungumzaji lisifaulu vilivyo kutokana na ukweli kwamba akili ya binadamu yaweza ikawa na mseto wa habari. Kutokana na hali hii, huenda msikilizaji asiipate maana kama ilivyokusudiwa na mzungumzaji. Nadharia hii inakubaliana na hali hii ya msikilizaji kutopata maana kama alivyokusudia mzungumzaji kwa kuyatumia maneno

aliyoyatamka. Hata hivyo, msikilizaji atatumia kanuni ya uhusiano ili kupata maana iliyokusudiwa na mnenaji kwa kuihusisha na mzungumzaji. Katika maelezo haya tunaona kwamba uhusiano kati ya mzungumaji na msikilizaji ni muhimu sana katika kubainisha maana katika muktadha wa mazungumzo. Umuhimu huu wa kutambua maana iliyokusudiwa na mzungumaji kwa kutumia kanuni ya uhusiano pia inatambuliwa na nadharia hii.

Muktadha wa mazungumzo ni muhimu katika kufanikisha maana iliyokusudiwa na mzungumzaji. Muktadha wa mazungumzo huwezesha utimilifu wa kanuni ya mahusiano. Msikilizaji huwa na chukulizi zake kutegemea muktadha wa mazungumzo, na huenda chukulizi hizo za msikilizaji zikathibitishwa na kupata nguvu zaidi, au zikafifia au zikapotea huku msikilizajiakipata chukulizi mpya kutokana na muktadha huo wa mazungumzo. Habari hiyo mpya anayoipata msikilizaji hufasiriwa na kuwekwa ubongoni. Asipoitumia habari hiyo kwa muda, habari hiyo hupotea.Sperber na Wilson (1995) wanasema kuwa:

> Kwa kujikita katika chukulizi alizo nazo, msikilizaji anapata habari mpya ambayo huenda ikapotea kabisa kama haina mtiririko katika habari hizo mpya au kama chukulizi hizo aidha zimesahaulika au kuhifadhiwa katika sehemu tofauti ya ubongo wa msikilizaji.(Tafsiri yetu)

Katika suala la mawasiliano, Sperber na Wilson (2004) wanasema kuwa kanuni hii hudhihirisha uhusiano wake wa kipekee.

Litakuwa jambo la busara tukizifafanua dhana muhimu katika nadharia hii ya mahusiano, kisha tueleze manufaa ya nadharia hii katika utafiti wetu.

### 1.7.1 DHANA MUHIMU KATIKA NADHARIA YA MAHUSIANO

Nadharia ya mahusiano ina dhana tatu muhimu ambazo ni:

i. Utambuzi
ii. Mawasiliano
iii. Uelewa

## i. MAHUSIANO NA UTAMBUZI

Utambuzi ni dhana inayohusu akili ya binadamu. Kwa kawaida, kila binadamu hujishughulisha na yale mambo tu ambayo ni muhimu kwake. Mzungumzaji na msikilizaji wanapokutana, hali ya kukisia maana itokanayo na tamko fulani huwepo. Hali hii husababishwa na mahusiano ambayo huwafanya washiriki watambue hali ya kukisia maana itokanayo na tamko fulani kutoka kwa mzungumzaji.

Utambuzi na mahusiano basi ni vitu viwili ambavyo haviwezi vikatenganishwa. Ni sawa na pande mbili za sarafu moja. Wakati mtu anapozungumza matarajio ya mahusiano pia yanaibuka. Lengo la mnenaji la kumjuza msikilizaji kuhusu jambo fulani hukamilika (hufaulu) pale ambapo chukulizi za msikilizaji ni sehemu ya utamaduni wake. Ukweli huu unakaririwa na Sperber na Wilson (2004) wanaposema:

> Kanuni ya utambuzi wa mahusiano inachukuliwa kuwa: utambuzi wa binadamu hutegemea ufanisi wa hali ya juu wa mahusiano. (Tafsiri yetu)

Binadamu kote duniani huwa na mawazo. Huwa na chukulizi fulani kuhusu dhana fulani. Chukulizi hizi huwapelekea watu kufanya maamuzi. Hali zote hizi hutokana na athari za kiutambuzi. Sperber na Wilson wanataja aina tatu za athari za kiutambuzi:

i. Utambuzi wa kimuktadha. Athari hii ya kiutambuzi huu hupelekea mtu kupata habari mpya zilizotokana na chukulizi za awali.
ii. Kutilia nguvu chukulizi zilizopo. Athari hii hupelekea kuweka wazi chukulizi za kitambo zilizokuwepo katika akili ya mtu kuhusu mtu, kitu au hali fulani.
iii. Athari ya kuondoa au kupunguza chukulizi zilizokuwapo. Katika athari hii, chukulizi za awali huweza kuondolewa au kupunguzwa kutegemea habari mpya inayopatikana katika muktadha wa mawasiliano.

Hebu tutoe mfano ili tuthibitishe aina hizi tatu za athari za kiutambuzi.

Mtu akikuambia, “Juma alivunjika mguu.” Kuna njia tatu ambazo kwazo sentensi hii inaweza kuchanganuliwa:

i. Juma amefungwa kitata mguuni. Msikilizaji anakuwa na chukulizi kuwa mzungumzaji anajua Juma amevunjika mguu. Juma amefungwa kitata mguuni kwa sababu amevunjika mguu. Kwa hivyo, msikilizaji anapata habari hii mpya kuwa Juma amevunjika mguu.
ii. Mzungumzaji alikuwa hospitalini Juma alipokuwa akitibiwa. Chukulizi hii inaongeza nguvu ile iliyokuwepo. Hivyo basi msikilizaji hatakuwa na mashaka yoyote kuhusu kuvunjika mguu kwa Juma.
iii. Mzungumzaji akisema kuwa Juma alivunjika mguu naye msikilizaji aseme, “lakini nimempata akicheza mpira uwanjani” inakuwa ni sentensi ambayo inaondoa au kupunguza athari za ile sentensi ya mzungumzaji.

Kutokana na mfano tuliotoa pamoja na maelezo yake, tunapata uelewa kwamba mazungumzo katika mchakato wa mawasiliano hukisiwa kuwa muhimu kutegemea athari za kiutambuzi za msikilizaji. Msikilizaji hutilia maanani kile kilicho muhimu tu katika mchakato wa mawasiliano na kukihifadhi akilini mwake.

### ii. MAHUSIANO NA MAWASILIANO

Mang’eni (2008:13) akimrejelea Schroeder (2002/2008) anasema kuwa vitendo vya mawasiliano na athari tunazozipata kutoka kwa vitendo vinatupa (vinafaulisha) mahusiano.

Ili kuweza kutilia nguvu maoni haya kuhusu mawasiliano na mahusiano, hebu tutoe mfano wa sentensi. Sentensi yenyewe ni:

Yohana: Wakati wa kucheza umefika.

Katana: Mpira unaletwa na Hamisi.

Katika sentensi ya kwanza, Yohana anatoa kauli kuwa wakati wa kucheza umefika. Yohana ana chukulizi kwamba Katana ataelewa kuwa anataka kuingia uwanjani kucheza. Kwa kutoa kauli hii, Yohana basi anatarajia kuwa Katana, ambaye huwa na mpira atakubaliana naye. Katika sentensi inayonenwa na Katana, tunaona wazi kuwa amekubaliana na kauli hiyo ya Yohana. Katana kwa mujibu wa kauli ya Yohana anapata uhusiano uliopo kati ya matamshi hayo ya

Yohana na wakati. Katika mfano tulioutoa hapo juu, tunapata uhalisi kuwa mawasiliano yanaweza yakawa ya wazi, hivyo maana iliyokusudiwa inaeleweka moja kwa moja.

Sperber na Wilson (2004: 612) wanasema yafuatayo kuhusiana na kanuni ya mawasiliano katika mahusiano;

> Kila kichocheo ambacho si halisi hubainisha mojawapo ya chukulizi za mahusiano zilizo bora zaidi. (Tafsiri yetu)

Ndipo mawasiliano yafanikiwe, majukumu mawili ni muhimu katika dhana hii ya mahusiano na mawasiliano.

i. Habari ya kuwasiliana.
   Kwa mujibu wa Blass (2007), jukumu hili hukusudia kuwasilisha habari fulani kwa msikilizaji. Jukumu hili la kuwasilisha habari hujikita katika vitendo ambavyo mzungumzaji hufanya ili kuweka wazi malengo yake.
ii. Lengo la kuwasiliana.
   Lengo la kuwasiliana linahusu hali ya kuafikia kufaulu kwa habari ya kuwasiliana. Mzungumzaji na msikilizaji wanapokutana, wanakumbwa na mzigo wa kuwasiliana. Mzungumzaji anapozungumza panakuwa na matarajio ambayo humwongoza msikilizaji kuafiki kilichokusudiwa na mzungumzaji.

Blass (2007) anaeleza lengo la kuwasiliana kuwa:

> Juhudi azifanyazo mzungumzaji ili habari ya kuwasiliana aliyo nayo itambulike na msikilizaji. (Tafsiri yetu).

Katika mawasiliano huenda maana iliyokusudiwa msikilizaji ikatimia au ikakosa kutimia. Hebu tutoe ufafanuzi kwa kutumia mfano huu:

Ukifika nyumbani wakati wa chamcha, mpishi atakupakulia chakula ili ule. Ukimaliza kula na uwe hujashiba, utaisogeza sahani yako mezani kama ishara ya kutaka nyongeza. Mpishi kwa upande wake huenda akafasiri ishara hiyo kuwa umeshiba na kwa hivyo ataiondoa sahani yako mezani. Kusogeza sahani peke yake hakutoshi kuupitisha ujumbe ulioukusudia, hivyo basi lengo

la kuwasiliana linakosa kufaulu kuipitisha habari kama ilivyokusudia; yaani kuongezewa chakula. Ili maana uliyoikusudia ifaulu, itafaa uishike ile sahani na kuitikisa huku ukiwa umeielekeza upande ule aliko mpishi. Kwa kufanya hivi, lengo la kuwasiliana litafaulu kupitisha habari ya mawasiliano. Mpishi ataelewa kuwa unataka nyongeza.

Kutokana na mfano huu tulioutoa, huenda mtu aliyekusudiwa kupata maana fulani katika ujumbe akaipata maana hiyo hiyo au akapata maana nyingine. Maana anayoipata msikilizaji hutokana na chukulizi alizo nazo pamoja na mahusiano yake na mzungumzaji katika muktadha wa mawasiliano. Kwa hivyo, namna ujumbe utakavyopokelewa na kufasiriwa ni muhimu katika kuakisi maana iliyokusudiwa na mzungumzaji. Katika mkondo wa mawasiliano, mzungumzaji atawasilisha ule ujumbe ambao anaamini kuwa ni muhimu kwa msikilizaji, kama anavyosema Blakemore (1987: 48) kuwa:

> Haina maana kwa mzungumzaji kupitisha habari kwa msikilizaji ila tu pale mzungumzaji anapojua kuwa ujumbe huo utakuwa na athari za kiutambuzi katika chukulizi ambazo msikilizaji tayari anazo. (Tafsiri yetu)

Katika maoni haya ya Blakemore tunapata ukweli tunaporejelea dhana ya utambuzi na mahusiano ambayo tumekwisha kuieleza. Athari za kiutambuzi za msikilizaji hutegemea chukulizi ambazo tayari anazo.

Sperber na Wilson (2004:13) wanasema kuwa msikilizaji anapopata habari mpya chukulizi zake aidha:

i. Zitapata nguvu.
ii. Zitapunguza nguvu
iii. Zitaondolewa katika kamusi ya uhifadhi katika ubongo wa msikilizaji.

Mambo haya matatu kuhusu chukulizi hutegemea muktadha wa mawasiliano na muonoulimwengu wa msikilizaji.

Blakemore (1987) anatilia nguvu suala hili anaposema kuwa chukulizi ambazo msikilizaji tayari huwa nazo hupinga, huondolewa au huthibitisha ile habari anayoipata kutoka kwa mzungumzaji. Huenda msikilizaji akapata au akajenga chukulizi mpya kutoka kwa habari mpya ambayo

ameipata kutoka kwa mzungumzaji. Chukulizi hizi mpya huenda zikawa kinyume na chukulizi zake za hapo awali.

Kwa mujibu wa Sperber na Wilson (2004), mahusianao yafaayo katika mawasiliano yatafaulu iwapo masuala haya yatazingatiwa;

i. Msikilizaji atumie mbinu ambayo haitakuwa na gharama kubwa ya mawasiliano katika kuafikia athari za kiutambuzi.
ii. Msikilizaji asizidi kuchanganua habari aliyoipata akisharidhika kuwa matarajio ya mahusiano yameafikiwa.

Masuala haya mawili yakiafikiwa na msikilizaji, basi mzungumzaji atakuwa amefaulu kuwasilisha maana aliyoikusudia kwa msikilizaji wake; kwamba mahusiano yafaayo zaidi yameafikiwa kwa kutumia gharama ya chini ya mawasiliano katika uchanganuzi na uelewa wa maana iliyokusudiwa.

### iii. MAHUSIANO NA UELEWA

Watu wanapozungumza, kiwango chao cha uhusiano hutarajiwa. Katika mchakato wa mawasiliano, mzungumzaji atampima msikilizaji wake kwa kutumia mbinu kadhaa ili gharama kubwa ya mawasiliano iepukike. Mbinu hizo ni kama vile ishara za uso, ishara za mikono na miondoko ambayo itamwelekeza msikilizaji kupata lengo la mzungumzaji. (Mang'eni 2008:16). Msikilizaji naye, kwa kutegemea ishara za mzungumzaji atakuwa na swali, 'je, anamaanisha nini?' Hivyo basi, katika mchakato wa mawasiliano, panakuwa na jitihada za kiutambuzi katika kuchanganua ujumbe unaowasilishwa na ishara ili kupata maana iliyokusudiwa.

Hii ndiyo sababu Sperber na Wilson (2004:13) kama tulivyokwisha kueleza kwamba mahusiano yafaayo yatatimia ikiwa:

i. Msikilizaji atatumia mbinu ambayo haitakuwa na gharama kubwa ya mawasiliano katika kuafikia athari za kiutambuzi.
ii. Msikilizaji hatazidi kuchangaanua habari aliyoipata akisharidhika kuwa matarajio ya mahusiano yameafikiwa.

Tunapozungumza kutumia sauti, tunaangazia mantiki kutoka kwa taarifa (usemi) ya mzungumzaji. Mpangilio wa maneno hutuwezesha kupata maana iliyokusudiwa. Iwapo tutatumia ishara zisizo za kutumia sauti, itatubidi kuchunza ile habari ambayo ni muhimu kwetu.

Kwa kurejelea mfano tulioutoa kuhusu sahani wakati wa kishuka, itakubidi uishike sahani yako, uitikise huku ukiielekeza kwa mpishi ndipo ujumbe ulioukusudia ueleweke. Fauka ya hayo, tamko kama, "niongezee tafadhali" litatilia nguvu lengo lako. Kuisogeza sahani mezani peke yake huenda kusibainishe lengo lako. Huenda mpishi akawa na chukulizi kuwa umeshiba, na kwa hivyo kuiondoa sahani mezani.

Sperber na Wilson (2004) wanasema kuwa kunazo njia mbili ambazo kwazo jambo linaweza likasemwa:

i. Kusema kwa njia iliyo wazi.
ii. Kusema kwa njia fiche (kimafumbo)

Katika kuelewa maana zilizo katika njia mbili hizi, Sperber na Wilson (2004) wanaendelea kusema kwamba mambo yafuatayo hufanyika:

i. Habari iliyo wazi hukisiwa maana kupitia urejelezi wa muktadha, ufasiri wa msamiati uliotumika au kwa kuchuja maana nyingine za usemi ili kubaki na maana iliyokusudiwa. Kwa kutumia njia hii, malengo ya mzungumzaji huafikiwa na msikilizaji wake pasi na taabu yoyote. Hivyo basi, msikilizji anaepushwa gharama kubwa ya kufasiri maana.
ii. Kukisia kilichokusudiwa na mzungumzaji katika muktadha wa mazungumzo. Katika hali hii msikilizaji huhitaji kufanya juhudi kubwa ya kuuchanganua ujumbe ili kupata uelewa wa kile mzungumzaji alichokusudia. Hii ni kwa sababu usemaji kwa njia ya kimafumbo huwa umeficha maana. Msikilizaji basi hatakuwa na budi ila kujikita katika muktadha wa mazungumzo ili aweze kuifasiri maana iliyokusudiwa na mnenaji.
iii. Kukisia maana hutegemea hitimisho lililopatikana kutokana na usemi wa kimafumbo. Katika kauli hii, maana ambayo imeeleweka na msikilizaji hutokana na ufasiri wa

usemi wa kimafumbo. Ufasiri huu utatumiwa na msikilizaji katika kuelewa maana ya kinachozungumziwa kwenye mazungumzo mengine ya kimafumbo.

Ni vyema tukitaja hapa kuwa si lazima uelewa upatikane kwa kufuata njia hizi tatu tulizozitaja hapo juu. Uelewa ni mchakato wa kiutambuzi ambao umo akilini mwa msikilizaji. Msikilizaji hujiamulia maana atakayoitambua kutegemea chukulizi zake za awali kwa mujibu wa muonoulimwengu wake.

Blass (2007) akiwarejelea Sperber (1994)na Wilson (1999) anaeleza kuhusu aina za wasikilizaji:

i. Wasikilizji wenye matarajio ya ukweli. Hawa ni wasikilizaji ambao hukisia kuwa habari wanayopata kutoka kwa mzungumzaji ni ya kweli na inatosha. Hivyo basi inafaa kuwa jinsi mzungumzaji alivyoikusudia iwe.
ii. Wasikilizaji wenye tahadhari. Hawa ni wasikilizaji ambao hutambua udhaifu wa mzungumzaji katika uwasilishaji wa habari yenye uhusiano ufaao.
iii. Wasikilizaji changamano. Hawa ni wasikilizaji ambao ufasiri wao wa habari hung’amua kasoro katika mazungumzo. Hivyo basi, ishara au usemi ulio na upungufu habainishwa na msikilizaji.

### 1.7.2 UMUHIMU WA NADHARIA YA MAHUSIANO KATIKA UTAFITI HUU

Nadharia ya mahusiano imetuongoza katika utafiti wetu. Methali hukusudiwa kutumiwa kwa kusudi la kuwasiliana; na inapotumika huwa na athari fulani kwa msikilizaji. Nadharia hii imetuongoza katika ufafanuzi wa mahusiano yaliyopo kati ya jamii ya Waswahili na mazingira ambamo jamii hiyo hupatikana.

Isitoshe, tumeitumia nadharia hii kueleza kuhusu uhusiano uliopo kati ya sifa, tabia na maumbile ya viumbe wa majini wanaoteuliwa na kutumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini na mazingira ambamo matumizi ya methali hizo yanarejelea. Kwa misingi hii, nadharia hii imetuongoza katika kuufafanua uhusiano huo wa msamiati wa viumbe hao na mazingira, na ni vipi uhusiano huo unaakisi matumizi ya msamiati wa viumbe hao katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.

Nadharia hii hali kadhalika imetuongoza katika ufafanuzi wa mahusiano na maafikiano ya watu katika jamii inayotumia lugha ya Kiswahili kwa kujikita katika msamiati wa viumbe wa majini wanaotumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Fauka ya hayo, nadharia hii imetufaa katika ufafanuzi wa uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii itumiayo lugha ya Kiswahili, pamoja na athari zitokanazo na matumizi ya methali zenyewe kwa kueleza dhana au hali fulani huhusishwa na methali gani inayorejelea viumbe wa majini.

## 1.8 . YALIYOANDIKWA KUHUSIANA NA MADA

Sankan (1971) ameangazia masuala ya jamii ya Wamaasai kwa ujumla wake. Mojawapo ya sehemu ambazo Sankan amezishughulikia ni ile ya fasihi simulizi ya jamii ya Wamaasai. Kati ya tanzu za fasihi simulizi ambazo zimeshughulikiwa ni mafumbo, vitendawili na methali. Katika utanzu wa methali, Sankan anaziorodhesha bila kutumia mbinu yoyote maalum ya uainishaji. Hali kadhalika, methali zimeorodheshwa tu bila kutolewa ufafanuzi wowote, hali ambayo huenda ikamkwaza msomaji ambaye hazielewi methali za Kimaasai; hasa ikizingatiwa kuwa katika kazi hii, methali hizo zimetafsiriwa katika lugha ya Kiingereza, hivyo utata unaofungamanishwa na utamaduni wa jamii ya Wamaasai na mazingira yao unaibuka kwa msomaji ambaye hafahamu kuhusu utamaduni na mazingira ya jamii ya Wamaasai. Isitoshe, kazi hii imezungumzia masuala muhimu ya jamii ya Wamaasai, hivyo inakosa uketo wa kina kuhusu suala fulani mahsusi.

Tofauti na kazi hii ya Sankan, utafiti wetu umejikita katika utanzu mmoja wa methali peke yake ambapo tumejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini na wala si methali zote za Kiswahili kwa ujumla wake. Tumeshughulikia msamiati uliotumika katika methali hizi kwa kuangazia vile mazingira yanavyooanishwa na sifa, tabia na maumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumika katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe hao wa majini.

Scheven (1981) ametafsiri methali za Kiswahili kwa lugha ya Kiingereza. Kazi hiyo imeainishwa kwa kigezo cha maudhui. Katika mtindo wake huu wa kuainisha methali kimaudhui, Scheven anaibuka na makundi madogomadogo hamsini na sita ya kimaudhui. Katika

kila kundi anaorodhesha methali ambazo zinaafiki kikundi hicho. Kazi hiyo pia imeshughulikia maneno magumu katika methali hizo, na pia kutoa ufafanuzi wa methali zenyewe. Isitoshe, kazi hii imeongeza methali kutoka lugha nyingine, hasa lugha ya Kiingereza ambazo zina uamilifu sawa wa kimaudhui na zile  za Kiswahili. Lengo lake likiwa ni kusahilisha uelewa wa methali hizo kwa wasomaji wake. Hata hivyo, kama asemavyo Wamitila (2001: vii) kwamba utaratibu alioutumia Scheven una udhaifu unaotokana na ukweli kwamba baadhi ya methali za Kiswahili huwa na maana mbalimbali, jambo linalozua utata mkubwa kwa uainishaji wa aina hii.

Tofauti na Scheven, utafiti wetu umejikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumefafanua sifa, tabia na maumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali hizo husika.

King'ei (1982) ni tasnifu ambayo imehakiki methali za Kikamba kwa kufuatisha misingi ya methali za Kiswahili. Katika kazi hii, masuala muhimu katika uhakiki wa methali yameshughulikiwa kama vile: chimbuko la methali, mtindo na sifa mbalimbali za kifasihi na kiisimu katika methali, matumizi ya methali, majukumu ya methali miongoni mwa mambo mengine. Hali kadhalika, kazi hii inatoa maelezo muhimu kuhusu jamii ya Wakamba kwa ujumla wake. Maelezo hayo ni kuhusu historia, utamaduni, mila na ada mbalimbali miongoni mwa mambo mengine yanayohusu jamii ya Wakamba. Licha ya uhakiki huu, kazi hii ina udhaifu kwa kuwa mtafiti amejaribu kuyaangalia mambo mengi sana, kwa hiyo hakuzihakiki methali hizo kwa kina.

Utafiti wetu kwa upande wake umeshughulikia methali za Kiswahili. Katika methali hizi tumejikita katika methali zinazorejelea viumbe wa majini. Tumeufafanua msamiati wa viumbe hao kwa kuangazia sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao waliotumiwa katika methali hizo kwa mujibu wa mazingira ambamo methali hizo zimetumika.

Arege (2011) ni kamusi ya methali ambayo imekusanya methali 3536(elfu tatu mia tano thelathini naa sita). Methali hizi ni za Kiswahili. Katika kazi hii, methali zimeorodheshwa kialfabeti. Katika sehemu ya utangulizi, kuna maelezo yanayohusu methali katika ujumla wake. Maelezo hayo yanahusu maana, sifa, dhima za methali pamoja na njia za kuainisha methali. Katika uainishaji, vigezo vya majukumu au uamilifu, dhamira, herufi za mwanzo au alfabeti,

muundo wa methali kutegemea sauti za kati na za mwisho na matumizi ya lugha kama sitiari na tashbihi zinaelezwa kama njia za kuainishia methali.

Kazi hii ina umuhimu kwa kuwa inaonyesha uhai uliopo katika lugha. Inabainika moja kwa moja kuwa methali zinaendelea kuongezeka kila uchao. Hii ndiyo kazi ya karibuni zaidi katika ukusanyaji wa methali za Kiswahili ambayo tumekumbana nayo.

Tofauti iliyopo baina ya kazi hii na utafiti huu ni kuwa Arege amezishughulikia methali kwa ujumla wake bila kuzitolea methali hizo husika maelezo ya kina kwa kurejelea msamiati wa maneno yanayotumika kuziunda methali hizo. Utafiti wetu umehusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumefafanua sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao waliotumiwa katika methali hizo kwa kuwafungamanisha na mazingira yao, ili tupate uelewa wa athari za msamiati huo kwa jamii tumizi lugha.

Karama, S. na Saidi M. (1983) nikazi ambayo methali za Kiswahili zimekusanywa, maana zake kuelezwa pamoja na matumizi yake. Licha ya kufanya hivi, kazi hii haijatoa ufafanuzi wa msamiati uliotumika, na athari zake katika mazingira ya watumizi lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu umelenga kuufafanua msamiati uliotumika katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini pamoja na athari zake katika mazingira ya watumizi lugha ya Kiswahili.

Wamitila, K.W. (2001) amezitalii methali za Kiswahili kwa kina. Katika kamusi hii ya methali, Wamitila ameshughulikia methali zaidi ya elfu mbili na mia tisa, ambazo amezikusanya, akaeleza maana zake pamoja na matumizi ya methali hizo. Pia, katika sehemu za dibaji na utangulizi tunapata maelezo yakinifu kuhusu methali. Kazi hii imekuwa mhimili muhimu sana katika utafiti wetu, kwa sababu ya idadi kubwa ya methali zinazorejelea viumbe wa majini na ambazo tumezitumia ili kuweza kutoa maelezo yakinifu na ya kina kuhusu tabia, sifa na maumbile ya viumbe katika utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wetu kinyume na kazi hii utahusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini na wala si methali zote kwa ujumla wake.

Andambi na Murono (2005) pia ni kazi ambayo imekuwa muhimu sana katika utafiti wetu. Kazi hii, licha ya kuzikusanya methali za Kiswahili, imeziainisha katika makundi ya nomino ambazo zimetumika katika kuziunda methali husika. Katika uainishaji wao, tunapata makundi ya methali zinazorejelea sehemu za mwili, wanyama, hali, ndege, wadudu, mimea na matunda, samaki na

wanyama wa majini na methali nyinginezo. Kazi hii pia imeshughulikia maana na matumizi ya methali hizo. Fauka ya hayo, kazi hiyo imetoa malengo mbalimbali ambayo methali zenyewe zimekusudia kutekeleza; kama vile kushutumu, kushauri, kuliwaza, kuonya kuhimiza na kadhalika. Kazi hii imekuwa ya muhimu sana kwetu, kwa sababu ya uainishaji wa methali katika makundi. Hata hivyo tofauti na kazi hii, utafiti wetu umejikita katika kundi moja tu, lile linalohusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.

Joon (1992) katika tasnifu yake, amehakiki methali za Kikorea na za Kiswahili. Katika kazi hii, Joon ameainisha methali katika umuhimu uliochukukuliwa na jamii kuwa wa manufaa. Joon (1992:71-74) akimrejelea C.L. Sibusiso Nyembezi (1963), aliziainisha methali za Kizulu, katika makundi makuu pamoja na vijikundi vidogo vidogo chini ya makundi makuu. Jambo ambalo uainishaji huu haukuzingatia, ni kuufafanua uteuzi wa msamiati ambao ungefaa kutumika katika methali, ili ioane na hali halisi ya mazingira ambamo methali hiyo inafaa, kwa kurejelea sifa na tabia za viumbe ambao wametumika katika methali hizo. Kazi yetu imejaribu kueleza kuhusu uteuzi wa msamiati ambao unafaa katika mazingira fulani kwa kutumia nadharia ya mahusiano. Hata hivyo, uainishaji huu umekuwa wa manufaa kwetu katika kuelewa mazingira ambamo methali husika ilifaa zaidi.

Finnegan (1983) ameshughulikia tanzu za fasihi simulizi katika bara la Afrika kwa ujumla wake kwa kujikita katika jamii za kutoka Afrika Magharibi na kusini mwa Afrika. Baadhi ya tanzu alizozishughulikia ni ushairi, vitendawili na methali. Katika utanzu wa methali, kazi hii inafafanua umuhimu wa methali katika jamii za Kiafrika. Isitoshe, mtindo na muundo wa methali za Kiafrika umeshughulikiwa. Kati ya makundi ya methali anazozizungumzia Finnegan ni zile zenye msamiati wa wanyama na ndege. Anaendelea kuzungumzia kuhusu ujumlishaji wa majukumu ya methali na hali ya maisha ya kila siku katika jamii. Hata hivyo, kazi hii haikushughulikia methali katika eneo la Afrika Mashariki ambamo lugha ya Kiswahili hutumiwa na watu wengi.

Utafiti wetu umejikita katika athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati, ambapo tumeufafanua msamiati katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kwa kutoa maelezo kuhusu sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao walioteuliwa na kutumika katika methali hizo.

Kipury (1983) ni kazi ambayo imerejelea fasihi ya Kimaasai kwa ujumla wake. Kati ya tanzu zilizoshughulikiwa katika kazi hii ni ule wa methali, ambapo methali mia tatu na ishirini zimekusanywa na kuainishwa. Kipury ameziainisha methali kiuamilifu. Amezigawa methali hizo katika makundi thelathini na matatu ya kiuamilifu. Chini ya kila kikundi, methali zinazohusiana na uamilifu huo zimeorodheshwa. Katika kazi hiyo, methali zimeandikwa kwa lugha ya Kimaasai kisha tafsiri pamoja na ufafanuzi kwa lugha ya Kiingereza unatolewa kwa ujumla wake bila kuufafanua msamiati uliotumika. Ni baadhi tu ya methali ambazo zimefafafuniliwa katika kazihii, huku methali nyingine zikiwa zimeorodheshwa tu pamoja na tafsiri za methali hizo. Upungufu wa kazi hiyo ni kuwa imeshughulikia makundi mengi ya methali, kwa hivyo maelezo ya kina kuhusu methali zenyewe yanakosekana.

Kazi yetu imejikita katika kundi moja tu la methali zinazorejelea viumbe wa majini. Tumeangazia athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati kwa kutoa maelezo kuhusu sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao walioteuliwa na kutumika katika methali hizo.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Katika mbinu za utafiti, tutaangazia mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

### 1.9.1 MAHALI PA UTAFITI

Utafiti wetu umejikita maktabani na pia nyanjani. Utafiti wa maktabani umetuongoza kupata kazi zinazohusiana na mada ambayo tumeshughulikia. Tumesoma vitabu na makala ya mtandao yanayotoa maelezo kuhusu fasihi simulizi hasa utanzu wa methali ili kutupa mwanga zaidi kuhusu utanzu wa methali ambazo tumetafiti. Kazi za maktabani pia zimetupa ufafanuzi kuhusu mihimili ya nadharia ambayo tumetumia katika utafiti wetu, na namna tunayopaswa kuitumia. Tumeangalia pia tasnifu mbalimbali zinazohusiana na methali ili kupata yale yaliyofanywa na wasomi wengine ili tupate mwongozo katika ufafanuzi wa mada yetu.

Isitoshe, katika utafiti wa maktabani tumefafanua msamiati uliotumika katika methali hizi tukijikita hasa kwenye sifa, tabia na maumbile ya viumbe ambao wameteuliwa na kutumiwa katika methali hizo. Tumetumia kamusi mbalimbali za methali za Kiswahili na za lugha ili kupata maoni na maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu msamiati ambao umetumika katika

methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumeifafanua kila methali kivyake ili kupata mahusiano ya msamiati uliotumika na mazingira ya matumizi.

Kule nyanjani tumefanya utafiti ili tuelewe kuhusu athari za msamiati huo teule kwa jamii tumizi lugha ya Kiswahili. Athari hizi zimetuelekeza kuelewa uamilifu wa majukumu ya methali zenye msamiati unaorejelea viumbe wa majini katika jamii.

#### 1.9.1.1 UTEUZI WA SAMPULI

Sampuli ambayo tumetumia ni sampuli lengwa ambayo ni methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini.

Mugenda na Mugenda (2003), wanasema kuwa aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudia kupata habari za kina na bila kujumlisha.

Kwa kurejelea haya maelezo, tumechaguamethali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kimakusudi.Methali hizi zimetufaa kupata habari za kina kuhusu suala ambalo tumelichunguza la athari ya mazingira katika uteuzi wa msamiati. Hii ni kwa sababu methali hizi zina uzito katika suala la uteuzi na athari za mazingira.

### 1.9.2 UKUSANYAJI DATA

Methali hizi tulizoteua katika utafiti huu zimefafanuliwa kwa njia ya maelezo. Methali sitini na nne zimekusanywa kutoka kwa kamusi za methali, kisha zimechunguzwa ili kubaini msamiati na uamilifu wa methali hizo ambazo zina msamiati unaorejelea viumbe wa majini katika mazingira ya jamii. Aidha, tumetumia hojaji ili kupata uelewa wa athari wa matumizi ya methali husika katika jamii ambayo hutumia lugha ya Kiswahili. Tuliwapa wanajamii hamsini ambao hutumia lugha ya Kiswahili wajaze hojaji katika shule za msingi na upili za Naikarra, katika kijiji cha Naikarra kilichoko katika tarafa ya Masai Mara kaunti ya Narok.

#### 1.9.2.1. UCHANGANUZI WA DATA

Data tuliyoipata tumeichanganua kwa njia ya maelezo kulingana na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ambayo tumetumia. Kwa kutumia msingi wa nadharia ya mahusiano, tumechanganua athari zinazojitokeza katika methali hizi. Kwa kutumia kanuni za utambuzi,

mawasiliano na uelewa katika nadharia ya mahusiano; tumeeleza ni sababu gani thabiti tunayotoa ili kuainisha msamiati husika kuwa unafaa katika mazingira mahsusi. Aidha, tumeeleza iwapo msamiati husika unaotumika kwenye methali hizi unatoa athari chanya au hasi kwa mtu binafsi au kwa jamii. Hii ni kwa sababu hiki ni kigezo mojawapo cha kuainisha athari kwa mujibu wa nadharia tunayotumia.

### 1.9.3. UWASILISHAJI WA DATA

Baada ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo ya data umefanywa kwa njia ya ufafanuzi, majedwali ya takwimu, kwa kutumia pai chati na baa grafu.

### 1.9.4 WALENGWA

Walengwa ni jamii tumizi lugha ya Kiswahili. Tumewalenga wanajamii ambao ni walimu na wafanyakazi katika shule ya msingi ya Naikarra na shule ya upili ya Naikarra, ambao idadi yao ni 50. Walimu na wafanyakazi ambao tumewalenga wametoka sehemu tofautitofauti za taifa la Kenya, kwa hivyo watakuwa kielelezo kizuri cha jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika katika maeneo mbalimbali ya taifa la Kenya. Shule hizi zimo katika kijiji cha Naikarra, tarafa ya Masai Mara kaunti ya Narok.

# SURA YA PILI

## DHANA MUHIMU KATIKA TAALUMA YA METHALI

### 2.0 UTANGULIZI

Itakuwa vyema tukiweka bayana masuala ambayo yatakuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Utafiti wetu ni wa kiisimujamii, hivyo itakuwa bora kufafanua dhana muhimu katika isimujamii, ambazo ni 'isimujamii', na 'jamii'.

Hali kadhalika tutajikita katika maelezo ya jumla kuhusu methali, maoni ya wasomi na wataalamu mbalimbali kuhusu methali. Isitoshe, jamii ndiyo ambayo huamua msamiati unaoteuliwa na kutumika katika methali kwa kuyarejelea mazingira yake. Tutatoa maelezo kuhusu methali, sifa za methali pamoja na mbinu za kuainisha methali kabla ya kutoa maelezo kuhusu maendeleo ya taaluma hii kwa kurejelea methali za Kiswahili.

Hatimaye tutajikita katika kueleza lugha ya Kiswahili na umuhimu wake katika utafiti huu, ambao umeteua methali za Kiswahili kuwa ndiyo data yake.

### 2.1 DHANA YA ISIMUJAMII

Isimujamii ni nomino ambayo imeundwa kutokana na mbinu ya uundaji maneno ya mwambatano. Kwa kutumia mbinu ya mwambatano (ambayo huunganisha maneno mawili au zaidi ili kuunda neno moja) tunapata uelewa kuwa isimujamii ni neno lililoundwa kutokana na maneno mawili, isimu na jamii. Isimu ni taaluma ambayo huichanganua lugha kisayansi, nayo jamii ni kundi la watu ambao wana kaida na tamaduni zinazofanana. Zaidi ya hayo jamii moja ya watu wenye utamaduni na kaida zinazofanana pia hutumia lugha moja. Sifa tulizozitaja zaweza kutumiwa kulitambulisha kundi hilo la watu. Kwa mujibu wa maelezo tuliyoyatoa, isimujamii ni taaluma ambayo kwa mujibu wa (Mekacha 2011:23) hutafiti, huchanganua na kufafanua uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii. Utafiti wetu unalenga kuuchanganua na kuufafanua msamiati ulioteuliwa na kutumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini kwa kuangazia suala la mazingira katika uteuzi wa msamiati huo husika, katika jamii ambamo lugha ya Kiswahili hutumika.

Iribemwangi na Mukhwana (2011:19) wanasema kuwa, "isimujamii hujihusisha na masuala ya kilugha yaliyo katika muktadha halisi wa kijamii." Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, tunaona kuwa isimujamii hujishughulisha na uteuzi wa msamiati ambao utaandamana sambamba na muktadha halisi wa kijamii. Hii ndiyo sababu Binyanya (2014: 27) anasema kwamba, "Muktadha wa mazungumzo humwezesha mzungumzaji kuteua mada mwafaka na pia kutumia lugha kwa njia inayoafiki muktadha"

Methali za jamii yoyote ile huteuliwa kwa njia iliyo mwafaka ili kuoana na hali pamoja na mazingira ambamo methali hiyo imelenga. Msamiati huweza kutofautiana kutoka muktadha mmoja hadi muktadha mwingine kutegemea uamilifu ambao msamiati umekusudiwa kutimiza katika muktadha au mazingira hayo mahsusi.

Taaluma ya isimujamii hulenga kufafanua ni nani anatumia lugha gani na nani, wakati gani na lugha yenyewe hutumiwa namna gani (Fishman 1968). Maoni haya ni muhimu kwa kuwa yanaonyesha kuwa mazingira na washiriki katika mazungumzo ndio huongoza mchakato mzima wa mawasiliano ili kuafikia uelewa. Hii ndio sababu utafiti wetu unafuata mkondo wa isimujamii.

## 2.2 DHANA YA JAMII

Katika utafiti wetu, neno hili jamii tumelitumia kumaanisha jumuiya ya watu walioungana pamoja na kutumia lugha moja, ya Kiafrika ambayo katika utafiti wetu ni lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za mawasiliano; licha ya kutoka katika maeneo tofauti ya kijografia, maeneo ambayo lugha tofautitofauti za kwanza (mama) huzungumzwa.

Binyanya (2014:3) anasema kuwa, jamii ni kikundi cha watu walio na sifa fulani mahususi ambazo zinaweza kutumiwa kuwatambulisha. Upekee wao wa kutenda na kuzungumza ni baadhi ya mambo ambayo huwafanya kuitwa jamii moja.

Kutokana na maelezo haya, jamii ya watu huenda ikawa imeundwa na watu waliotoka katika eneo moja la kijografia au wakatoka sehemu tofauti za kijiografia, lakini wakawa na lengo moja linalowaunganisha, ambalo ni shughuli za kielimu.

## 2.3 DHANA YA MSAMIATI

Msamiati tutaifafanua kuwa ni maneno katika lugha fulani katika idadi au jumla yake. Mzawa wa lugha yoyote ile huwa na uwezo mkubwa wa kutumia msamiati mpana katika lugha yake. Iribemwangi na Mukhwana (2011:154) wanasema kuwa msamiati ni hazina ya maneno ambayo mzungumzaji wa lugha humilliki. Wanaendelea kusema kwamba ikiwa mtu yeyote anataka kuwa na utaalamu fulani hana budi kuwa na hazina kubwa ya msamiati wa taaluma inayohusika. Msamiati unaohusishwa zaidi na taaluma fulani huitwa istilahi. Maelezo ya wataalamu hawa yanatilia mkazo umuhimu wa msamiati kwa mzungumzaji wa lugha na pia mtaalamu yeyote katika taaluma yake. Ni kweli hapa kusema kwamba mtu asiyeelewa msamiati fulani, basi yeye haelewi lugha au taaluma inayohusishwa na msamiati huo.

Iribemwangi na Mukhwana (2011:155-156) wanaeleza kuhusu kategoria nne za msamiati:

i. Msamiati wa mazungumzo

Huu ni msamiati ulio na maneno machache ambayo ni rahisi kushika na kutamkika katika ulimi wa mzungumzaji, na kwamba kulingana na usemaji wa mtu, idadi ya msamiati ambao mtu huyo huenda akawa nao ni mia chache au elfu chache tu. Msamiati huu hutumika na watu wengi zaidi kutokana na ukweli kwamba hata watu ambao hawafahamu kusoma na kuandika huwa wanaweza kuzungumza. Msamiati huu hutumika ili kukidhi mahitaji ya kawaida ya kimsingi.

ii. Msamiati wa kuandika

Msamiati huu ndio kiunganishi kati ya ule wa kuzungumza na ule wa kufikirika. Huu ni msamiati ambao hutumiwa na watu walio na elimu. Mwandishi huteua kutoka kwa orodha yake na kutumia msamiati ulio mpana katika maandishi yake. Msamiati wa kuandika ni mpana kuliko ule wa mazungumzo.

iii. Msamiati wa kusoma

Msamiati huu hutumika na watu wana uwezo wa kusoma. Msamiati wa kusoma kwa kawaida hautumiki katika mazingira ya kawaida kama ule msamiati wa mazungumzo. Msamiati wa kusoma huwa mpana zaidi kuliko ule wa kuandika. Mtu husoma mambo mengi ambayo kwa kawaida huwa hayazungumzi ama kutumika katika hali ya kawaida ya mazungumzo.

iv. Msamiati uliozoeleka

Huu ni msamiati ambao unajumlisha aina tatu za msamiati tulizozitaja hapo juu, na ndio msamiati mpana zaidi. Katika msamiati uliozoeleka, msikilizaji huwa hajui kwa uhakika maana ambayo hubebwa na neno au maneno katika msamiati huo. maana za maneno hayo hukisiwa tu katika muktadha wake wa matumizi.

## 2.4 METHALI

Taaluma ambayo hushughulikia methali kwa kuzichunguza huitwa paremiolojia. Wamitila (2001: vii). Anaendelea kusema taaluma hii huhusishwa mno na mtaalamu aliyejulikana kama Archer Taylor, na kuwa baadhi ya wataalamu wanadai kuwa Taylor ndiye aliyeanzisha taaluma ya paremiolojia.

Kipengele cha methali ni muhimu sana katika jamii nyingi barani Afrika. Finnegan (1983:379) anasema kuwa methali zinapatikana karibu kila mahali barani Afrika. Anaendelea kutaja sehemu ambazo methali zinapatikana kwa wingi pamoja na jamii za watu ambao hutumia methali katika shughuli zao za maisha ya kila siku, ambapo sehemu ambazo Wabantu wanaishi hususan Wabantu wa Kusini mwa Afrika, Kongo na Afrika Magharibi walikuwa na hazina kubwa sana ya methali. Baadhi ya jamii za Waafrika kwa mujibu wa Finnegan zina methali nyingi sana kama vile jamii ya Warundi ambao wana methali 4000 zilizokusanywa na kuchapishwa na wanaparemiolojia.

Methali ni kipengele kimoja katika fani ya fasihi simulizi (Wamitila 2001: viii). Hakuna mpaka ulio wazi ambao upo kati ya methali na vipera vingine vya fasihi simulizi.

Finnegan (1983:382) anasema yafuatayo kuhusiana na hali hii.

> (Methali) hazifai kuchukuliwa kuwa semi zilizotengwa ili zikusanywe kwa mamia na maelfu kivyake, bali zichukuliwe kuwa kipengele kimoja cha sanaa katika jamii nzima na muktadha andishi (Tafsiri yetu)

Ni kutokana na maelezo haya ambapo tunapata kuwa kuna utata katika kuweka mpaka kati ya methali na misemo ya kimethali. Mtu anaopoelekezewa methali au msemo wa kimethali huenda yote kwake yakawa yale yale mamoja kuwa ameelekezewa methali.

Sehemu inayofuata inatoa maelezo kuhusu sifa za methali, huku misemo ya kimethali ikijumuishwa kuwa sawa na methali.

### 2.4.1 SIFA ZA METHALI

Katika sehemu hii tutaangazia baadhi ya sifa za methali kwa mujibu wa wataalamu katika taaluma hii. Sifa za methali zitatuongoza kupata uelewa zaidi kuhusu methali zenyewe kwa ujumla wake, pamoja na jamii ambamo methali hizo zimetoka.

#### 2.4.1.1 UWILI

Sifa hii ya methali inatokana na ukweli kwamba methali huwa na maana mbili, maana iliyo wazi ambayo hubainika kutokana msamiati uliotumika, na maana batini. Mzungumzaji anapotumia methali, itabidi msikilizaji asikomee kwenye maana ya juujuu tu ya methali hiyo, bali awaze kufikiria zaidi ndipo apate maana ya ndani yaani maana batini. Msikilizaji hana budi kuoanisha mazingira ya mazungumzo, uhusiano wake na mzungumzaji, pamoja na athari zake za kiutambuzi ndipo afikie uelewa kama ulivyokusudiwa na mzungumzaji.

Wamitila (2001: xiii) na Finnegan (1983:385) wanazungumzia sifa hii. Kutokana na maelezo yao, aghalabu methali zote zina sifa hii ya uwili.

Mifano ya methali

i. Jiwe la kutupa ngomani humpiga wako.
ii. Mali ni sawa na maua.
iii. Mwanamke mzuri hakosi kilema.
iv. Paka ana nusura tisa.
v. Ukitaka kula nguruwe chagua aliyenona.

#### 2.4.1.2 MKATO NA UFUPISHO WA KIMUUNDO

Methali huwa semi zinazotumia maneno machache ili kusahilisha maelezo. Kwa kutumia methali, sifa za kiuchumi zinapatikana kwa sababu ya muda mfupi ambao methali hutumia kuwasilisha ujumbe ambao ungewasilishwa kwa maneno mengi ya kawaida.

Mifano ya methali:

i. Mjumbe hauwawi.
ii. Kikulacho ki nguoni mwako.
iii. Mzazi haachi ujuzi.
iv. Nguzo ya nyumba ni mke.
v. Nyongeza haigombi.

Naye Finnegan (1983: 288) anasema kuwa hali ya uchumi imeafikiwa pia kwa kutumia mbinu ya kitangulizi, ambapo mzungumzaji hutaja tu neno la mwanzo la methali, kisha msikilizaji anaelewa mkondo wa mawasiliano.

Kwa mfano:

i. Kawia …
ii. Jungu kuu…
iii. Majuto…
iv. Penye nia…
v. Kuteleza…

**2.4.1.3 MBINU YA USHAIRI**

Methali nyingine huwa na sifa ya kutumia mbinu ya ushairi, hasa ushairi wa kiarudhi. Kuna methali ambazo zimechukua usawa wa mizani katika upande wa kwanza na upande wa pili, vilevile vina vya kati na vya mwisho huenda vikafanana (Wamitila 2001: xiv)

Kwa mfano:

i. Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa
ii. Uongo haramu, ingawa mtamu
iii. Haraka haraka, haina baraka
iv. Penye nia, pana njia
v. Penye tamu, pana sumu
vi. Penye uhondo, pana uvundo.

### 2.4.1.4 MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI

Sifa hii hutumiwa katika methali nyingi. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo methali hutumia ni pamoja na

a) Sitiari

Sitiari ni muhimu sana hata katika mazungumzo ya watu ya kila siku. (Wamitila 2001: x-xi) Mifano ya methali ambazo zimetumia sitiari ni:

i. Ujana ni moshi ukienda haurudi.
ii. Mambo ni kangaja, huenda yakaja.
iii. Mapenzi ni majani, popote penye mbolea hujiotea.
iv. Nguvu ya mamba ni maji.
v. Mali ni ngazi, utakapo hupanda.

b) Chuku

Chuku ni tamathali ya usemi ambayo huongeza chumvi au kupunguza chumvi habari kuhusu hali fulani.

Mifano ya methali ambazo zimetumia tamathali ya chuku kwa mujibu wa Wamitila (2001: ix) ni:

i. Ndovu akitamba ni masika.
ii. Hakuna kubwa lisiloshindwa.
iii. Papo kwa papo kamba hukata jiwe.

### 2.4.1.5 MATUMIZI YA LAHAJA NA MSAMIATI WA KALE

Methali ni mojawapo ya taaluma zilizo na hazina muhimu sana ambayo huwezesha lugha yoyote ile kuhifadhi msamiati wake wa kale. Baadhi ya methali huweza kutumia msamiati wa kale. Finnegan (1983: 391) akimrejelea Chatelaine (1894: 22) anasema:

> Methali zinatambulika na hufanya hivyo kwa kutumia mbinu nyingi zikiwemo matumizi japo si kila wakati maneno ya kale au msamiati usiokuwa wa kawaida… (Tafsiri yetu).

Wamitila (2001: ix) ameorodhesha mifano ya methali ambazo zimeundwa kwa kutumia msamiati wa kale na matumizi ya lahaja:

i. Mchama ago hanyele huenda akauya papo.
ii. Kuva mva na mvuvi
iii. Afadhali dooteni kama ambari kutanda.
iv. Msi kucha kwambwa nyamba
v. Ukilala na ng'ombe tinde huamkia kuchuna
vi. Sitapiki nyongo harudi haramba
vii. Nguwe huagana wakenenda.

### 2.4.2 MBINU ZA KUAINISHA METHALI

Methali huweza kuainishwa kwa namna tofauti tofauti, kulingana na dhamira au lengo la mwanaparemiolojia anayezikusanya na kuziainisha methali zenyewe. Katika sehemu hii, tutaeleza kuhusu mbinu hizo za kuziainisha methali hizo husika.

#### 2.4.2.1 UANISHAJI WA KIMAUDHUI

Katika uainishaji huu, methali huwekwa kwa makundi kutegemea maudhui yanayopatikana katika methali hizo kwa mujibu wa mtafiti. Mfano wa uainishaji huu wa kimaudhui ni ule unaozungumziwa na Joon (1992:71-74) akimrejelea C.L. Sibusiso Nyembezi (1963), ambaye ameainisha methali za Kizulu, katika makundi makuu yafuatayo pamoja na vijikundi vidogo vidogo chini ya makundi makuu:

1. Utu
    a. Ukarimu
    b. Tabia mbaya
    c. Fahari
    d. Utovu wa shukrani
    e. Ukaidi
    f. Utovu wa utu wema na maadili murua
    g. Mengineyo yanayohusika na utu.

2. Uaminifu na utovu wa uaminifu
    a. Udanganyifu
    b. Hila
    c. Utovu wa uaminifu

3. Urafiki na uhasama
    a. Vitisho
    b. Kisasi
    c. Utovu wa huruma
    d. Uadui
    e. Urafiki
    f. Uhasama
    g. Mengineyo yanayohusika na urafiki na uhasama.

4. Bahati njema na bahati mbaya
    a. Bahati njema
    b. Bahati mbaya
    c. Taabu
    d. Kazi bure
    e. Kutofaulu
    f. Kukata tama
    g. Tashwishi
    h. Kutia moyo
5. Ujasiri na woga

6. Mambo ya nyumbani
    a. Ndoa
    b. Urithi
    c. Uendelezaji wa nyumba
    d. Uzawa

    e. Wazazi na watoto
    f. Mizimu
    g. Mazungumzo
    h. Mwazimo
    i. Mengineyo yanayohusu mambo ya nyumbani

7. Mapito ya wakati
    a. Uzee
    b. Kifo

8. Busara na ujinga

9. Tahadhari
    a. Malezi ya watoto
    b. Hatari
    c. Kufanya mambo mwenyewe
    d. Kutafuta mashauri
    e. Madhara ya vitu vidogo
    f. Kufanya mambo bila kujali
    g. Huruma kwa wengine
    h. Shukrani
    i. Utondoti
    j. Uvivu na jitihada
    k. Mengineyo yanayohusu tahadhari

10. Mengineyo yasiyotengwa chini ya makundi tisa ya juu.

#### 2.4.2.2 UAINISHAJI  UNAOTEGEMEA SAUTI ZA KATI NA ZA MWISHO

Katika uainishaji huu, methali huwekwa kwa makundi kutegemea sauti za kati na za mwisho ambazo zimetumika kuiunda methali husika.

Mifano ya methali hizo ni hizi zifuatazo:-

i. Haraka haraka, haina baraka.
ii. Binadamu ni ngamba, hawakosi la kuamba
iii. Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa.
iv. Mambo ni kangaja, huenda yakaja.
v. Mwana mtukana nina, kuzimu enda kiona.

### 2.4.3 UANISHAJI KATIKA MAKUNDI YA NOMINO

Katika uainishaji huu, methali huwekwa katika makundi ya nomino ambazo zimetumika katika uundaji wa methali husika. Hebu tutumie uainishaji wa Andambi na Murono (2005).  Baadhi ya makundi katika uainishaji wao ni haya yafuatayo:

#### 2.4.3.1 METHALI ZONAZOREJELEA SEHEMU ZA MWILI

Methali zote ambazo hurejelea sehemu za mwili huwekwa katika kundi moja. Mifano ya methali katika Andambi na Murono (2005) katika kundi hili ni kama:-

i) Mkono mmoja hauchinji ng’ombe.
ii) Mwenye macho haambiwi tazama.
iii) Sikio la kufa halisikii dawa.
iv) Jino la pembe si dawa ya pengo.
v) Shingo hubeba vyombo, roho hubeba mambo.

#### 2.4.3.2 METHALI ZINAZOREJELEA WANYAMA

Mifano ya methali katika Andambi na Murono (2005) katika kundi hili ni kama ifuatavyo:-

i) Paka hashibi wali, matilabaye panya
ii) Siku ya kufa nyani miti yote huteleza.
iii) Ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona.

iv) Mbwa hafi maji akiona ufuko.

v) Fahali wawili hawakai zizi moja.

**2.4.3.3 METHALI ZINAZOREJELEA NDEGE**

Mifano ya methali katika Andambi na Murono (2005) katika kundi hili ni kama ifuatavyo:

i) Makuukuu ya tai si mapya ya kengewa

ii) Dua la kuku halimpati mwewe.

iii) Kuku akiacha wana ana mayai tumboni

iv) Kunguru mwoga hukimbiza ubawawe

v) Ndege asiyenaswa leo ni kitoweo cha kesho.

**2.4.3.4 UANISHAJI WA METHALI ZINAZOREJELEA WADUDU**

Mifano ya methali katika Andambi na Murono (2005) katika kundi hili ni kama ifuatayo:

i) Dudu liumalo silipe kidole

ii) Fuata nyuki ule asali

iii) Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.

iv) Nzi kufia tuini si hasara.

v) Ganda la muwa la jana, chungu kaona kivuno.

**2.4.3.5 METHALI ZINAZOREJELEA MIMEA NA MATUNDA**

Mifano ya methali katika Andambi na Murono (2005) katika kundi hili ni kama hii ifuatayo:-

i) Gogo la mvule si la mbuyu

ii) Buyu kali ni dawa ya mwana mimba

iii) Atakaye kupika mchuzi, kiungo ni malimau

iv) Mbaazi kukataa kuzaa husingizia jua.

v) Masukuzi ya leo ndio msitu wa kesho.

### 2.4.3.5 METHALI ZINAZOREJELEA HALI

Methali katika (2005) katika kundi hili kwa mujibu wa Andambi na Murono (2005) zinaoanishwa na mifano ifuatayo:

i) Majuto ni mjukuu, huja baadaye
ii) Hamna hamna ndimo mliwamo
iii) Asiyejua kufa na atazame kaburi
iv) Asiyejua hili ajua lile
v) Baada ya dhoruba huja utulivu

Udhaifu wa kuainisha methali kwa mujibu wa nomino, ni kuwa baadhi ya methali huwa na nomino Zaidi ya moja, na kwa hivyo kuweza kuziainisha ipasavyo linakuwa jambo gumu.

Mifano ifuatayo inaonyesha hali hii.

i) Joka la mdimu hulinda watundao. (mnyama na mmea)
ii) Bua huua ndovu. (sehemu ya mmea na mnyama)
iii) Bahili huchumia nondo na kutu. (binadamu na mdudu)

### 2.4.4 METHALI ZA KISWAHILI

Methali za Kiswahili zimekusanywa katika kazi kadhaa za kifasihi. Kazi hizo zimefafanuliwa kwa lengo la kuwaongoza wasomaji wa kazi hizo. Wamitila (2001: vii) anatuambia kuwa kazi ya kwanza ambayo ilikusanya methali za Kiswahili ilikuwa ya Taylor, ambayo ilichapishwa mwaka wa 1891; kazi hii imeadimika siku hizi. Kazi hiyo ya Taylor inajulikana kama *African Aphorisms*. Anaendelea kusema kuwa kazi ya Saleh Farsi, *Swahili Sayings* ndiyo iliyokuwa ya kwanza kushughulikia methali katika mazingira ya Afrika Mashariki. Kazi hii inachukuliwa kuwa msingi wa uchunguzi wa methali.

Kamusi mbalimbali za methali zimechapishwa baada ya kazi ya mwanzo ya Farsi. Wamitila (2001: vii) anamrejelea Albert Scheven na kazi yake *Swahili proverbs*, kazi ambayo imekusanya methali mbalimbali kutoka kwa maandishi mbalimbali ya Kiswahili, kisha akazipanga methali hizo katika makundi tofauti tofauti kwa mujibu wa maudhui au dhamira zilizomo katika methali husika. Wamitila (2001:vii) anaendelea kusema kuwa kazi hiyo imelenga hadhira ya Wazungu.

Katika kazi hiyo, Scheven anaziainisha methali za Kiswahili katika matapo au makundi madogomadogo hamsini na sita baada ya kuainisha methali kwa kutumia kigezo cha maudhui.

Baadaye tafiti nyingi kuhusu methali za Kiswahili zimefanywa. Nyingi ya tafiti hizo zinabainisha jinsi lugha ya Kiswahili inavyozidi kupanuka katika mawanda ya matumizi yake. Baadhi ya kazi za utafiti wa methali ambazo zimekwisha kufanywa ni kama vile: Karama (1983), Ndalu (1989), Wamitila (2001), Andambi (2005) King'ei (2008) na Arege (2011). Kadri utafiti unavyozidi kufanywa ndivyo idadi ya methali inavyozidi kuongezeka. Kwa mfano; Wamitila (2001) amekusanya jumla ya methali elfu mbili mia tisa na sitini na nne, naye Arege (2011) amekusanya methali elfu tatu mia tano thelathini na sita. Kazi hizi zinaonyesha wazi kuwa methali ni muhimu sana katika jamii na kwa hivyo methali zinapewa uamilifu mkubwa.

## 2.5 LUGHA YA KISWAHILI

Utafiti wetu umejikita katika lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inatumika na watu wengi zaidi nchini Kenya katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa taifa.

Mukhwana (1990:1) anasema kuwa lugha haiwezi ikatenganishwa na jamii, kwa sababu mahusiano ya kilugha ni mahusiano ya kijamii vilevile. Anaendelea kusema kuwa, kuchagua lugha fulani itumike mahali fulani na watu fulani hufanywa ili kuathiri muundo wa jamii husika ili kutosheleza mahitaji fulani ya kijamii. Maelezo haya yanatupa mwelekeo kuwa lugha fulani hutumiwa na jamii katika mazingira yanayoruhusu lugha hiyo kutumiwa ili itimize lengo fulani.

Methali za Kiswahili hutumiwa baina ya wanajamii ambao wanaielewa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kufanikisha mawasiliano kwa namna ya kipekee. Methali fulani hutumika katika mazingira mahsusi ili kuleta athari fulani kwa mwanajamii. Athari hiyo hulenga kufanikisha uamilifu wa jukumu au majukumu fulani kwa msikilizaji.

Lugha ya Kiswahili ina nafasi kubwa miongoni mwa lugha nyingine za kiafrika nchini Kenya. Ni lugha ya Kiswahili peke yake ambayo imetunukiwa majukumu mawili, jukumu la kutumiwa kama lugha ya taifa na jukumu la kuwa lugha rasmi. Methali za Kiswahili hutumika katika mazungumzo ya kila siku, yawe rasmi au ya kawaida tu.

Katika mahusiano baina ya watu mbalimbali, mawasiliano huanza kwa namna mbalimbali hadi kunapotokea mabadiliko katika mawasiliano ambayo mwishowe hujenga maafikiano baina ya watu hao. Hii ndiyo sababu Kiswahili hutumiwa na watu wa matabaka yote (Whiteley 1974: 190, 208).

Kwa kuwa lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli nyingi za mawasiliano na watu wa jamii tofauti nchini Kenya, methali za Kiswahili pia huwa sehemu mojawapo ya shughuli hizo, kwa kuwa hutumika kwa lengo la kufanikisha mawasiliano. Hii ndiyo sababu lugha ya Kiswahili itakuwa mhimili mkubwa katika utafiti wetu, kwani ina hadhi na majukumu mengi nchini.

## 2.6 HITIMISHO

Katika sura hii tumeeleza dhana muhimu katika utafiti wetu. Methali ni utanzu muhimu sana katika maisha ya kila siku ya binadamu. Umuhimu huu unatiliwa nguvu na utafiti ambao unafanywa na watafiti wanaparemiolojia ambapo methali nyingi zimekusanywa kwa kuziainisha kwa mbinu tofautitofauti na pia kwa kueleza sifa za methali. Kutokana na umuhimu huu wa methali katika jamii pamoja na sifa zake, ufahamu wa dhana za isimujamii na jamii ni muhimu katika kuelewa matumizi yafaayo ya methali. Methali za Kiswahili kama ilivyo lugha ya Kiswahili ni muhimu kwa jamii katika eneo hili la Afrika Mashariki na Kati, kwa kuwa wanajamii wengi wanaielewa lugha ya Kiswahili.

# SURA YA TATU

## UFAFANUZI WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI: SIFA, TABIA NA MAUMBILE YA VIUMBE WALIOTUMIKA KATIKA METHALI HIZO

### 3.0 UTANGULIZI

Joon (1992:36) anasema kuwa sifa moja ya methali ni ufupi. Katika kutumia methali mzungumzaji hufupisha maelezo mengi kutokana na utumizi wa maneno machache sana. Kwa sababu hii basi, Joon anatuambia kwamba ni kazi ngumu inayohitaji ustadi wa kiwango cha juu katika uteuzi na matumizi ya maneno.

Kutokana na maelezo haya, hatuna budi kukubaliana naye katika shughuli inayohusiana na uteuzi wa methali zenyewe. Uteuzi wa msamiati katika methali unafaa kusheheni sifa ambayo haitamkanganya msikilizaji kwa kuwa anauelewa msamiati wenyewe na wakati huo huo kupitisha ujumbe ambao ungefafanuliwa au kuelezwa kwa kutumia maneno mengi sana.

Katika sura hii, tumezifafanua methali za Kiswahili zinazotumia msamiati wa viumbe wa majini. Katika ufafanuzi wetu, tumetoa maelezo kuhusu methali husika kwa kuzingatia tabia na maumbile ya viumbe kwenye methali husika kwa mujibu wa jamii ya Waswahili.

Tumeziainisha methali zenyewe kwa njia ya kialfabeti. Katika kutumia mtindo huu wa uainishaji tumekumbana na baadhi ya methali ambazo zimetumia msamiati ule ule ila kwa mtindo tofauti ambapo msamiati au neno fulani litapatikana mwanzoni mwa methali fulani na neno lilo hilo lipatikane katika sehemu tofauti kwenye methali tofauti. Pale ambapo tumejipata katika hali kama hiyo basi tumemwelekeza msomaji hadi kwenye methali ni sawa na hiyo ambayo tayari tumeshaishughulikia.

Katika sura hii, tumeangazia jinsi wataalamu wanavyosema kuhusiana na msamiati ulioteuliwa. Kwa kufanya hivi, tumekuwa katika hali bora ya kuweza kuupambanua msamiati uliotumika na jinsi unavyofaa kutumika katika methali fulani iliyoteuliwa.

Katika utafiti wetu, tumetumia methali zinazorejelea viumbe wa majini zinazopatikana kutoka kwenye kamusi za methali ambazo tulikumbana nazo. Kwa kufanya hivi, tunataka kuungama

kuwa huenda kukawa na methali nyingi zaidi ambazo zinarejelea viumbe wa majini, ila hatujazitaja katika utafiti wetu.

Tamathali za usemi za tashbihi, istiara na uhuishaji zimetufaa katika kutoa maelezo kuhusiana na msamiati ulioteuliwa pamoja na kuiangalia jamii katika mazingira yake, kwa kuangazia tabia, sifa na maumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali hizo na uhusiano wao na viumbe wengine, na mazingira yao kwa jumla. Hivyo basi, msamiati uliotumika katika methali hizo husika utakuwa muhimu sana katika utafiti wetu, ili tupate uelewa kuhusu sababu za uteuzi wa viumbe wa majini katika methali hizo.

1. **ALAYE KITU CHA MAMBA ASIFIKE MAJINI**

Mamba ni mnyama mkubwa ambaye huishi majini. Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu (2013:320) wanasema kuwa ni mnyama kama kenge mkubwa mwenye magamba akaaye mtoni na ziwani.

Tofauti na wanyama wengine wa maji baridi kama vile kiboko ambaye hutoka ndani ya maji usiku na kula nyasi, mamba yeye hubaki majini na kuyafanyia mawindo yake pale pale. Mamba, atawasubiri wanyama ambao huenda kukata kiu chao majini ndipo wawe chakula chake.

Tabia hii ya mamba inatufafanulia sababu za kuteuliwa kwake na kutumiwa katika methali hii, kuwa mamba kwa kawaida huwa yuko majini au karibu na maji, na kwamba mawindo yake hutekelezwa pale majini. Mamba hula nyama.

‘Alaye’ ni kitenzi kilicho katika hali ya mazoea. Katika methali hii, mamba hupata chakula chake pale majini kwa kuwavizia wanyama wanaoenda kunywa maji yale. Hivyo basi tunaona namna ambayo uteuzi wa msamiati katika methali hii unavyooana, yaani hali ya kula kwa mamba, na mamba kwa maji. Moja kwa moja mchango wa mazingira katika uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali hii unabainika bila wasiwasi wowote.

Katika mazingira ya mtoni huenda mtu asimpate mnyama kama kiboko majini kila wakati au katika maeneo ya majini, hali ambayo ni tofauti kwa mamba ambaye daima huwa kama hayuko ndani ya maji, hujibarizi au hujibanza karibu na maji ili aote jua, na anapomuona mnyama

yeyote akielekea majini mamba hurudi ndani ili kujitafutia chakula; ambacho huwa ni mnyama huyo ambaye anayanywa yale maji.

Si ajabu basi neno ‘majini’ limetumika kumaanisha ndani ya maji. Kutokana na hali hii, pana uwezekano mkubwa mno wa kukutana na mamba ndani ya maji, na hivyo kuwa chakula chake. Sifa na tabia hii ya mamba inaoana vyema na mazingira yake, hivyo uteuzi mwafaka wa msamiati katika methali hii.

**2. ANA NCHI YAKE SIMBA ANA MAJI YAKE MAMBA**

‘Ana’ ni kitenzi kilicho na maana ya kumiliki katika nafsi ya tatu. Kama tulivyokwisha kueleza, mamba ni kiumbe ambaye daima huwa na uhusiano mkubwa sana na maji. Mamba huishi majini na kuyafanyia mawindo yake pale majini. Awapo majini, mamba huwavizia viumbe wengine ambao huenda kukata kiu chao mtoni, na kuwawinda ndipo awale. Hali hii ya mamba humfanya kumithilishwa na mfalme wa majini kama asemavyo Wamitila (2001:27) kuwa mamba ni mfalme wa majini ambaye hula nyama.

Sote tuna ufahamu wa simba kuwa ni mnyama maarufu sana miongoni mwa wanyama pori kwa kuwa na nguvu, ni mkali na pia mwindaji hodari, kwa hivyo yeye kwa kawaida hula nyama.

Wamiltila (2001:27) anasema kuwa, ‘simba ndiye mfalme kwenye nchi kavu.’

Kutokana na maelezo haya, tunaelewa moja kwa moja kwamba simba ni mnyama mkubwa wa porini na pia hula nyama. Simba siye mnyama mkubwa zaidi wa nchi kavu. Kunao wanyama wakubwa kuliko simba kimaumbile kama vile ndovu, ila ndovu hali nyama.

Tabia za mamba na simba za kuwawinda wanyama wengine na kuwala zimefananishwa na za mfalme au kiongozi wa wanadamu ambaye ana haki ya kuwatawala na kuwatendea watu anaowatawala jinsi atakavyo.

Uhusiano uliopo kati ya mamba na simba katika janibu wanazomiliki, ulifaa katika matumizi ya methali hii, kuwa hakuna eneo, boma, nchi au ufalme ambao hauna kiongozi wake ambaye ana uwezo mkubwa kwa wale anaowatawala, na kuwa kila kiongozi hutawala eneo lake mahsusi na wala hawezi akatawala kwa kiongozi mwingine. Uhusiano uliopo kati ya simba, mamba na maeneo yao ya kimazingira ambayo wao huyatawala unaonekana

### 3. ANAYETAKA KUFA NA ALA BUNJU, ATAZAME REHEMA YA MUNGU

TUKI (2013:48) inasema kuwa bunju au bungu ni samaki wa baharini wa kahawia anayejifurisha mwenye sumu ambayo huondoka akisafishwa vizuri. Wamitila (2001:29) anasema kuwa, 'bunju ni aina ya samaki ambaye huwa na sumu.'

Maelezo haya yanayomhusu bunju yanatupa ukweli kuhusu samaki huyu, kuwa ana sumu ambayo inaweza kumdhuru au hata kumuua mtu, hasa iwapo samaki huyu hakusafishwa vizuri kabla ya kuandaliwa.

'Anayetaka' ni kitenzi kilicho na maana ya kuwa na hamu fulani ya mtu, kitu au kitendo fulani. Hivyo basi, anayetaka kufa ni kiumbe aliye na hamu ya kuaga dunia. 'Ala' ni kitenzi kula katika wakati usiodhihirika -a huenda ukawa wakati wa hali ya mazoea au wakati uliopo. Hivyo basi wakati wowote ule afikiriapo mtu kula bunju, atakuwa akijitia katika hatari ya kuathirika kutokana na ulaji wake kwa sababu ya sumu ya bunju.

Atazame rehema ya Mungu, kama asemavyo Wamitila (2001:29) kuwa ni kuomba msamaha wa Mungu kwa kuwa atakufa tu.

Katika methali hii, tunaona uhusiano uliopo kati ya kumla bunju na matokeo yake ambayo hatimaye ni kifo.

Bunju basi ni samaki ambaye ameteuliwa na kutumika katika methali hii kwa sababu ya sifa yake ya kuwa na sumu ambayo anamiliki. Si samaki wote huwa na sumu, kwa hivyo Waswahili walikuwa na lengo la kuwasilisha ujumbe mahususi kwa kutumia samaki bunju ambaye ana sifa na maumbile yanayosadifu ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa kwa msikilizaji au wasikilizaji.

### 4. ATAKAYE MAJI MTONI ASIMTUKANE MAMBA

Methali hii imetumia jina mamba kama ile iliyotangulia. Hivyo basi, maelezo kumhusu mamba ni sawa na yale ambayo tayari tumeshaeleza. Neno 'atakaye' limetumika, nalo ni kitenzi kutoka kwa mzizi 'tak' kilicho na maana sawa na 'hitaji'. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013: 535) inatuambia kuwa 'taka' ni kuwa na hamu au haja ya jambo fulani. Kitenzi hiki kinaingiliana na mamba kwa sababu mamba huishi katika maji baridi kwenye mito au maziwa. Maji baridi ni maji ambayo hayana chumvi. Binadamu aghalabu huyatumia maji haya baridi katika shughuli

zake za kawaida za nyumbani. Ndiposa ayapate maji haya basi, huwa hana budi kufika mtoni au sehemu nyingine zenye maji baridi ili ayapate, na mito ni makao ya mamba. Pana mito ambayo hupitia majanibu ya Waswahili, kama vile mto Galana, ambao huwa na mamba wengi. Katika methali hii basi tunaona jinsi msamiati ulioteuliwa unavyokubaliana na mazingira halisi ya jamii ya Waswahili, pamoja na shughuli zao.

Ndipo upate maji mnyama unayeweza kukumbana naye ni mamba, na wala si wanyama wengine hatari wa majini kama vile papa ambao huishi baharini.

Uteuzi huu wa msamiati unatusawiria ukweli wa mazingira halisi ya jamii ya Waswahili kwa kutupa uhusiano uliopo kati ya mamba, binadamu na maji.

**5. AVUMAYE BAHARINI PAPA KUMBE WENGINE WAPO**

Katika methali hii, neno papa limetumika. Andambi A. (2005) anatoa fasili ya neno hili papa kuwa samaki mkubwa na mkali ambaye huishi baharini. TUKI (2013:450) inafasili papa kuwa samaki mkubwa wa bahari asiye na mamba, mwenye ngozi nene ya kijivu hafifu.

Tumetajiwa pia baadhi ya aina za papa wakiwemo papa upanga, papa pingusi, papa usingizi na papa amrani. Katika ufafanuzi wetu, hatutatoa maelezo ya kila mmoja ya aina hizi za papa bali tutatoa maelezo ya jumla.

Katika maelezo ya jina papa, tunaona kuwa ni samaki mkubwa mwenye ngozi nene mkali na ambaye huishi baharini. Bahari ni eneo kubwa la maji yenye chumvi, na ambalo hutenganisha mabara. Uteuzi wa neno hili ni kubainisha uwezo alio nao papa akilinganishwa na samaki wengine.

Pia kitenzi ‘avumaye’ kimetumika. Kitenzi hiki ambacho kinatokana na mzizi ‘vum’ kimetumika kwa maana ya kutoa sauti yenye uzito na pengine yakutisha kama vile sauti ya simba, upepo mkali, ngoma, nyuki au maji mengi yanapomiminika kwa kasi TUKI (2013:625). Sababu za kuteua kitenzi hiki ni kuleta mshabihiano kati ya papa na vishindo vyake baharini. Licha ya ukweli kwamba samaki hawatoi sauti majini, kitenzi hiki kinatudhihirishia nguvu za papa anapoogelea pale baharini.

Kumbe wengine wapo ni maneno ambayo yanaweza yakaelezwa kwa njia mbili. Kwanza, maneno haya yameteuliwa kuwakilisha samaki na viumbe wengine wa majini katika mazingira ambamo papa yumo. Samaki wengine wadogo kama vile changu, taa, mkizi, kaa miongoni mwa wengine wanadhalilishwa katika mazingira ambamo papa yumo.

Uteuzi huu pia unawarejelea viumbe wengine wa baharini ambao wanatisha na kuwa wakubwa zaidi ya papa mwenyewe. Mfano ni papa wengine na nyangumi ambao ni wakubwa zaidi kuwashinda papa. Katika kuegemea mtazamo huu, tunaona ukweli kwamba licha ya papa kutisha kule baharini, kunao papa wengine na nyangumi ambao pia wanatisha na hata huwa na ukubwa uliozidi ule wa papa wa awali.

Katika maelezo haya tunaona jinsi mazingira halisi ya bahari yanavyooana na sifa ya papa unapomfananisha na viumbe wengine wa majini. Uteuzi huu unadhihirisha ufanisi mkubwa wa methali hii katika jamii ya Waswahili, kwa kutupa uhusiano uliopo baina ya papa na viumbe wengine katika mazingira ya bahari.

## 6. BINADAMU NI NGAMBA HAWAKOSI LA KUAMBA

Wamitila (2001:54) anatuambia kuwa ‘ngamba ni aina ya kasa. Gamba lake hutumiwa kutengeneza vijaluba, vitana na kadhalika.

Kutokana na maelezo haya, tunapata ufahamu kuhusu kiumbe ngamba na gamba lake. Magamba ya ngamba hutumika kutengenezea bidhaa kama vile viluba na vitana. Binadamu anapopata gamba la ngamba, analihusisha na bidhaa fulani ambayo huenda anaihitaji. Ataitengeneza bidhaa hiyo kwa kutumia gamba la ngamba alilolipata. Hivyo basi, kutokana na gamba la ngamba binadamu ataunda bidhaa kadhaa.

Katika Mazungumzo ya kila siku, ya binadamu wao huweza kuzugumza kuhusu mambo mengi, mengine huenda yakawa ya kutia moyo au hata ya kuvunja moyo. Binadamu ambaye leo atakusemea mazuri kesho atasema kinyume kukuhusu, kwa kutumia kinywa kile kile kimoja.

Uteuzi wa msamiati wa kiumbe huyu umeleta uwiano mzuri na tabia ya binadamu, kuwa kama gamba moja linavyotumika kutengeneza bidhaa maridhawa vivyo hivyo binadamu huzungumza kuhusu mambo mengi. Hivyo basi tabia hii ya binadamu inaonyesha uhusiano wake na kazi

ambayo gamba la ngamba hufanya. Binadamu akipata gamba hatakosa bidhaa ya kuunda kama walivyo binadamu wanapokutana, hawatakosa la kusema kuhusiana na tukio au hali yoyote ile anayokumbana nayo.

## 7. CHAFI KANDANI MWAKO NI CHAFI- KIYENGE

TUKI (2013:54; 191) inasema kuwa chafi au tafi ni ‘samaki wa baharini wa kijivujivu, mpanampana na batabata’ mifano ya chafi ni chafi mavenga na chafi uzio. Kanda ni fuko kubwa lililosukwa kwa chane za miyaa au majani ya mvumo ambalo hutumiwa kuwekea chakula au vitu kama vile karafuu au tende. Wamitila (2001:60) anasema kuwa chafi – kiyenge ni ‘aina ya samaki wadogo, ambao pia huitwa tafi’.

Maelezo haya yanatusawiria uhusiano uliopo kati ya ‘kanda’ na ‘chafi-kiyenge’. ‘Kanda’ ni fuko kubwa nao ‘chafi-kiyenge’ ni aina ya samaki wadogo.

Mtu anapowaweka chafi-kiyenge kwenye kanda, huenda kanda lake likaonekana kuwa tupu, hali ambayo inasababishwa na udogo wa samaki waliomo kandani; yaani chafi-kiyenge.

Katika methali hii, tunaona jinsi maumbile ya samaki aliyetumika yanavyoakisi ukweli wa mazingira ambamo wamewekwa, kwenye kanda. Udogo wa chafi humfanya mwenye kanda kuona kuwa kanda lake ni tupu. Kwa kawaida mazoea ya binadamu katika maisha ni kuwa kitu, mtu au mahali pakubwa panahusishwa na kitu, mtu au mahali pengine pakubwa.

Lakini wakati mwingine huenda mambo na hali zisiwe jinsi tunavyofikiria na kuonekana kinyume cha matarajio ya watu. Hivyo basi, ingawa chafi ni samaki, akiwekwa kandani huonekana kuwa chafi kiyenge, lakini ukweli ni kwamba yeye ni chafi. Uteuzi huu wa msamiati umedhihirisha ukweli wa maisha kwamba kila wakati maisha huwa si yale yale, huenda tukakumbana na hali ambazo ni kinyume cha matarajio kutegemea mazingira na mahusiano ya viumbe husika katika mazingira yao halisi.

## 8. CHAFI RASILMALI YAKE UTUMBO (MATUMBO)

Tumekwisha kutoa maelezo yanayomhusu chafi katika methali, ‘chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge’. Kwa kusema kuwa chafi ni samaki, ingawa si mkubwa kama samaki wengine, na kama asemavyo Wamitila (2001:60) chafi pia ana sifa zake na ana faida zake.

Kiulinganishi, chafi ni samaki mdogo kuliko samaki wengine. Hata hivyo ana faida na sifa zake. Licha ya udogo wake kimaumbile chafi anaponaswa huweza kutayarishwa na kuwa mlo ambao huwafaidi walaji. Wanaomla chafi watakuwa wamekula sawa na wale ambao wanawala samaki wengine wakubwa. Chafi hushibisha tu sawa na wale samaki wakubwa.

Katika methali hii, tunaona jinsi uteuzi wa msamiati unavyowiana na mazingira ambamo chafi huishi, udogo wake na umuhimu wake katika mazingira aliyomo, licha ya kudunishwa na kudharauliwa chafi huwa na umuhimu wake katika jamii.

## 9. CHOKOCHOKO KAMCHOKOE PWEZA, BINADAMU HUTAMWEZA

Kuchokoa ni kudungadunga au kumsumbua mtu na kusababisha hali ya kutokuwa na utulivu au raha, hali ambayo mwishowe humsababishia au humfanya mtu kukereka. Wamitila (2001:65) anasema kuwa, Chokochoko ni kitendo cha kuchokoa au kupitisha kijiti au kitu mahali kuona kuna nini. Pia ni usumbufu.

Pweza ni samaki ambaye huishi kwenye sehemu zenye miamba baharini. Ili mvuvi aweze kumnasa pweza, itabidi achokoechokoe majini na katika sehemu zenye miamba baharini ili hatimaye pweza atoke alimojificha ili anaswe na mvuvi. Mvuvi huwa na uhakika kuwa pweza atatokea amnase, na kwa sababu hii basi mvuvi atakuwa amefanikiwa katika malengo ya utendakazi wake na kwa hivyo hatachoka kuchokoa sehemu ambazo pweza hupatikana ili hatimaye afaulu kumnasa.

Njia rahisi ya kumnasa pweza katika mazingira yake ni kwa kuchokoachokoa majini na sehemu aishimo ili kumfanya atoke alikojificha ndiposa akamatwe.

Binadamu kwa upande wake ni tofauti na pweza. Tofautii hii husababishwa na hali kwamba tabia ya binadamu haitabiriki. Kupitia mambo wanayoyapitia katika nyakati tofautitofauti za maisha, tabia na mienendo ya binadamu nayo hubadilikabadilika. Tabia na mienendo hii ya binadamu katika nyakati tofautitofauti hufanya ubashiri na uelewa wa hali, tabia na mienendo ya binadamu kuwa mgumu sana.

Methali hii inaonyesha kwa uwazi tofauti za kitabia zilizopo kati ya binadamu na pweza katika mazingira yao. Ukimsumbua pweza kwa kuchokoachokoa majini utampata, hali ambayo ni tofauti na binadamu ambaye huwa ni mgumu kumwelewa kitabia.

## 10. CHOMBO CHA SAMAKI HAKIACHI KUNUKA VUMBA

Wamitila (2001:65) wanasema kuwa vumba ni harufu ya samaki baada ya kutolewa kwenye maji. Pia harufu hiyo ya samaki huitwa shombo.

Chombo ni kitu chochote cha kufanyia kazi (TUKI 2013:68). Hivyo basi katika hali hii, chombo chochote kile ambacho kina mahusiano na samaki hunuka vumba.

Methali hii imeteua na kulitumia neno ‘samaki’ kwa maana kwamba, bora awe ni kiumbe anayeishi ndani ya maji ana mapezi na mkia basi hunuka vumba anapovuliwa. Neno hili limejumlisha sifa ya samaki wote baharini, maziwani na kwenye mito. Samaki wote huwa na harufu mbaya wanapovuliwa katika mazingira yoyote yale. Mahusiano yaliyopo kati ya sifa hii ya samaki wote katika mazingira yao inaonekana na pia kwamba, chombo chochote kinachohusishwa na samaki hubainika bila tatizo lolote kwa sababu ya vumba litokalo kwenye chombo hicho.

## 11. CHOMBO KILICHOPIKIWA SAMAKI HAKIACHI KUNUKA VUMBA

Chombo ambacho kimetumiwa kumpikia samaki huwa kinatoa harufu ya samaki. Samaki yeyote yule huwa na harufu, hivyo msamiati uliotumika katika methali hii unaoana na ule wa methali,‘chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba’. (2.1.10)

## 12. CHURA AKITUPWA MAJINI HAFI

Chura ni mnyama mdogo ambaye hurukaruka sana na kukoroma kwenye vidimbwi na pia kwenye mabwawa ya maji hasa katika msimu wa mvua. Huwa na ngozi laini yenye unyevu na huwa na uwezo wa kuishi katika nchi kavu na pia majini.

Katika maelezo haya, tunapata sifa muhimu kumhusu chura. Chura ana uwezo wa kuishi katika nchi kavu na pia majini. Hapa basi, tunaona sababu ya uteuzi wa chura ambaye ana sifa ya uwili kimaskani, nchi kavu na majini. Ukimpata chura katika nchi kavu kisha umrushe majini, maeneo yote mawili kwa chura ni mamoja. Chura ataendelea kuishi tu. Methali hii inatubainishia uhusiano uliopo kati ya chura na nchi kavu na pia chura na maji. Mazingira ya chura ni yale yale katika nchi kavu ama katika maji. Hivyo uteuzi wa msamiati umeoana na mazingira ambamo chura huishi.

## 13. CHURA HUPENDA MAJI LAKINI SI MAJI MOTO

Maelezo kuhusu chura ni sawa na yale katika methali; chura akitupwa majini hafi.

Ukweli unabainika kuhusu mapenzi ya chura majini. Wakati wa majira ya mvua za masika, vyura husikika wakikoroma kwenye vidimbwi, mabwawa na maeneo mengine yenye maji baridi. Unapokaribia bwawa kwa mfano, utawaona vyura wakiruka na kujitosa bwawani.

Licha ya mapenzi haya ya vyura majini, maji moto huwa ni adui wa chura na wanyama wengine wote wa majini. Hivyo basi, ingawa chura hupenda sana maji, kuna kiwango ambacho mapenzi hayo ya chura hufikia (chura hupenda maji baridi wala si maji moto). Uteuzi wa msamiati katika suala la mapenzi ya chura na maji.

## 14. CHURA HUWEZA KUMWUA TEMBO

Katika maelezo ya chura, tumesema kuwa chura ni mnyama mdogo ambaye anao uwezo wa kuishi katika nchi kavu au pia kuishi majini.

Tembo kwa upande wake ni kiumbe ambaye ni kinyume kimaumbile na chura. Tembo au ndovu ni mnyama mkubwa anayeishi katika nchi kavu. Huwa na masikio makubwa tena mapana sana, mkonga yaani mwiro na mabori mawili kichwani na hula mimea.

Katika maelezo haya, tunaona hali mbili za kimaumbile katika methali hii; ukubwa wa tembo na udogo wa chura.

Wakati ndovu anapokunywa maji, chura anaweza akamuua kwa kujitosa katika mkonga wake; Wamitila (2001:70). Hali hii inaonyesha jinsi kiumbe mdogo kama chura alivyo na uwezo mkubwa wa kufanya mambo makubwa kama kumuuua ndovu ambaye ni mnyama mkubwa sana. Chura hupenda sana maji kama tulivyoeleza. Ndovu anapoenda katika milki ya chura, chura anao uwezo mkubwa wa kumtendea tembo huyo jambo kubwa ambalo hatimaye litamdhuru huyo tembo.

Uteuzi wa msamiati umeafiki ukweli wa mazingira ambamo wanyama hawa wawili huishi.

### 15. CHURA (HU)MZUIA MAJI NDOVU AKIYATAMANI

Methali hii ni sawa na ile ambayo tumeishughulikia, chura huweza kumwua tembo. Katika methali hii, ndovu huelewa kuwa chura ana uwezo wa kumsababishia madhara makubwa na hata kumwua tembo. Katika methali hii ndovu huelewa uwezo wa chura awapo majini. Ndovu hufahamu kuwa chura ana uwezo wa kumsababishia madhara makubwa na hata kumwua iwapo chura atajitosa katika mkonga wake. Hivyo basi, ndovu amwonapo chura majini, hawezi akayanywa maji yale hata kama anayatamani sana. Ndovu ataonelea heri akae bila kutumia maji yale kuliko kupata madhara makubwa kutoka kwa chura ambaye ni mnyama mdogo lakini ndiye anayeyamiliki maji hayo. Uteuzi wa msamiati hapa ulikusudiwa kuonyesha uhusiano wa wanyama wawili ambao wana maumbile tofauti lakini uamilifu wao ni kinyume cha maumbile yao.

### 16. DAGAA AMEMPONZA NDOBE

Dagaa ni samaki mdogo sana. Ndobe huishi kwenye maji baridi ya mito na maziwa; ana kimo kikubwa na anafanana na kambare. Katika uteuzi wa maneno haya ukweli unajidhihirisha kwamba dagaa na ndobe hupatikana katika maji baridi. (maana ni kuwa kuna samaki wakubwa kwa wadogo katika maji baridi, kama ilivyo katika bahari.). Dagaa ni samaki aliye na sifa ya kudharauliwa kwa sababu ya udogo wake.Si ajabu basi pale mvuvi anapowavua dagaa pekee

katika jarife lake, huenda asifurahi kama mvuvi anayenasa samaki wakubwa. Dagaa anapouzwa sokoni, huwa samaki wa thamani ndogo hivyo huuzwa kwa bei ya chini.

Kwa upande mwingine, ndobe ni samaki mkubwa ambaye anapovumiliwa huwa afueni kwa mvuvi kwa sababu ya ukubwa wake hivyo atauzwa kwa bei nzuri sokoni.

‘Amemponza’ ni kitenzi kilichotokana na mzizi ‘ponz’. Neno hili lina maana ya kuweka mashakani au matatani kwa kuletea shida. Katika uteuzi huu tunaona kuwa tabia moja walio nayo dagaa ni kukaa pamoja, ili wasidhulumiwe na samaki wakubwa kama vile ndobe ambao hutaka kuwakamata na kuwatumia kama chakula chao. Tabia hii ya dagaa ya kukaa katika makundi huweza kuwasaidia sana wasiliwe na samaki wakubwa. Samaki wakubwa nao kama ndobe hupata taabu sana katika kuwakamata dagaa ambao huungana na kuwa pamoja ili kujiepusha na adui zao.

Katika maelezo haya tuliyoyatoa, tunaona jinsi uteuzi wa msamiati ulivyofanikiwa katika utoaji wa sifa na tabia za samaki hawa wawili kwenye mazingira yao mahsusi. Tunaona kuwa umoja wa dagaa unawafaa katika kujiepusha na hatari ya kuliwa, japo wao ni wadogo, huku ndobe wakishindwa kuwakamata ijapokuwa wao ni wakubwa.

### 17. DUNIA MWENDO WA NGISI

Neno ‘ngisi’ kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013:423) ni mnyama wa baharini mwenye kichwa mfano wa ua lililochanua, mikono kumi mirefu na hutoa kiowevu cha rangi nyeusi.

Kutokana na maelezo haya tunapata sifa na tabia za ngisi. Kwanza ana kichwa mfano wa ua lililochanua, hali ambayo inafanya uteuzi wa samaki huyu kuwa mwafaka. Binadamu kwa kawaida hupenda maua. Maua huwa na rangi aina nyingi za kupendeza pamoja na harufu nzuri.

Pili ngisi ana mikono kumi. Ukweli wa mikono hii ni kuwa ngisi anaweza kwa mfano kujichukulia chakula kupitia mkono wowote ule kati ya mikono yake kumi. Ukweli huu unatokana na hali kwamba ngisi huishi majini na kwa hivyo chakula kinaweza kikatokea upande wowote ule, juu chini, upande, nyuma au mbele yake.

Tatu, tunaambiwa kuwa hutoa kiowevu cha rangi nyeusi. Kiowevu hiki cha rangi kulingana na Andambi (2005: 123) hutumiwa kama njia ya kujikinga. Kutokana na ukweli huu ngisi anapoogelea huutoa wino huo ili maadui zake wasimuone.

Hali kadhalika pana neno dunia. Dunia ni sayari ya tatu kutoka kwa jua. Humu ndimo unamoishi. Dunia huwa na mambo mengi ambayo huendelea ndani yake kwa waliomo humo.

Kwa mfano kuzaliwa. Kusoma, kuoa, magonjwa, vita, utajiri na umaskini. Hivyo methali hii inarejelea hali ya maisha duniani.

Kitenzi kilichotumika katika methali hii ni mwendo kutokana na mzizi end yaani kuondoka kutoka sehemu moja hadi nyingine. Ufaafu wa neno hili ni kuonyesha kuwa mambo duniani hayakai vile yalivyo daima na kwamba huweza kubadilikabadilika.

Tunapomrejelea ngisi kule baharini, anaweza kuonekana kwa hali tofautitofauti kama ua, mwenye mikono kumi na mtoa kiowevu cha rangi nyeusi. Kwa mfano anapofungua mikono yake huweza kuhadaa kuwa na kuonekana kama ua lililochanua na kumbe ni mikono ya kumkamata kiumbe na kumfanya kitoweo. Hivyo lile ua hugeuka na kuwa mauti. Tabia na sifa za ngisi zimefaa katika uteuzi wake katika methali hii.

Kutokana na maelezo tuliyoyatoa tunaona namna mazingira mahsusi yalivyoshamiri uteuzi wa msamiati uliotumika. Sifa, tabia na maumbile ya ngisi yamefanikisha uteuzi wake katika methali hii kwa mujibu wa mazingira yake ya baharini.

### 18. EWE MTUJE, KWAMBA WALI TAFI UNGALIKUWAJE?

Katika methali hii pametumika maneno mawili yanayorejelea samaki. Mtuje na tafi au chafi kutokana na maelezo tunayopata kutoka kwa kazi za wataalamu, mtuje ni samaki wa baharini ambaye huwa na miondoko ya kipekee baharini, kutokana na rangi yake ya kupendeza pamoja na madaha yake ya kipekee anapoogelea.

Tafi naye kwa mujibu wa Andambi (2005:123) ni aina ya samaki wa baharini aliye mweusi na mpana. TUKI (2013:54) inasema chafi ni samaki wa baharini wa kijivujivu, mpanampana na batabata. Umbo hili la tafi pamoja na rangi yake zinamfanya awe samaki ambaye havutii.

Pia neno 'ewe' limetumika kwa maana ya wewe. Katika neno hili, utenzi unadhihirisha kwamba anayelengwa ni mtuje mwenyewe. Hii inatokana na madoido pamoja na rangi za kupendeza alizo nazo mtuje. 'Wali' ni neno lililoteuliwa kumanisha,'kama ungalikuwa'.

Kutokana na maelezo haya, tunaona mtuje ni aina ya samaki ambaye ana miondoko ya kipekee pamoja na rangi za kuvutia. Hivyo basi, mtuje ni samaki maridadi sana baharini. Tafi kwa upande wake ni samaki aliye na umbo lisilopendeza pamoja na rangi isiyovutia. Kwa kuwatumia viumbe hawa wawili wa baharini, sifa, maumbile na tabia zao wahenga wanatuonyesha busara yao isiyo na kifani, ambayo inaonekana wazi katika msamiati waliouteua, unaoonyesha tofauti vinyume vya sifa, tabia na maumbile ya viumbe hawa wawili. Moja kwa moja tunaona vile ufanisi umeafikiwa katika uteuzi huu wa msamiati, ambao kusudi lake ni kuleta hali ya ulinganisho. Uteuzi huu unaonyesha kwa yakini mchango wa mazingira katika msamiati uliotumika. Tabia, sifa na maumbile ya viumbe hawa katika mazingira yao.

## 19. HASIRA YA MKIZI TIJARA (FURAHA) YA MVUVI

Katika methali hii neno mkizi ndilo linalorejele kiumbe wa majini. Mkizi kwa mujibu wa Wamitila (2001:99-100) ni "aina ya samaki ambaye ana hasira sana na kila anaposhikwa na nyavu za mvuvi hujirusharusha huku na huku na kwa njia hiyo kuishia kunaswa kabisa."

Andambi (2005:123) katika kumfafanua mkizi anasema kuwa ni samaki ambaye huwa na hasira sana na wavuvi wanapomnasa kwa nyavu zao, hurukaruka juu huku na huko kwa hasira na katika hali hiyo huishia kunaswa hata zaidi.

Ukweli wa mambo ni kuwa hatujui kama aliyo nayo mkizi ni hasira, ni uoga au hata ujasiri. Sababu iliyopelekea uteuzi wa msamiati huu wa samaki mkizi, ni ile tabia yake ya kurukaruka. Hata ukweli ukitukia kuwa mkizi huruka kwa sababu ya hasira, swali linaingia akilini mwetu, je ni nani ambaye hawezi akakasirika akichokozwa mastakimuni mwake au mahali popote pengine?

Maoni kuwa akikamatwa na nyavu za wavuvi ndipo mkizi hurukaruka inatukia kuwa kweli kwa sababu mazingira yake halisi huwa wavuvi wamehitilafiana nayo. Naye mkizi hurukaruka kwa ungo la kujinasua na kujirejeshea uhuru wake aliokuwa nao awali.

Hasira na furaha ni msamiati ambao umetumika kutubainishia ukweli ambao aghalabu huwepo katika jamii katika mazingira yake. Kwa mfano, kuna watu ambao hufurahia na kuchangamkia hali ambapo mtu fulani amekubwa na shida au hitilafu fulani. Kwa hivyo, uteuzi huu wa msamiati unaakisi hali halisi ya maisha duniani katika mazingira halisi ya kijamii.

Mvuvi katika methali hii imetumika kuwakilisha wafanyakazi katika mazingira yao ya kikazi. Ni kweli kwamba mazingira ya kikazi ya wavuvi ni baharini, pahali ambapo patawafanya wakumbane na viumbe wa majini kama vile samaki aina ya mkizi.

Maelezo haya basi yanatuonyesha wazi wazi kuwa uteuzi wa msamiati husika haukuteuliwa kivoloya tu, bali uliafiki sifa na tabia za viumbe wa majini katika mazingira yao.

## 20. HUNA MSHIPI, HUNA NGWE KUOMOA TENGA NI NINI?

Mshipi na ngwe ni kamba ambazo katika muktadha wa methali hii hutumiwa katika kunasa samaki, kuomoa ni kuchimba udongo kama vile maji yanavyomomonyoa na kufanya shimo (TUKI 2013: 441,550) Tenga ni samaki mkubwa mwenye umbo kama taa.

Methali hii imetumia msamiati ili kuleta hali ya ulinganisho. Ulinganisho huu unaonyesha hali za kinyume kati ya vifaa vya uvuvi na samaki ambaye anavuliwa. Mshipi na ngwe si dhabiti kiasi cha kuweza kumnasa tenga; hivyo swali, ‘kuomoa tenga’ ni nini?

Matumizi ya neno tenga ni kumrejelea aina moja ya samaki mkubwa ambaye hunaswa kwa kutumia vifaa thabiti vya uvuvi, kutokana na ukubwa wa samaki huyu, basi nguvu zake nazo ni nyingi na kwa hivyo hubidi mvuvi utumie vifaa vya uvuvi vilivyo imara ili afanikiwe kumnasa tenga.

Mvuvi ambaye hana hata mshipi wala ngwe, atajitia vipi katika uvuvi wa samaki mkubwa kama tenga? Mvuvi huyo hatafanikiiwa kwa sababu ni lazima awe na vifaa vifaavyo kutekelezea kazi yake ya uvuvi, kwa sababu katika mazingira na maumbile ya tenga, ni sharti mvuvi awe amejiandaa vilivyo ili aweze kumnasa tenga, la sivyo hatafanikiwa kamwe.

Uteuzi wa msamiati katika methali hii umeafikia malengo ya kulinganisha hali mbili zilizo na sifa tofauti za kimaumbile.

## 21. KAA AKIINUA GANDO MAMBO YAMEKATIKA

Methali hii inamrejelea kiumbe wa majini aitwaye kaa, pamoja na sehemu au kiungo cha mwili wake kiitwacho gando.

Wamitila (2001:120) anatuambia kuwa, “kaa ni mnyama mdogo wa majini mwenye miguu zaidi ya sita na gamba mwilini”. Jino la kaa vilevile hujulikana kama gondi.

Kaa kwa kawaida huwa ni mnyama mdogo ambaye huenda hata asitambuliwe awapo baharini. Gando nalo huwa na manufaa makubwa kwa kaa huyo, kwa sabubu katika kulitumia gando lake, kaa huweza kunasa chakula kilichomo katika mazingira yake.

Msamiati mwingine uliotumika unahusu kukatika kwa mambo. Uteuzi wa msamiati huu ni ishara kuwa hali si hali tena kama ilivyokuwa kabla ya kuinuliwa kwa gando. Kaa huwa si yule yule mdogo kwa sababu gando Lake Linaponasa, mnyama aliyenaswa hawezi akajinasua.

Kutokana na ufafanuzi huu, tunaupata ukweli kwamba mazingira ni muhimu sana katika uteuzi wa msamiati, na hivyo basi sifa na tabia zinalandana na mazingira ambamo kiumbe husika hupatikana.

## 22. KAA MKUU NG’OMBE WA MAJI AKIINUA GANDO MWELEMEZE NANDA

Katika methali hii, msamiati unaoleta hali ya mfananisho umetumika. Kama tulivyokwisha kusema, methali hukusudiwa kuwasilisha ujumbe uliokamilika kwa kutumia maneno machache yaliyoteuliwa.

Kaa, kama tulivyokwisha kusema katika methali (3.1.21) ni mnyama mdogo wa baharini mwenye miguu sita au zaidi na gamba mwilini. Tulisema kuwa japo kaa ni mnyama mdogo, analo jino lenye nguvu sana linaloitwa gando.Kaa akikamata mnyama yeyote kwa gando lake, mnyama yule aliyekamatwa hata ajitahidi vipi hawezi akajinasua. Huwa gando liking’ata, hungata kwelikweli. Msamiati huu umetumika kutueleza kuhusu uwezo wa kaa (ambaye ni mnyama mdogo) katika mazingira yake ya baharini. Hivyo basi, neno “mkuu” linatuonyesha uwezo huo wake mkubwa majini, unaofananishwa na uwezo wa ngombe (ambaye ni mnyama

mkubwa) katika mazingira yake ya baharini. Hivyo basi neno ‘mkuu’ linatuonyesha uwezo huo wake mkubwa majini, unaofananishwa na uwezo wa ng’ombe katika nchi kavu.

Ng’ombe ni mnyama mkubwa mwenye nguvu na ambaye hufugwa na binadamu. Uwezo wa ng’ombe na nguvu zake hubainika pale anaporusha mateke kwa nguvu. Njia bora ya kujilinda kutokana na mateke hayo ya ng’ombe ni kwa kuweka nanda kati yako na ngombe huyo ili ujinusuru. Nanda ni kigongo cha panda.

Msamiatikatika methali hii, unatuonyesha jinsi uwezo na nguvu za mnyama mdogo kama kaa zinavyolinganishwa na za mnyama mkubwa kama ng’ombe. Viumbe wawili hawa, katika vimo vyao tofauti, huwa na uwezo sawa katika mazingira yao asilia. Basi uteuzi wa msamiati hapa unashabiliana na mazingira halisi. Uhusiano kati ya uwezo wa viumbe hawa katika mazingira yao halisi unabainika moja kwa moja.

**23. KAJIGEUZA CHACHANDU KUJIPALIA MAKAA**

Neno Chachandu kwa mujibu wa Andambi (2005:124) ni aina ya samaki. Katika kuulizia kwetu hapa na pale, tuliambiwa kuwa chachandu ni aina ya samaki ambaye huwa na mikono mingi inayoitwa minyiri. Anapokamatwa na wavuvi hutumiwa kama mlo. Wavuvi wanapomchoma, yule chachandu hujaribu kujiokoa kwa kutaka kutoka motoni. Katika harakati zake hizo za kujiokoa, minyiri yake hiyo huvuta makaa ya moto hadi kwenye mwili wake hivyo hujitia hatarini zaidi.

Pana kitenzi ‘kujipalia’ kinachotokana na mzizi ‘pali’. (TUKI 2013:447) inasema kuwa kitenzi hiki ‘palia’ kina maana ya, “kuweka makaa ya moto juu ya kifuniko kwenye sufuria kwa lengo la kupitisha joto juu ya chakula kipikwacho kama vile wali.” Kutokana na maelezo haya, tunaelewa moja kwa moja kuwa neno hili halikuteuliwa kisadfa katika methali hii, bali lilikuwa na maana fulani mahsusi.  Minyiri ya chachandu inapoyavuta makaa, huyavuta mpaka hata juu ya mwili wake wote, jambo linalomfanya kuchomeka kila sehemu ya mwili, kwa kuwa makaa ya moto huwa yamefunika mwili mzima, juu na chini ya mwili wake.

Kujigeuza ni hali ya kuwa na kitu, dhana, tabia,maumbile na kadhalika kutoka hali moja hadi nyingine. Neno hili linatupa hali halisi ya mazingira ya chachandu, ambaye kwa kawaida huwa

hayuko katika hatari ya kuchomwa moto. Akiwa baharini, minyiri yake humsaidia katika shughuli zake za kutafuta chakula na kuogelea, hivyo, minyiri humsaidia chachandu kuishi katika mazingira yake halisi.

Msamiati huu unatupa ukweli ambao humpata chachandu anapobadilishiwa mazingira yake halisi na kuwekwa kwenye mazingira mengine tofauti. Minyiri ambayo huwa msaada wake baharini hugeuka na kuwa ya maana tofauti katika mazingira mapya. Minyiri yake chachandu huchangia maangamizi ya chachandu anapotiwa motoni. Methali hii basi imefanikiwa kuleta uhalisi wa mazingira katika methali hii. Kutupa uhusiano uliopo kati ya chachandu na mazingira tofauti.

## 24. KAMBARE MKUNJE ANGALI MBICHI

Kambare ni samaki wa mtoni au ziwani mwenye masharubu na kichwa bapa (TUKI 2013:189) Katika uteuzi wa msamiati huu, kambare ni samaki mmoja kati ya samaki wakubwa wa maji baridi. Katika uteuzi huu ambao unamrejelea kambare aliyevuliwa anafaa kukunjwa akiwa angali mbichi, la sivyo kambare atavunjika. Hivyo azimio la kumkunjakambare halitafaulu. Mazingira yanadhihirishwa katika methali hii kutokana na ukweli kuwa kambare akiwa majini ambayo ndiyo mazingira yake, hamna haja ya kumkunja lakini ukimtoa katika mazingira yake ya kawaida, basi itabidi umkunje.

## 25. KANGAJA SIMLE, MCHUZI KITOWEO

Kati ya samaki wenye vumba au harufu kali, mmoja wao ni kangaja. Hii ndiyo sababu Andambi (2005: 125) anasema kuwa “Kangaja ni aina ya samaki aliye na harufu mbaya.”

Kutokana na maelezo haya, tunaelewa kuwa kangaja ni samaki kama wale wengine, ila ana sifa moja kuwa ana harufu mbaya au vumba kali. Sifa hii ya samaki huyu ndiyo chanzo cha uteuzi wake katika methali hii. Ili kubainisha sifa hii ni kitenzi kilichotumika ‘simle’. Kitenzi “simle” ni ukanusho wa hali yakinishi ‘mle’. Kitenzi hiki kinatilia nguvu na kukubaliana na sifa ya harufu mbaya. Kwa kawaida binadamu hupenda harufu nzuri, huku harufu mbaya ya kukirihi, ikichukiza. Hivyo basi, si ajabu kwamba mtu hangependa kumla kangaja kwa sababu ya harufu yake mbaya.

Mchuzi ni neno jingine lililotumika kwa maana ya kitoweo cha majimaji kilichopikwa kwa kuchanganya kwa mfano nyama, samaki, mbogamboga pamoja na viungo kama bizari, vitunguu, mafuta au nyanya. TUKI (2013:330) Hivyo basi, mchuzi ni kitoweo ambacho TUKI (2013:250), inasema ni "Kitu kama vile mchuzi, mboga, samaki au nyama kinachotumiwa kwa kulia chakula."

Kutokana na maelezo haya, tunafahamu kwamba mchuzi ni sehemu muhimu sana katika mlo. Hutumika kwa kulia chakula kingine kama vile sima na wali.

Kangaja ni samaki ambaye licha ya kuwa na vumba kali katika hali yake ya kawaida, huweza kutumika kwa mapishi ambapo huunga mchuzi mtamu sana ambao hutumika kama kitoweo. Mtu anapotumia mchuzi ule huwa anaufurahia sana, ijapokuwa umepikwa kwa kutumia kangaja ambaye ana harufu mbaya (vumba kali).

Uteuzi wa msamiati huu unatubainishia jinsi sifa mbaya au hali isiyoridhisha huweza kuwa na matokeo mema. Hapa tunaona jinsi sifa ya kangaja ya kuwa na vumba kali katika mazingira yake halisi inabadilika na kuwa sifa ya kuwa na kitoweo kitamu sana.

## 26. KASIRANI YA MKIZI NI FURAHA KWA MWENYE TANDO

Wamitila (2001:124) anasema kasirani ni hasira inayoandamana na matendo. Tando ni wavu. Wavu hutumiwa na wavuvi katika shughuli zao za kuwavua samaki.

Mkizi anapokasirika, huruka juu kwa sababu ya hasira zake, jambo ambalo humfurahisha mwenye tando (wavu). Methali hii imetumia msamiati uliosawa na ule ulio katika methali; "hasira za mkizi furaha (tijara) ya mvuvi".

## 27. KIBOKO ALIYEPASHA HABARI HAPASUI MTUMBWI

Wamitila (2001:129) anaeleza kiboko kuwa mnyama mkubwa na mnene anayeishi katika maji baridi.

Mtumbwi ni chombo kilichotengenezwa kutokana na gogo la mti, na hutumika katika usafiri wa majini. Katika maeneo waishio Waswahili na jamii nyingine ziishizo karibu na maeneo yenye

maji kama vile mito, mitumbwi hutumika katika usafiri kwa kuwa ni njia ya haraka kusafiri kuliko kutumia miguu.

Kiboko ni mnyama aliye na tabia ya kuwashambulia wanadamu na kuwaua. Watu wengi wamejeruhiwa na viboko, kutokana na tabia ya viboko ya kuwashambulia watu bila habari, hasa kwa kutokeza ghafla kutoka vichakani na kushambulia.

Binadamu wanapomuona kiboko na kusikia vishindo vyake kwa mbali kabla ya kuwafikia, huweza kukimbilia usalama wao na kujiokoa wasiuawe na kiboko huyo. Watu hujiokoa kutokana na ghadhabu za kiboko wanapopata habari mapema kabla ya kiboko kuwashambulia. Wanapojinusuru, na kutoroka, kiboko hupata mtumbwi ambao hauna wasafiri, na kwa hivyo hawezi akaushambulia na kuupasua. Uhusiano uliopo kati ya kiboko na upasuaji wa mtumbwi hutegemea wasafiri walio katika mtumbwi huo.

Katika methali hii tunaona jinsi uteuzi wa msamiati ulivyoafiki mazingira ambamo umetumika. Mtumbwi aghalabu hutumika katika usafiri wa mito na ziwani, sehemu ambayo si mbali sana na upwa.

## 28. KILA KIBOKO NA KIVUKO CHAKE

Kiboko ni mnyama mkubwa sana ambaye huishi katika maji baridi mchana, na hutoka usiku kujitafutia lishe. Wanapokuwa majini, kila kiboko huwa na mahali pake anapoishi, aidha pawe ziwani mtoni, bwawani au dimbwini. Kila arudipo kutoka katika nchi kavu akikoenda kula nyasi, hurudi palepale ambapo huwa anaishi. Anapotoka katika makazi yake, kiboko huwa na njia yake ya kutokea na pia kuingilia majini.

Msamiati huu unatupa ukweli kuhusu tabia za viboko katika mazingira yao halisi. Hivyo basi, tunaona kuwa mazingira yana uhusiano mkubwa mno katika uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali hii.

## 29. KILA MVUVI WA PWEZA TUTAONANA MWAMBANI

Mwamba pia huitwa jabali. Jabali laweza kupatikana majini au pia katika nchi kavu. Andambi (2005:125) anatueleza kuwa pweza samaki aliye na umbo la duara lililozungukwa na minyiri au mikono minane. Makazi ya pweza ni katika miamba.

Mvuvi ni mtu anayefanya kazi ya kuvua samaki kwa kawaida, uvuvi wa samaki huhusu urushaji wa nyavu katika sehemu za maji ambazo hazina miamba. Mvuvi anayevua katika sehemu zisizokuwa na miamba atawanasa samaki wengi isipokuwa pweza.

Mvuvi anapotaka pweza, ni sharti aende miambani akamsake. Pweza naye hujificha miambani ili asikamatwe na mvuvi. Katika kumvua pweza basi mvuvi lazima awe hodari katika kazi yake, ndipo aweze kumpata huyo pweza. Kupitia uvuvi wa pweza basi, wavuvi hodari hutambulika.

Mazingira halisi aishimo mtu huamua aina ya uhodari wa mtaalamu katika mazingira hayo. Kila mtaalamu ni sharti afike kwenye mazingira yale ili majukumu yake yafaulu, hivyo uteuzi wa msamiati ulifanikiwa kabisa. Wataalamu wanaojisifia kazi fulani hawana budi kukutana katika maeneo yao ya kazi. Wanakutana katika maeneo yao kuonyesha uhodari wao na hivyo basi kujitofautisha na watu wengine wasiokuwa na uhodari kama wao.

## 30. KILICHOMPATA NGWENA NA KIBOKO NI HICHO

Ngwena ni mamba. Maelezo kuwahusu ngwena na kiboko ni sawa na za methali (1 na 26).

Viumbe hawa wawili huishi katika maji baridi. Kwa kawaida wao huwa ni majirani majini. Katika hali hii basi, chochote ambacho kitampata ngwena na kiboko hakitamsaza. Kwa mfano; maji ya mto yakichafuliwa ngwena na kiboko wote wataathirika. Pia, wakati wa kiangazi, mto wenye ngwena na kiboko unapokauka viumbe wote wawili watakuwa mashakani.

Uteuzi wa msamiati katika methali hii umetupa uhusiano wa viumbe ambao huishi katika mazingira mamoja. Baharini kuna wanyama wa aina nyingi, lakini maji ya bahari hayakauki kama maji ya baadhi ya mito yenye ngwema na kiboko, hivyo ukweli katika uteuzi wa msamiati unaoana na majira tofauti ya hali ya anga; hivyo uhusiano kati ya majira na athari zake kwa viumbe walio katika mazingira fulani unaonekana.

## 31. KITATANGE HUTIA CHAFI LEMANI

TUKI (2013:248) inasema kuwa kitatange ni samaki ndogo wa umbo la duara, mwenye rangi ya manjano iliyochanganyika na nyeupe, na pezi lililotanda mgongo mzima, mwenye tabia ya kuwasakiza wenziwe kwenye mtego kama vile dema kisha, yeye anatoka.

Lema pia huitwa dema. Dema ni mtego ambao wavuvi huutumia kunasia samaki na huwa limefumwa kwa kutumia vijiti.

Tabia ya kitatange katika ufafanuzi wake inabainika bila wasiwasi wowote. Kitatange ana tabia ya kuwaongoza samaki wengine kama vile chafi hadi kwenye dema ambapo wananaswa.

Wamitila (2001:145) anatoa maelezo ya kitatange kuwa "samaki mdogo mjanja ambaye ana mazoea ya kuwaongoza samaki wengine kwenye mtego lakini mwenyewe akaepuka". Kutokana na maelezo haya, tunaelewa moja kwa moja kuwa kitatange huwatia samaki wengine hatarini kisha mwenyewe akaiepuka hatari hiyo kwa kutoka na kukwepa. Huenda ikawa samaki wanaotiwa kwenye dema ni wa aina nyingi, wengi wao ambao ni wakubwa kuliko kitatange.

Katika methali hii, uteuzi wa msamiati umelenga kueleza kinagaubaga maumbile na tabia ya kitatange. Kimaumbile; kuwa ni samaki mdogo lakini kitabia ni samaki mwenye ujanja mwingi ambao hatimaye huishia kuwatia samaki wenzake wakubwa kuliko yeye matatani.

## 32. KUMLA NGURU SI KAZI, KAZI NI KUMWOSHA

Katika methali hii, msamiati wa kiumbe wa majini 'nguru' umetumika. Nguru kwa mujibu wa TUKI (2013:426) ni 'samaki mkubwa mrefu wa maji ya chumvi mwenye umbo la mviringo, rangi ya kijivu mgongoni na nyeupe tumboni.' Andambi (2005: 125) anatuambia kuwa nguru ni samaki ambaye 'huwa na harufu kali.' Kutokana na maelezo haya, tunaelewa kuwa nguru ni samaki ambaye ana harufu kali, na kama tulivyokwisha kusema, hakuna binadamu atakaye harufu mbaya. Kwa sababu hii, kazi ya kumwosha nguru huwa ni kazi kubwa. Itambidi mtu kutumia muda mrefu kumwosha samaki huyo ili harufu hiyo yake ya kukirihi yaani kuchukiza iondoke.

Tunabaini katika msamiati wa methali hii kwamba hata baada ya kuchukua muda mwingi kumwosha nguru, ulaji wake bado huwa kazi kwa sababu harufu yake yote huenda bado ikawa haikutoka.

Sifa hii ya nguru inaupa mshikamano na mazingira halisi hivyo uteuzi wake ulifaa katika kufanikisha mawasiliano katika jamii, ambapo matokeo yanayonasibishwa na hali za mazingira yameangaziwa.

## 33. KUMLA NGURU SI KAZI, KAZI NI KUMTOA MAGAMBA

Msamiati katika methali hii unatubainishia ukweli uliopo kumhusu nguru. Nguru ni samaki ambaye ana mamba mwilini mwake na pia ana harufu kali wakati wa kumvua na hata kula. Kwa sababu hii, nguru ni samaki ambaye huhitaji muda mwingi ili awe tayari kupikwa na kuliwa. Maumbile haya ya nguru yanamfanya awe samaki ambaye anafaa katika utumizi wa methali hii. Nguru huwapa watu muda mwingi wanapomtayarisha na pia wanapomla.

## 34. KUVUA NUMBI SI KAZI, KAZI NI MAGAWIONI

Kwa mujibu wa TUKI (2013:431) ‘numbi ni samaki anayefanana na kolekole, lakini mfupi na ana mstari wa buluu mgongoni.’ Ili tuiweze kumuelewa numbi kwa uyakinifu, tumuangalie kolekole ni nani ambapo pia (TUKI 2013:261) inatuambia kuwa kolekole ni ‘samaki asiye magamba mwenye umbo bapa rangi ya fedha na mkia mwembamba mrefu.’

Maelezo haya yametupa mwangaza kuhusu sifa ya numbi kuwa ni samaki asiye na magamba mwilini mwake.

Aina nyingine za samakiaghalabu huwa na magamba miilini mwao. Wavuvi wanapowavua samaki wenye magamba huwa kazi kubwa ya kuwapara na kuwaosha samaki wale inapatikana. Katika kuwapara na kuwaosha magamba huwa yanatolewa ndipo wale samaki wawe tayari kwa matumizi yaani kupikwa, kukaushwa au kuuzwa.

Numbi kwa upande wake huwa tayari kwa matumizi pindi tu anapovuliwa (angalau huwa hawezi kuparwa ili kutolewa mamba) Kwa sababu hii wavuvi wengi huenda wakashirikiana katika

kuwavua numbi, kwa sababu wana ufahamu kuwa pindi wanapowavua hawatakuwa na kazi kubwa ya kuwaandaa samaki wale kwa matumizi kama samaki wengine wenye mamba walivyo.

Magawioni ni sehemu ambapo wavuvi hukutana ili wagawe samaki ambao wamewavua. Katika hali hii wavuvi huenda wakawa wamewavua samaki aina tofauti tofauti, wengi wao wakiwa wana mamba. Wanapowagawa samaki wenye mamba, wavuvi huwa wanakubaliana, kila mvuvi na sehemu yake. Wakati wa kugawa numbi, huenda wavuvi wakachukua muda mrefu kwa sababu ya kutoelewana. Hali hii husababishwa na yale maumbile ya numbi kuwa samaki asiyekuwa na magamba.

Sifa hii ya numbi inaleta ukweli wa mazingira halisi ya makazi yake na kwa hivyo tunaona jinsi uteuzi wa msamiati huu ulivyofaulu kwa kuleta uelewa na mahusiano kati ya wavuvi na mazingira yao ya kikazi pamoja na sifa hii ya numbi.

## 35. MAJI MAREFU MWULIZE CHURA

Katika maelezo ya chura, rejelea methali “Chura akitupwa majini hafi”.

Maji marefu ni maji ambayo yana kina kirefu. Katika maelezo yetu ya awali, kuhusu chura ni kuwa chura ni kiumbe ambaye hupenda maji sana. Wakati wa mvua, chura hukoroma kwenye vidimbwi vya maji, kwenye visima, mito na maeneo mengine yenye maji baridi.

Wanadamu hutumia maji baridi katika shughuli zao za kila siku. Watu huyapata maji hayo kwenye visima, vidimbwi, mito na kadhalika. Katika kuyapata maji hayo, watu wakati mwingine huyapata katika sehemu ambazo maji yenyewe hayana kina kirefu na wakati mwingine huyapata katika sehemu ambazo maji yenyewe yana kina kirefu.

Kilindi cha maji baridi aghalabu hutegemea majira na misimu hivi kwamba wakati wa msimu ya masika maji yanakuwa mengi na msimu wa kiangazi maji hupungua au kukosekana katika maeneo ambayo huwa yanapatikana.

Hali kadhalika, chura ni kiumbe ambaye hawezi akawadhuru wanadamu; tofauti na wanyama wengine kama mamba na kiboko ambao ni maadui wa binadamu.  Hivyo, kwa kumtumia chura, methali hii inabainisha ukweli kuwa chura ni kiumbe asiye na madhara yoyote kwa binadamu.

Isitoshe, chura aghalabu hupatikana katika maeneo yote yenye maji baridi, tofauti na viumbe wengine wa maji baridi kama mamba na kiboko ambao hawapatikani katika maeneo yote yenye maji baridi. Kwa sababu hii, tunaona kuwa msamiati katika methali hii unaturejesha katika mazingira ambamo binadamu hupatikana. Kwa kuwa binadamu hawaishi tu karibu na maeneo ya mito na maziwa yenye maji baridi kule kwenye viumbe wengine wa majini kama mamba na kiboko, bali pia wao huishi katika maeneo ambamo maji baridi si mengi, na katika maji kama yale utawapata vyura, hivyo basi mahusiano kati ya mazingira na kiumbe aliyeteuliwa na kutumika katika methali hii yanafaulu.

## 36. MAMBA HUTOKA MAJINI NA KULAMBA UMANDE

Katika maelezo yetu ya awali kuhusu mamba kama vile katika methali ya (1.) tumeona kwamba mamba amepewa sifa ya kuwa mfalme wa majini, na kwamba maji ni sehemu ya maisha ya mamba.

Kutokana na sifa hii ya mamba na ukuruba wake na maji, mamba anafaa katika methali hii. Mamba ndiye mmiliki wa maji mengi baridi ambayo yeye huishi.

Licha ya wingi wa maji hayo, mamba hutoka majini na kulamba umande. Wakati wa majira fulani ya mwaka huwa tunapata unyevu, aghalabu wakati wa asubuhi ambapo unyevu huo hutanda juu ya majani na nyasi. Mamba huyaacha maji yake mengi na kuyafuatia yale maji madogo kama ya umande. Hii inaweza kuelezwa kama ishara ya mamba kutotosheka na maji yake mengi na kutaka hata yale ya umande.

Umande huwa kiasi kidogo sana cha maji ukilinganisha na maji ya mto au ziwa anamoishi mamba. Hivyo basi swali linajitokeza ni, “je, mbona mamba alambe umande?”

Katika kulijibu swali hili, tunakubaliana na hali kwamba majira tofauti kuwa na athari tofauti kwa mazingira. Huenda maji katika maeneo ambayo mamba huishi yakapungua au wanyama ambao huenda majini kunywa maji wakayakosa maji yale. Kwa sababu hii mamba atafanya lolote kumaliza njaa yake kwa kulamba umande; tofauti na kiumbe kama kiboko ambaye atasafiri mbali kujitafutia lishe. Katika methali hii basi, uhusiano kati ya mamba na mazingira yake unabainika.

## 37. MASKINI HAJUI KULA NA MKWASI, AKIANZA KULA SAMAKI HUANZA KICHWANI

Katika methali hii, kiumbe aliyetumika ni samaki. Samaki ni nomino inayojumlisha. Hakuna aina fulani ya samaki mahsusi ambaye amerejelewa.

Katika matumizi ya neno hili tunapata uelewa kuhusu maskini na tajiri, huwa ni watu ambao wana mbinu tofauti za kufanya mambo yao, na kuwa wanapokutana kuyatekeleza majukumu yale pamoja, kila mmoja atatumia mbinu yake.

Katika jamii, tajiri huenziwa sana kuliko maskini, na ndiyo maana kuwa katika methali hii, kula kwa maskini kunaonekana kuwa si kwa  kawaida lakini kule kwa tajiri kuko sawa. Vile ambavyo maskini atafanya jambo lolote wakiwa na tajiri, jambo hilo la maskini litaonekana kuwa na kasoro na lile ta tajiri litaonekana kuwa sawa. Hivyo basi maskini hawezi akafanya jambo lolote mbele ya tajiri na liishie kuwa sawa.

## 38. MBIO ZA KASA SI MBIO LAKINI HUMFIKISHA AENDAPO

Kasa kwa mujibu wa Wamitila (2001:197) ni “mnyama wa baharini anayefanana na kobe”. Hivyo basi kasa ni mnyama wa majini anayemithilishwa na kobe, na ambaye huishi katika nchi kavu. Kasa ni kiumbe mwenye magamba makubwa mwilini na na pia hutaga mayai sawa tu na kobe.

Kutokana na maelezo haya, tunapata ufahamu kumhusu kasa. Ni mnyama afananaye na kobe. Kobe hujulikana kwa sifa ya kutembea pole pole. Kasa naye ana sifa hiyo ingawa yeye hasa ni wa majini naye kobe ni wa nchi kavu.

Kwa kawaida, mwendo wa kasa majini huwa ni wa pole pole ukilinganishwa na wa viumbe wengine kama vile papa. Licha ya mwendo wake wa pole pole, kasa mwishowe hufika alikokusudia kwenda.

Sifa hii ya kasa ya mwendo wa pole pole anapoogelea baharini imeoana na mazingira ya kasa majini anapolinganishwa na viumbe wengine, viumbe wengine hao wana mbio majini tofauti na kasa. Kasa naye hufaulu kufika alikokusudia kwenda sawa na viumbe wengine wa majini ambao

wana mwendo wa mbio. Hivyo basi, uelewa wa sifa hii ya kasa unafaa katika uteuzi wake kwenye methali hii.

## 39. MCHAGUA SAMAKI HUPATA ALIYECHINA

Kuchina ni kuharibika kwa kitu na hata pengine kuoza baada ya kukaa sana (Arege 2011:211). Kwa mfano: chakula kilichopikwa na matunda. Kuchagua ni hali ya kuteua kitu fulani katika kundi fulani kama vile nguo, viatu, samaki na matunda.

Katika methali hii uteuzi unarejelea neno la jumla 'samaki.' Neno hili basi linajumlisha aina zote za viumbe wa majini kwa kuwa wote wana sifa ya kuharibika na kuoza. Ukweli huu unaakisi ukweli kuwa samaki wote huharibika na hata kuoza baada ya kukaa kwa muda mrefu baada ya kuvuliwa.

Mtu yeyote ambaye huchelewa kutekeleza jambo fulani, mwishowe hatafanikiwa. Ukweli huu unadhihirika waziwazi katika uteuzi uliotumika katika methali hii. Kisawe cha methali hii ni 'mchagua nazi hupata koroma.'

Mtu anayechukua muda kabla ya kufanya uamuzi wake kuhusu samaki atakayemchagua mwishowe hupata Yule aliyeharibika. Hali hii inatokana na ukweli kwamba maeneo waishimo Waswahili ni maeneo yenye joto kali na kwa hivyo bidhaa za vyakula vikiwemo samaki huoza haraka.

## 40. MTAFITAFI HULA SAMAKI (NSWI), MTULIVU HULA NYAMA

Andambi (2005:126) anatuambia kuwa mtafitafi ni mtu anayezurura hapa na pale.

Katika utamaduni wa jamii ya Waswahili, samaki ni sehemu muhimu ya mlo wao wa kila siku. Si ajabu basi mtu anapokuambia, 'leo tumekula sima kwa samaki.' Kama zilivyo jamii nyingine zote duniani, ambapo huwa pana vyakula vya kawaida, na pia vyakula ambavyo ni maalumu ambavyo hutumiwa katika shughuli maalum. Hivyo basi katika jamii ya waswahili samaki ni sehemu ya mlo wa kawaida katika jamii hiyo.

Nyama kwa upande wake kilikuwa ni chakula adimu katika jamii ya Waswahili. Tofauti na jamii kama ya Wamaasai ambayo shughuli zake za kiuchumi aghalabu ni ufugaji hivyo nyama kuwa

sehemu ya kawaida ya mlo wao, jamii ya Waswahili katika shughuli ya ulaji nyama ilikuwa nadra sana, labda pawe jambo au mtu ambaye si wa kawaida katika jamii ile. Nyama ni chakula ambacho huenziwa sana na jamii nyingi ulimwenguni.

Kutokana na mujibu wa methali hii basi, samaki ametumika kuwakilisha hali ya kawaida, nalo neno nyama limetumika kuwakilisha hali ya kipekee. Mtu asiyetulia katika kutekeleza majukumu yake huwa yumo katika hali ile ile ya kutoweza kusonga mbele na kufaulu. Watu katika janibu zile watamzoea kutokana na tabia zake kuwa kwa kawaida hatulii kama ilivyo kawaida kupata samaki katika jamii ya Waswahili.

Kwa upande wa pili, mtu ambaye hutulia na kutekeleza majukumu yake ipasavyo anamithilishwa na sherehe ya kufana iandaliwayo mtu wa kipekee anapomtembelea mwenyeji waake. Akifika kwa mwenyeji wake hataandaliwa samaki ambacho ni chakula cha kawaida bali ataandaliwa nyama ambacho ni chakula kitumikacho katika sherehe na kwa watu maalumu.

Methali hii basi hutumiwa kumithilisha sifa na tabia za watu katika mazingira yao ya kijamii. Hivyo basi, msamiati ulioteuliwa na kutumika unaoana na mazingira halisi ya jamii, uhusiano wa watu wenye tabia tofauti katika jamii umeafikiwa kwa matumizi ya methali yenye msamiati huu. Samaki anawakilisha hali ya kawaida katika jamii ya Waswahili, huku nyama ikitumika kurejelea hali maalumu katika jamii ya Waswahili. Methali hii inatueleza uhusiano uliopo kati ya Waswahili na vyakula vyao.

### 41. MVUVI NDIYE AJUAYE PWEZA ALIPO

Pweza ni kiumbe wa majini ambaye huishi sehemu zenye miamba baharini. Ili kumpata pweza huyo, mvuvi ambaye ni hodari katika shughuli za uvuvi ndiye ambaye ataelewa sehemu bora zaidi kati ya miamba ambapo atampata pweza huyo. Ukweli huu unabainisha uteuzi wa msamiati katika methali hii. Ugumu wa kumpata pweza kati ya miamba ni shughuli ambayo inahitaji mvuvi aelewe kwa kina sehemu ambamo pweza huyo yumo. Hapa tunaona jinsi mazingira yameathiri uteuzi wa msamiati huu; kati ya pweza na makazi yake.

## 42. NGUVU YA MAMBA NI MAJI

Kama tulivyokwisha kueleza, mamba ni kiumbe ambaye amepewa hadhi ya kuwa mfalme wa majini. Hadhi hii imetokana na uhusiano wa karibu na pia hufanyia mawindo yake pale pale majini.

Katika methali hii, tunaona kwamba hadhi hii aliyotunukiwa mamba inamfanya ateuliwe tena katika methali hii. Mamba anapokuwa majini, huwa na nguvu na ujasiri mkubwa sana wa kupambana na kiumbe yeyote yule majini. Mamba huwavamia wanyama wakubwa na wenye nguvu kumshinda kama vile nyati.

Akiwa nje ya maji, mamba huwa hawezi kuwavamia wanyama kama hao, na anapowavamia akiwa katika nchi kavu, huwa ni vigumu kwake kufaulu kumnasa mnyama huyo na kumfanya chakula chake.

Katika methali hii, tunaona jinsi nguvu ya mamba inavyooanishwa na mazingira yake ya majini na wala si ya nje ya maji, ukweli ambao unadhihirishwa na viumbe ambao aghalabu hushindwa kujinasua wanapokamatwa na mamba majini.

Pia, mamba ametumiwa katika methali hii tofauti na kiboko, ambaye huenda wakati mwingine hasa nyakati za usiku asiwe majini hali ambayo ni tofauti na mamba. Kiboko hula nyasi na majani, naye mamba hula nyama. Hivyo basi ni sharti mamba awasubiri viumbe wanaoenda kunywa maji ndipo awakamate awale.

Wanadamu nao katika shughuli zao za kutafuta maji ya kutumia, kiumbe au mnyama ambaye watakutana naye aghalabu ni mamba, hivyo ufaafu wa msamiati uliotumika katika methali hii kwa kurejelea mazingira. Hii ni kwa sababu mamba anaweza kuwakataza wanandamu nafasi ya kuteka maji wakati wowote ule, mchana au usiku kwa sababu mamba huwa majini au karibu na maji tofauti na kiboko ambaye kuna wakati ambapo huwa mbali na maeneo ambayo maji yapo, hasa nyakati za usiku.

## 43. NGWENA NA MWENZAKE (MWINGINE) HAWAPATANI

Ngwena ni kisawe cha mamba. Mamba huwa na sifa ya kuwa mfalme wa majini, ambapo huwinda kiumbe yeyote ambaye hujitosa katika milki yake. Chakula kinapopatikana, ndipo uhasama unazuka kati ya mamba waliomo pale majini, kwa kuwa kila mamba anang’ang’ania lile windo. Katika hali hii basi, uhasama unazidi kwa kuwa kila mamba atatumia nguvu zake kupata windo lile.

Kwa kawaida, wafalme wawili hawawezi wakatawala ufalme mmoja kwa wakati mmoja. Hivyo basi, mamba ambaye ni mfalme wa majini hawezi akaelewana na mamba mwingine katika eneo lile la maji yale yale mamoja. Mamba hao watapigana huku kila mmoja akinuia kumshinda mwenzake ili awe mfalme wa eneo lile la maji.

Katika hali hiyo ya mashindano, mamba watashambuliana huku mmoja akitaka kumshinda mamba mwenzake ili apate umiliki wa maji na mawindo anayoyapata majini. Hapa basi, uteuzi wa msamiati na mazingira unaoana vizuri.

## 44. NYAMA WOTE WANGAWAKO, MKUZA PEZI NI PAPA

Pezi kwa mujibu wa Wamitila (2001:294) ni kiungo kinachomwezesha samaki kwenda na kinachokuweko mbavuni na mgongoni.

Papa ndiye samaki tu ambaye hufahamika sana baharini kwa sababu ya ukali wake. Papa hufanya mengi baharini kama kuogelea kwa vishindo. Hivyo viumbe wengine wa baharini hawafikiriwi sana. Methali hii ni sawa na: Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo.

## 45. PONO MMOJA AKIOZA HUOZA NA SHAZILE

TUKI (2013:465) inatuambia kuwa pono ni samaki wa baharini ambaye hupenda kukaa mahali penye mwani au mchipwi, mwenye umbo la mviringo na rangi mbalimbali, aghalabu za kijani, buluu au kijivujivu. Mara nyingi huwa katika hali ya utulivu kama kiumbe aliyelala.

Wamitila (2001: 310) naye anatuambia kuwa pono ni aina ya samaki mwenye umbo la mviringo anayekaa mahali kwenye mwani na mwenye rangi mbalimbali na ambaye hutamaniwa kwamba humletea mtu usingizi mwingi amlapo.

Maelezo haya yanatupa habari muhimu kumhusu pono; kwanza pono ni samaki mwenye rangi tofautitofauti ambazo huvutia sana macho ya mtazamaji. Mifano ya rangi za pono ni kijani, buluu na kijivujivu. Rangi hizi tofauti humfanya pono kupendeza kwa sababu ya umaridadi wake unaosababishwa na rangi zake hizo.

Pili, pono ni samaki ambaye huaminiwa kuwa humletea mtu usingizi mwingi amlapo. Huwa ni tumaini la kila mtu kwamba anapoenda kulala, basi atapata usingizi mzito ambao utamfaa sana. Watu hupenda kulala vizuri kwa kupata usingizi mzito, kinyume na kupata usingizi wa mang'amung'amu au kutopata usingizi kabisa. Huenda ikawa si ajabu kuwa watu humla pono nyakati za jioni kama chajio, ili walalapo usiku wapate usingizi mnono na kuleta ukweli wa msemo 'amelala usingizi wa pono'.

Tatu tunapata uelewa kuhusu tabia ya pono, kuwa mara nyingi huwa katika hali ya utulivu kama kiumbe aliyelala. Tabia hii ya utulivu humithilishwa na usingizi mzito aupatao mtu usiku.

Shazi ni mtungo wa vitu kama vile samaki, Wamitila (2001:310). Pono wanapowekwa pamoja basi tunakuwa na shazi la pono. Pono mmoja katika shazi aozapo, basi shazi lote linakuwa katika hatari kubwa ya kuoza pia. Uozo wa pono mmoja unaharibu uzuri wa shazi nzima.

Katika maelezo haya, tunaona kuwa sifa moja mbaya ya pono mmoja huharibu sifa nyingine zote zinazohusishwa na pono. Katika methali hii, uozo unaharibu sifa ya rangi nzurinzuri za pono pamoja na tabia ya utulivu ambayo pono huwa nayo.

Maelezo haya yanatusawiria jinsi mazingira yalivyoathiri uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali hii kwa kujikita katika sifa na tabia za kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii.

## 46. PWEZA KAMWAMBIA NGISI, 'TUSIFANYE MAJILISI, MAJI YAKIPWA TUKISI'

Pweza kwa mujibu wa Wamitila (2001:311) ni samaki mwenye umbo la duara na minyiri au mikiamikia. TUKI (2013:311) inasema kuwa pweza ni mnyama wa baharini mwenye umbo la duara lililozungukwa na mikono au minyiri minane.

Kumhusu ngisi, Wamitila (2001:311) anasema kuwa ni samaki mdogo mwenye umbo la duara ambaye hutoa rangi anapokumbwa na hatari. TUKI (2013: 423) inasema kuwa ngisi ni mnyama wa baharini mwenye kichwa mfano wa ua lililochanua, mikono kumi mirefu na hutoa kiowevu cha rangi nyeusi.

Katika ufafanuzi kuhusu viumbe hawa walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii, maumbile yao yanabainika waziwazi. Wao ni viumbe wenye mikono /miguu mingi, pweza ana minane naye ngisi ana kumi. Kutokana na maumbile haya, pweza na ngisi wanapoogelea baharini inakuwa ni rahisi kwao kuonekana na wavuvi kwa sababu ya maumbile ya miili yao. Mikono yao huenea katika pande tofauti za baharini hivyo kuwavua inakuwa kazi rahisi.

'Yakipwa' ni kitenzi kinachomaanisha kuondoka kwa maji ufukoni. Hali kama hii itokeapo pweza na ngisi wanakuwa windo rahisi kwa wavuvi kwa sababu ya maumbile yao. Ndipo wafaulu kuogelea viumbe hawa wanahitaji maji yenye kina kirefu. Kina cha maji marefu ni sehemu ambapo maji hayapwi.

'Tukisi' pia ni kitenzi kilicho na maana ya twende zetu au tuondoke. Wamitila (2001:311) Kwa mujibu wa maelezo haya, pweza na ngisi wanafaa kuwa tayari kuondoka ufuoni wakati wowote maji yakipwa, ili waepuke hatari ya kunaswa na wavuvi au kushindwa kuogelea maji ya bahari yakipwa.

Tunaona kuwa viumbe hawa wana adui mmoja ambaye ni mvuvi, na ili waweze kujinusuru wanashauriana kuhusu umuhimu wa kufanya wanalofanya mahali walipo wakati huo walio nao kisha waondoke kabla ya hatari ya kuvuliwa na wavuvi kuwafikia.

Hapo basi tunaona kuwa mazingira yamechangia utenzi wa msamiati uliotumika katika methali hii kwa sababu maumbile ya viumbe walioteuliwa yanafanana na wote wanaishi baharini na kuwa na adui mmoja ambaye ni mvuvi.

### 47. SAMAKI AKILIA MACHOZI YAKE HUPELEKWA NA MAJI

Katika methali hii neno samaki limetumika kuonyesha kuwa ni jumla. Samaki wote huishi majini. Shughuli zao zote hutekelezwa majini. Ni kutokana na ukweli huu ambapo samaki yeyote yule ana uhusiano na maji. Mazingira yake rasmi yamo majini. Kwa hivyo anapolia,

hakuna atakayefahamu kwa sababu machozi pia ni kimiminika kama maji yalivyo. Samaki anapotoa machozi machoni, machozi yale yanakuwa sehemu ya maji na hakuna yeyote atakayefahamu kuwa samaki huyo analia.

Uteuzi wa msamiati katika methali hii unaakisi ukweli wa mazingira ambamo samaki wote huishi. Wote kwa jumla bila kumrejelea samaki yeyote mahsusi. Hivyo, ukweli wa mazingira unabainika katika maneno ‘samaki’, ‘machozi’ na ‘maji’ na vitenzi ‘akilia’ na ‘hupelekwa’.

### 48. SAMAKI HUANZA KUOZA KICHWANI

Samaki yeyote yule aanzapo kuoza huanzia kichwani. Huu ni ukweli kwamba samaki yeyote yule asipohifadhiwa vizuri huanza kuoza, na akianza kuoza huanzia kichwani.

Katika methali hii, tunaona ukweli wa msamiati huu kwa kujikita katika mazingira ambamo samaki au viumbe wengine wa majini hupatikana.

### 49. SAMAKI MKUNJE ANGALI MBICHI

Msamiati katika methali hii unawarejelea samaki wote kwa jumla. Samaki yeyote yule asipokunjwa angali mbichi, basi kumkunja baadaye akishakauka haitawezekana kwa kuwa atavunjika tu.

Ukweli wa sifa ya samaki wote inajitokeza katika methali hii kuwa samaki wanavunjika wasipokunjwa mapema, wawe wakubwa au wadogo, wa maji baridi au wa maji ya chumvi. Sifa hii ambayo samaki wote wanayo imewezesha ueuzi wake katika methali hii kuwa unafaa kwa kunasibisha sifa hii ya samaki wote, wawe wa maji baridi au maji ya chumvi.

### 50. SAMAKI MMOJA AKIOZA, HUOZA WOTE

Katika methali hii, sifa ya ambayo imesheheni kwa samaki wote sawa na viumbe wote ni ile ya kuoza baada ya kufa, na kama tulivyoona katika methali, ‘pono mmoja akioza huoza na shazile’ ni kuwa samaki mmoja kati ya kundi la samaki anapooza basi wote huoza. Samaki mmoja aliyeoza huharibu sifa za samaki wenzake katika kundi lake hata kama hawajaoza.

Aina yoyote ile ya samaki huharibiwa sifa iwapo samaki mmoja tu katika kundi lao atakuwa ameoza, na kwa hivyo basi sifa hii imeakisi hali ya mazingira kiuhusiano. Uozo wa samaki mmoja katika kundi huhusishwa na kuoza kwa samaki wote katika kundi hilo.

### 51. SAMAKI MMOJA AKIOZA NI MTUNGO PIA

Mtungo ni kitita cha vitu kama vile shanga au samaki waliofungwa kwa kupitisha kamba, uzi au waya kwa kila kimoja cha vitu hivyo (TUKI 2013:394). Mtungo basi ni samaki waliofungwa pamoja. Msamiati wake ni sawa na methali (49) hapo juu .

### 52. SAMAKI WOTE HUNUKA WALIMSHUKU KAMBARE

Maelezo ya kambare ni sawa na yale ambayo tumeyatoa katika methali ya (25); 'kambare mkunje angali mbichi.'

Kutokana na maelezo hayo, kambare ni samaki wa maji baridi. Maji baridi huwa hayana chumvi. Chumvi ni madini ambayo hupunguza athari za harufu na kuoza kwa vyakula kama vile nyama na samaki. Maji ya mtoni au ziwani ambamo kambare hupatikana yameleta ukweli wa mahusiano kati ya mazingira ya kambare na uteuzi wake katika methali hii. Hivyo basi, kambare anatunukiwa sifa hii ya vumba kali kwa sababu ya mazingira yake ya maji baridi.

Hii inatupa sababu nzuri ya kambare kushukiwa kuwa na harufu kali kuliko samaki wengine, lakini ukweli ni kuwa samaki wote huwa na vumba. Maji baridi ambamo kambare huishi yanatupa ukweli wa mahusiano kati ya mazingira ya kambare na uteuzi wake katika methali hii. Hivyo basi, kambare anatunukiwa sifa hii ya kuwa na vumba kali kwa sababu ya mazingira yake, yaani maji baridi ambamo yeye huishi.

### 53. SHUKA YA MASKINI NDIYO ITANDIWAYO DAGAA

Dagaa ni aina ya samaki wadogo. Wamitila (319:2001) anatuambia kuwa maskini ni fakiri, fukara au mchochole. Mtu asiye na uwezo.

Hapa, tunaona jinsi uteuzi wa msamiati unavyoona na hali halisi ya maisha ya mwanajamii. Tunaona kuwa dagaa ni samaki mdogo sana ambaye anadunishwa akilinganishwa na samaki wengine. Kwa sababu hii basi vyombo au nguo za thamani (ambazo humilikiwa na wakwasi)

haziwezi zikatumiwa kuwahifadhia wale dagaa. Moja kwa moja, kitu duni huelekezwa kwa watu ambao ni duni pamoja na mali yao. (maskini na shuka lake).

### 54. TAA HAACHI MWIBAWE

Taa, kwa mujibu wa Wamitila (2001:327) ni samaki mwenye kinywa kilichochongoka kama mwiba. TUKI (2013:530) inasema kuwa 'taa ni samaki mkubwa mwenye umbo bapa na mkia mrefu.'

Maelezo haya yanatupa taswira nzuri kumhusu taa, kuwa ni samaki mwenye maumbile yanayofanana na mwiba mdomoni. Taa ana mwiba mwilini mwake. Umuhimu wa mwiba kwa taa ni kuwa ndicho kinywa cha taa mwenyewe. Licha ya ukweli kuwa mwili wa taa una umbo bapa, mwiba wake ni tofauti na samaki wengine kwa kuwa ni mviringo. Hata hivyo, mwiba huo ni muhimu sana kwa taa kwa sababu ndicho kinywa cha taa ambacho atakitumia katika shughuli zake za ulaji wa chakula.

Maumbile haya ya taa yanamfanya awe mmoja kati ya samaki wa kipekee baharini, tofauti na samaki wengine wenye vinywa vilivyochongoka, lakini wenye umbo la mviringo kama vile mchumbururu.

### 55. UKIKAA NA SIMBA, VAA NGOZI YA MAMBA

Methali hii ni sawa kimsamiati na,'ana nchi yake simba ana maji yake mamba'.

Viumbe hawa wawili wamepewa sifa ya kuwa wafalme katika milki zao, simba nchini na mamba majini. Kwa hivyo, unapokuwa kwa mfalme simba, vaa ngozi ya mamba ili simba akudhani kuwa wewe ni mamba. Kwa kufanya hivi, utafaulu kukaa na simba. Sifa za viumbe hawa wawili zinafaa kwa matumizi ya methali hii, hivyo basi uteuzi wa msamiati umefaulu kwa kurejelea mazingira wapatikanapo simba na mamba, na uhusiano uliopo kati ya viumbe hao na mazingira yao.

### 56. ULIMWENGU UMEMSHINDA KAA ENDAYE UPANDE UPANDE

Kaa ni kiumbe wa baharini mwenye miguu sita au zaidi, na ana uwezo wa kwenda upande wowote ule atakao, mbele, nyuma au upande upande.

Licha ya umahiri huu mkubwa alio nao kaa, bado ulimwengu umemshinda. Kaa kama viumbe wengine hukumbana na matatizo mengi, hivyo ulimwengu hauchagui umahiri au uwezo alio nao kaa na kumtenga kutoka kwa viumbe wengine. Tabia hii ya kaa ya kwenda upande wowote atakao baharini imefaa kwa matumizi katika methali hii. Tabia hii ya kaa katika mwendo wake ni ya kipekee kwa kaa, lakini ulimwengu unamtatiza kaa sawa na viumbe wengine wasiokuwa na tabia kama hiyo ya kaa.

### 57. UMEKUWA NGUVA HUHIMILI KISHINDO?

Nguva ni kiumbe mkubwa wa baharini, hula mwani na huwanyonyesha watoto wake. Ana mwili dhaifu sana Wamitila (2001:355). Nguva ni samaki ambaye hula mwani na huwa na mwili ambao hudhoofika haraka hasa baada ya kujeruhiwa.

Sifa moja muhimu tunayopata kutokana na maelezo tuliyoyatoa inaonekana, kuwa nguva ana mwili dhaifu dana. Kutokana na sifa hii, nguva hawezi akastahimili fujo, ghasia, pigo au jeraha mwilini mwake. Nguva anapopatwa na jeraha, linalofuata basi ni mauti.

Sifa hii ya nguva inatusawiria ukweli wa mazingira aishimo nguva na uhusiano uliopo kati ya mazingira yake na mwili wake. Hivyo mazingira yamechangia uteuzi wa msamiati huu kwa mujibu wa sifa hii ya nguva.

### 58. UMEONA WAPI MNANDI KUJENGA NYUMBA MACHWEONI

Mnandi ni ndege anayewala samaki na akaaye baharini, mtoni au ziwani. Wamitila (2001:356). Mnandi ni ndege ambaye hajishughulishi na ujenzi wa kiota au hata tundu la kuishi.

Machweo ni wakati wa jioni. Mnandi ni ndege ambaye daima hana kiota chake cha kuishi. Yeye huishi baharini, ziwani tofauti na ndege wengine ambao hujitafutia makao yao.

Hata wakati wa jioni jua lianapokuchwa, mnadi huwa hana haja ya kutafuta makao bali huendelea na shughuli yake ya uwindaji. Sifa hii ya kutojali kwa mnandi ndiyo sababu ya uteuzi wa msamiati huu katika methali hii. Mnandi ni ndege aliye na tabia tofauti na ndege wengine ambao machweoni hurudi viotani mwao, bali mnandi hubaki nje. Katika msamiati huu tunaona ukweli kuwa mazingira yamechangia uteuzi ambao unafaa katika methali hii.

## 59. UNGEENDA JUU KIBOKO MAKAZI YAKO PWANI

Kiboko ni kiumbe wa majini ambaye hutoka nyakati za usiku na kwenda kujitafutia lishe. Chakula cha kiboko ni nyasi na majani, hivyo basi kiboko hubidi atoke majini ili akajitafutie chakula hicho chake ambacho hakipatikani majini. Hata aende umbali gani, mwishowe atarudi pwani ndani ya maji, ambayo ndiyo makazi yake.

Kiboko ameteuliwa kutokana na tabia yake ya kutoka majini usiku kula kisha kurejea majini kabla ya mapambazuko, tabia hii inaoana na mazingira apatikanapo kiboko ya kuishi majini na kula nyasi usiku. Hivyo basi uteuzi wa msamiati huu umefaulu katika methali hii inayomrejelea kiboko.

## 60. USIKU KIZA MANGAZIBWE MTUMBUU HUWA PAPA

Mangazibwe ni hali ya kudanganyika au kuona kitu jinsi kisivyo. Mtumbuu ni samaki mdogo. Wamitila (2001: 363)

Wakati wa usiku kukiwa na giza kunakuwa na madanganyo mengi. Jambo dogo kwa kawaida ambalo halina hatari wakati kukiwa mwanga, linaweza kuonekana kuwa kubwa na la kutisha ajabu wakati wa giza.

Mtumbuu katika methali hii ni samaki ambaye kwa kawaida hana madhara kwa binadamu lakini wakati wa usiku huenda akatisha kutokana na giza ambalo humzuia mtu kutambua kiumbe huyo ni hatari, na chukulizi kwamba viumbe wakali huwinda nyakati za usiku.

Hivyo basi, tunaona namna mnyama ambaye kwa kawaida hatishi katika mazingira yake anavyogeuzwa na chukulizi alizo nazo binadamu na kuwa kiumbe mkubwa tena hatari. Hivyo kuna ufanisi wa mazingira katika uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali hii.

## 61. USO WA SAMAKI HAUSIKII VIUNGO

Samaki wote wana vichwa. Vichwa vya samaki wote vina sifa moja, hubakia vile vile baada ya kupikwa. Haya ni kwa mujibu wa Wamitila (2001: 368).

Katika upishi na maandalizi ya samaki, vichwa vyao hubakia vilevile hata uweke viungo vipi katika mapishi yako. Sifa hii ya vichwa vya samaki kutosikia viungo ni ya kweli wakati wa

kupika samaki. Hivyo basi mazingira ambamo samaki huandaliwa na kuliwa kama vile nyumbani yanaoana na ukweli huu. Kichwa cha samaki kitasalia kuwa vile vile tu kilivyokuwa; kikavu na hakitakuwa na ladha yoyote wakati wa kukila.

### 62. WAVU UTAKAONASA SAMAKI WENGI HUANZA MAPEMA

Wavu hutumuika na wavuvi katika shughuli yao ya uvuvi. Wavu unapowambwa majini, uwezekano wa samaki kunaswa unakuwa juu.

Katika methali hii, neno samaki limetumika kwa maana ya samaki wote kwa jumla, kumaanisha kwamba hakuna samaki ambaye hawezi akanaswa na wavu. Huu ni ukweli kwa sababu wavu hunasa samaki yeyote ambaye huingia wavuni.Ndiyo sababu samaki wa aina nyingi hunaswa na nyavu za wavuvi. Hivyo basi uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali hii ameakisi ukweli wa mazingira ambamo shughuli ya uvuvi huendeshwa.

### 63. WAVUVI WA PWEZA HUJUANA MWAMBANI

Methali hii ni sawa na, ‘kila mvuvi wa pweza tutaonana mwambani.’ Ambayo ni 3.1.29 katika kazi hii.

### 64. ZOBE NA MSUWELE WOTE NI WAMOJA

Kwa mujibu wa wamitila (2001: 389) Zobe na msuwele ni vinyama vya baharini ambavyo vina miguu (michacha) na mikono (migando) mfano wa kaa.

Zobe na mswele mi viumbe ambao wana uhusiano wa kimaumbile. Wote ni wadogo na wana miguu na mikono. Kufanana kwao kimaumbile kunafanya wawe na tabia zinazofanana kwa mfano katika mwendo huenda mwendo wao ukafanana kwa sababu ya michacha na magando waliyo nayo. Kufanana huku kimaumbile kumewapa viumbe hawa nafasi ya kuteuliwa na kutumiwa katika methali hii, ambayo inapelekea tabia na mienendo ya viumbe hawa kuwa sawa, hivyo zobe na msuwele wote ni wamoja kwa kuwa wote wana uhusiano mmoja.

### 3.2 HITIMISHO

Katika sura hii ya tatu tumefafanua methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Katika kuangazia msamiati ulioteuliwa na kutumika katika methali hizi za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini, ufafanuzi na maelezo yetu yanathibitisha ukweli kwamba msamiati uliotumika haukuteuliwa kisadfa tu, bali tabia, sifa, na maumbile ya viumbe hao yakitiliwa maanani na wanajamii. Katika ufafanuzi wetu wa msamiati ulioteuliwa na kutumika katika methali hizi, tumebainisha kuwa mazingira ni muhimu sana katika uteuzi na matumizi ambamo msamiati huo husika umelenga. Hivyo basi, mazingira ni sehemu muhimu sana katika ufanikishaji wa msamiati wa kiumbe fulani katika methali mahsusi.

# SURA YA NNE

## ATHARI KWA JAMII PAMOJA NA UAMILIFU WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI KATIKA JAMII

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tumefafanua msamiati ulioteuliwa na kutumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Katika sura hiyo, tumeifafanua kila methali kivyake. Ili kufanikisha lengo letu la ufafanuzi wa msamiati, tumejikita hasa katika kiumbe aliyeteuliwa na kutumika katika methali husika, huku tukiangazia tabia, sifa na maumbile ya kiumbe au viumbe walioteuliwa na kutumika katika methali hiyo. Hali kadhalika, tumeangazia maneno mengine katika methali husika katika baadhi ya methali, huku tukiwa na lengo la kuelewa kwa kina mambo yanayohusu methali kama vile wakati wa matumizi.

Katika sura hii ya nne, kwa kutumia nadharia ya mahusiano ya kina Sperber na Wilson (1995) tumechunguza na kubainisha athari kwa jamii pamoja na uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii ambamo lugha ya Kiswahili hutumika.

Nadharia ya mahusiano hushughulika na ufasiriwa matamshi au maandishi ili kupata maana iliyokusudiwa. Katika nadharia hii, athari za kiutambuzi za msikilizaji, uhusiano wake na mzungumzaji katika mazingira waliyomo, huchangia kufanikiwa kwa mawasiliano.

Katika sura hii ya nne, data yetu inawasilishwa kwa njia ya muhtasari kwa kutumia mbinu za maelezo, majedwali, baa grafu pamoja na pai chati.

Data hii ilikusanywa kutoka kwa walimu na wafanyakazi katika shule za msingi na upili za Naikarra. Katika ukusanyaji wa data hii, tulitilia maanani madhumuni yetu ya pili na tatu ya utafiti. Hivyo basi, ukusanyaji wetu wa data katika hojaji ulilenga kupata uelewa kuhusu athari zinazotokana na matumizi ya methali yenye kutumia msamiati wa kiumbe wa majini, na kutaka sifa au maumbile ya kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali husika. Isitoshe, tulinuia

kupata uamilifu wa methali zenye kutumia msamiati huo kwa jamii ambayo hutumia lugha ya Kiswahili.

Jumla ya hojaji hamsini zilipewa walimu na wafanyakazi, huku hojaji 40 ambazo zilijazwa kikamilifu zikirejeshwa. Hojaji zilizorejeshwa ni alisimia 80, ambazo tuliona zinatosha kufanya uchanganuzi katika sura hii.

## 4.2 HABARI YA WALIOJAZA HOJAJI

Katika sehemu hii, tulidhamiria kupata ufahamu wa waliojaza hojaji, kwa kuangazia umri wao pamoja na vituo vyao vya kufanyia kazi.

### 4.2.1 UMRI WA WALIOJAZA HOJAJI

Katika hojaji, tuliwaomba waliojaza watunukulie kifungu cha miaka yao. Kutoka kwa majibu yao ilionekana kwamba wengi wa walioshiriki katika kuijaza hojaji walikuwa umri kati ya 36 – 40, wakifuatiwa na hawa wafuatao kwa msanjari uo huo: 20-25, 31-35, 26-30, 45-50, 51 na Zaidi.

**Jedwali 4.2 Waliojaza hojaji kwa mujibu wa umri wao**

| **Umri** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| 20-25 | 9 | 22.5 |
| 26-30 | 7 | 17.5 |
| 31-35 | 9 | 22.5 |
| 36-40 | 10 | 25 |
| 41-45 | 0 | 0 |
| 45-50 | 3 | 7.5 |
| 51 na zaidi | 2 | 5 |


Kutoka kwa matokeo haya kama yalivyo katika jedwali hili, ni wazi kuwa watu wenye umri wa miaka thelathini na moja na kuendelea  ndio waliojaza hojaji kwa wingi kuliko wale wa umri wa miaka thelathini na kushuka. Hali hii huenda inatokana na ukweli kwamba methali ni fumbo na pia huwa na sifa ya kutumia msamiati wa kale, hivyo basi huhitaji msikilizaji au msomaji kufikiri sana ndipo apate uelewa wa yale mzungumzaji anayokusudia.

### 4.2.2 KITUO CHA KUFANYIA KAZI

Waliojaza hojaji walitakiwa kuonyesha kituo chao cha kufanyia kazi. Wale wa shule ya msingi waliojaza hojaji walikuwa 21 ambayo ni sawa na asilimia 52.5 ya waliojaza, huku 19 ambao ni sawa na asilimia 47.5 ya jumla ya waliojaza walitoka katika shule ya upili.

Hii yaonyesha katika grafu 4.2 chini.


**Grafu 4.2.2 Kituo cha kufanyia Kazi.**




## 4.3 MSAMIATI NA ATHARI ZAKE KATIKA MAZINGIRA MAHSUSI KWA MWANAJAMII AU WANAJAMII

Katika sehemu hii ya hojaji, washiriki walifaa kujibu maswali mawili:

Katika swali la kwanza, washiriki walitakiwa kueleza ikiwa mazingira huathiri uteuzi wa msamiati. Washiriki wote 40 sawa na 100% walikubali kuwa mazingira huathiri uteuzi wa msamiati. Pai chati ifuatayo inaonyesha maoni ya washiriki kuhusu nafasi ya mazingira katika uteuzi wa msamiati.





Katika swali la pili washiriki walitakiwa kuchagua athari ambayo hutokana na matumizi ya msamiati fulani katika mazingira mahsusi. Walitakiwa kuchagua jibu moja kati ya majibu haya matatu:

A. Athari chanya ( )
B. Athari hasi ( )
C. Athari chanya au hasi ( )

Katika majibu yao washiriki 3 ambao ni sawa na asilimia 7.5 walichagua athari chanya huku washiriki 37 ambao ni sawa na asilimia 92.5 wakichagua athari chanya au hasi.

Kutokana na majibu yao, inaonekana kwamba mwanajamii anaweza akapata athari chanya au hasi kutegemea mazingira aliyomo. Katika kuelewa nadharia ya mahusiano, msikilizaji (huufasiri) ujumbe kutegemea mazingira yake pamoja na uhusiano wake na mzungumzaji wake. Hata hivyo, baadhi ya washiriki walichukulia kuwa msamiati unapotumika katika mazingira yoyote yale huwa na athari chanya au hasi huku wengine wakichukulia kuwa msamiati huo husika huwa na athari chanya unapotumiwa katika mazingira yoyote yale. Hii huenda inatokana na chukulizo alizo nazo msikilizaji.

Kutokana na majibu haya, tunaona ukweli jinsi msamiati hufasiriwa kwa njia tofauti na watumizi lugha. Pai chati ifuatayo inaonyesha athari za msamiati katika mazingira mahsusi kwa mujibu wa washiriki.




## 4.4 ATHARI KWA JAMII KUTOKANA NA METHALIZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI

Katika sehemu hii, washiriki walitakiwa kuchagua athari ambayo wataipata kutokana na matumizi ya methali ambayo imetumia msamiati wa kiumbe ama viumbe wa majini. Hali kadhalika washiriki walitakiwa waeleze athari yenyewe ilisababiswa na nini kati ya sababu hizi tatu:

a) Tabia ya kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali
b) Sifa za kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali
c) Maumbile ya kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali


Hatimaye, washiriki walitakiwa waandike uamilifu ambao hutokana na matumizi ya methali zenye msamiati huo wa viumbe wa majini.

Kati ya methali 64 ambazo tumezishughulikia katika sura ya tatu, tumeteua methali ambazo zinarejelea viumbe wa majini bila kuwarudia. Lengo letu la kufanya hivi ni kuepuka hali ya kuwachosha washiriki kwa kuwa na hojaji ndefu. Kwa sababu hii basi, tuliweza kupata methali 32 ambazo tulizitumia katika hojaji yetu.

### 1. ALAYE KITU CHA MAMBA ASIFIKE MTONI


Kiumbe wa majini aliyetumika katika methali hii ni mamba. Washiriki 12 ambao ni asilimia 30 walichukulia kuwa methali hii ina athari chanya huku 28 ambayo ni asilimia 70 wakijaza kuwa na athari hasi.

a. **Athari kwa jamii kutokana na matumizi ya methali yenye kutumia msamiati wa mamba**




Katika kueleza chanzo cha athari yenyewe, washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya mamba ni washiriki 27 ambayo ni asilimia 67.5, sifa za mamba washiriki 12 ambao ni asilimia 30 huku maumbile ya mamba yakichaguliwa na mshiriki 1 ambao ni asilimia 2.5. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.


b. **Baa Grafuinatoa maelezo kuhusu visababishi vya athari katika methali zinazorejelea msamiati wa mamba.**



2. **ANAYETAKA KUFA NA ALA BUNJU, ATAZAMEREHEMA ZA MUNGU**

Katika methali hii, washiriki 10 ambao ni asilima 25 walionyesha kuwa na athari chanya wengine 30 ambao ni asilimia75 wakiwa na athari hasi kutokana na matumizi ya bunju.


Grafu ifuatayo inatoa maelezo haya




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya bunju ni washiriki11 ambao ni asilimia 27.5, sifa za bunju ni washiriki 27 ikiwa ni asilimia 67.5 huku maumbile ya bunju yakichaguliwa na washiriki 2 ambao ni asilimia 5. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.

**Visababishi vya athari.**



### 3. AVUMAYE BAHARINI PAPA KUMBE WENGINE WAPO


Katika methali hii papa ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa. Jedwali lifuatalo linaonyesha athari za msamiati wa neno hilo kwa washiriki waliotumika kujaza hojaji.




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya papa ni washiriki 7 ambao ni asilimia 17.5, sifa za pweza ni washiriki 28 ambao ni asilimia 70 huku maumbile ya papa yakichaguliwa na washiriki 5 ambao ni asilimia 12.5. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.

**visababishi vya athari yenyewe**





Katika grafu hii inaonekana kwamba wengi wa washiriki walichukulia sifa ya ukali wa papa kuwa ndiyo iliyowapelekea kuchagua athari chanya au hasi. Kutokana na athari za papa kwa

watumizi wa lugha ya Kiswahili, tunaona kwamba washiriki walilenga sifa za papa kuwa chanzo cha athari yao.


### 4. BINADAMU NI NGAMBA HAWAKOSI LA KUAMBA

Hii ni methali ambayo imemtumia ngamba. Washiriki 32 sawa na asilimia 80 walisema kuwa methali hii ina athari chanya huku wengine 8 sawa na asilimia 20 wakisema methali hii ina athari hasi. Katika kueleza athari, pai chati ifuatayo itafaa:




**Athari za neno ngamba katika methali**

Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya ngamba ni washiriki 11 ambao ni asilimia 27.5, sifa za ngamba ni washiriki 2 ambao ni asilimia 5 huku maumbile ya ngamba yakichaguliwa na washiriki 27 ambao ni asilimia 67.5. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.





**Visababishi vya athari**

Athari chanya kwa mujibu wa jamii unatokana na maumbile ya ngamba ambaye huwa na gamba ambalo binadamu hulitumia katika kutengeneza bidhaa mbalimbali.

### 5. CHAFI KANDANI MWAKO NI CHAFI- KIYENGE


Katika methali hii, kiumbe wa majini aliyeteuliwa na kutumiwa ni chafi.

Asilimia 22.5 ya washiriki waliona kuwa chafi ana athari chanya katika methali hii, hawa ni washiriki 9, huku washiriki 31 sawa na asilimia 77.5 wakiona kwamba chafi ni kiumbe ambaye analeta athari hasi katika methali hii. Hebu tutazame jedwali lifuatalo.




**Athari katika matumizi ya msamiati wa chafi katika methali hii**


Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa: tabia ya chafi ni washiriki 6 ambao ni asilimia 15, sifa za chafi ni washiriki 3 ambao ni asilimia 7.5 huku maumbile ya chafi yakichaguliwa na washiriki 31 ambao ni asilimia 77.5. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.




**Visababishi vya athari**


### 6. CHOKOCHOKO KAMCHOKOE PWEZA, BINADAMU HUTAMWEZA

Katika methali hii, pweza ndiye kiumbe wa majini aliyetumika. Athari zinazotokana na matumizi ya methali hii ambayo imetumia pweza ni; washiriki 11 ambayo ni sawa na asilimia 27.5 waliona kuwa methali hii ina athari chanya huku washiriki 29 ambayo ni sawa na asilimia 72.5 wakiona kuwa methali hii ina athari hasi kwa msikilizaji.




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya pweza ni washiriki 27 ambayo ni asilimia 67.5, sifa za pweza ni washiriki 7 ambayo ni asilimia 17.5 huku maumbile ya pweza yakichaguliwa na washiriki 6 ambayo ni asilimia 15. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.





**Visababishi vya athari**

## 7. CHOMBO CHA SAMAKI HAKIACHI KUNUKA VUMBA

Samaki ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Samaki ni neno la jumla ambalo linawarejelea viumbe wengi wa majini.


Athari zinazotokana na matumizi ya methali yenye kutumia msamiati huu wa samaki kwa mujibu wa washiriki waliojaza hojaji ni kama ifuatavyo: 22 sawa na asilimia 52.5 walisema kuwa matumizi ya msamiati huu yanaleta athari chanya huku washiriki 18 sawa na asilimia 47.5 wakiona kuwa matumizi ya methali yenye msamiati wa samaki yanaleta athari hasi.

Hebu tutazame pai chati ifuatayo:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Washiriki walisema visababishi vya athari zao kuwa; tabia ya samaki ni washiriki 5 ambayo ni asilimia 12.5, sifa za samaki ni washiriki 29 ambayo ni asilimia 72.5 huku maumbile ya samaki yakichaguliwa na washiriki 6 ambayo ni asilimia 15. Habari hii tumeiwasilisha katika baa grafu ifuatayo.




**Visababishi vya athari**


8. **CHURA AKITUPWA MAJINI HAFI**

Katika methali hii chura ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki waliojaza athari zinazotokana na matumizi ya methali hii kama ifuatavyo: washiriki 36 sawa na silimia 90 kuwa na athari chanya huku washiriki walioona methali hii kuwa na athari hasi ni 4 sawa na asilimia 10. Hebu tutazame pai chati ifuatayo:




**Athari zinazotokana na matumizi ya neno chura katika methali**


Washiriki waliojaza hojaji walionyesha kuwa athari zao zilitokana na: washiriki 7 ambao ni asilimia 17.5walisema athari yao ilitokana na tabia ya chura,washiriki 14 sawa na asilimia 35 walisema athari yao ilitokana na sifa za chura, huku washiriki 19 sawa na asilimia 47.5 wakisema athari yao ilitokana na maumbile ya chura. Hebu tutazame baa grafu ifuatayo.




**Visababishi vya athari**


## 9. DAGAA AMEMPONZA NDOBE

Dagaa na ndobe ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 21ambao ni sawa na asilimia 52.5 walisema kwamba msamiati wa viumbe hawa una athari chanya kwao huku washiriki 19 sawa na asilimia 47.5 wakijibu kuwa msamiati wa viumbe hawa una athari hasi. Hebu tutazame pai chati ifuatayo;




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Athari zenyewe zilitokana na tabia ya viumbe hawa. Hii ilipata asilimia 15 sawa na washiriki 6. Sifa za viumbe hawa ikapata asilimia 15, ambayo pia ni sawa na washiriki 6 nayo maumbile ya viumbe hawa ikapata asilimia 70 sawa na washiriki 28. Hebu tutazame baa grafu ifuatayo ili kuonyesha hali hii.





**Visababishi vya athari**

Maumbile ya viumbe hawa wawili ilichochea athari kwa wanajamii.

**10. DUNIA MWENDO WA NGISI**


Ngisi ndiye aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 12 sawa na asilimia 30 walisema kuwa methali hii ina athari chanya huku washiriki wengine 27 sawa na asilimia 70 wakaona kuwa methali hii ina athari hasi.

Hebu tutazame pai chati ifuatayo.




**Athari zinazotokana na matumizi ya ngisi katika methali.**


Athari kwa mujibu wa washiriki zilitokana na: tabia ya ngisi washiriki 8 sawa na 20%,sifa za ngisi washiriki 6 sawa na 15% nayo maumbile ya ngisi yakachaguliwa na washiriki 26 sawa na 65%, kama ilivyo katika hii baa grafu.




**Visababishi vya athari**


**11. EWE MTUJE, KWAMBA WALI TAFI UNGALIKUWAJE?**

Mtuje na tafi au chafi ndio viumbe wa majini walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 8 sawa na asilimia 20 walisema kuwa matumizi ya viumbe hawa yanaleta athari chanya huku washiriki wengine 32 sawa na asilimia 80 wakisema kuwa msamiati wenyewe unaleta athari hasi. Hebu tutazame pai chati ifuatayo:




**Athari zinazotokana na matumizi ya mtuje na tafi katika methali.**


Baa grafu ifuatayo inaonyesha visababishi vya athari. Washiriki 28 sawa na asilimia 70 wakisema athari inatokana na tabia ya viumbe hao, washiriki 10 sawa na asilimia 25 wakisema athari yenyewe inatokana na sifa za viumbe hao huku washiriki 2 sawa na asilimia 5 wakisema athari inatokana na maumbile ya viumbe hao.




**Visababishi vya athari**

**12. HASIRA ZA MKIZI TIJARA (FURAHA) YA MVUVI**


Katika methali hii, mkizi ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa. Washiriki 19 sawa na asilimia 47.5 walisema kuwa matumizi ya methali hii yanaleta athari chanya huku washiriki waliosema kuwa matumizi ya methali hii yanaleta athari hasi ni 21 sawa na asilimia 52.5. Hebu tutazame pai chati ifuatayo:




**Athari zinazotokana na matumizi ya mkizi katika methali.**

Visababishi vya athari kwa mujibu wa washiriki ni kama ifuatavyo: washiriki 31 sawa na asilimia 77.5 walisema ni tabia ya mkizi, washiriki 6 sawa na asilimia 15 wakasema ni sifa za mkizi huku washiriki 3 sawa na asilimia 7.5 wakisema ni maumbile ya mkizi.


Hebu tutazame baa grafu ifuatayo:




**Visababishi vya athari.**

**13. HUNA MSHIPI, HUNA NGWE KUOMOA TENGA NI NINI?**


Tenga ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumika katika methali hii. Washiriki 8 sawa na asilimia 20 walisema kuwa methali hii ina athari chanya huku washiriki 32 sawa na asilimia 80 wakisema kuwa methali hii ina athari hasi. Athari hizi ziko katika pai chati ifuatayo:




**Athari zinazotokana na matumizi ya methali zenye kutumia kiumbe tenga.**

Visababishi vya athari ni kama hivi vifuatavyo: Washiriki 7 sawa na 17.5 walisema athari inatokana na tabia ya tenga, washiriki 9 sawa na asilimia 22.5 wakasema athari inatokana na sifa za tenga nao washiriki 24 sawa na asilimia 60 walisema maumbile ya tenga.


Visabibishi vya athari ni kama vilivyo katika baa grafu ifuatayo:




**Visababishi vya athari.**


### 14. KAA AKIINUA GANDO MAMBO YAMEKATIKA

Kaa ndiye aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 20 sawa na asilimia 50 waliona kuwa msamiati katika methali hii unawaathiri kwa njia chanya huku wengine 20 sawa na asilimia 50 wakiona kuwa methali hii inawaathiri kwa njia hasi. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii.




**Athari zinazotokana na matumizi ya kaa katika methali.**


Kwa mujibu wa wanajamii waliojaza hojaji hiyo athari zao pamoja na idadi yao vinasababishwa na: washiriki 15 sawa na asilimia 37.5 walisema athari yenyewe inasababishwa na tabi ya kaa, washiriki 7 sawa na asilimia 17.5 walisema athari yao ilisababishwa na sifa za kaa huku washiriki 18 sawa na asilinmia 45 walisema athari yenyewe ilisabishwa na maumbile ya kaa. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii.




**Visababishi vya athari.**


**15. KAJIGEUZA CHACHANDU KUJIPALIA MAKAA**

Chachandu ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 3 sawa na asilimia 7.5 waliona kwamba chachandu huwaathiri kwa njia chanya huku washiriki 37 sawa na asilimia 92.5 wakasema kuwa chachandu ana athari hasi kwao katika hii methali. Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya athari:




**Athari zinazotokana na methali yenye kutumia chachandu**

Washiriki 26 sawa na asilimia 65 walisema kuwa athari yao ilitokana na tabia ya chachandu, ilhali washiriki 9 sawa na asilimia 22.5 wakasema kuwa athari yao ilitokana na sifa za chachandu, huku washiriki 5 sawa na asilimia 12.5 wakisema athari yao ilitokana na maumbile ya chachandu. Hebu tuingize habari hii katika jedwali lifuatalo.





**Visababishi vya athari**

**16. KAMBARE MKUNJE ANGALI MBICHI**


Katika methali hii, kambare ndiye kiumbe wa majini aliyeteuliwa na kutumiwa. Washiriki 32 sawa na asilimia 80 walisema kuwa methali yenye msamiati huu ina athari chanya huku washiriki 8 ambayo ni asilimia 20 wakisema kuwa methali yenye msamiati huu ni hasi.

Hali hii inaonyeshwa katika pai chati ifuatayo:




**Athari zitokanazo na matumizi ya kambare katika methali**


Washiriki 11 sawa na asilimia 27.5 walisema kuwa athari yao inasabaishwa na tabia ya kambare. Washiriki wengine 11 sawa na 27.5 walisema kuwa athari yao inasababishwa na sifa za kambare huku washiriki 18 sawa na asilimia 45 wakisema athari yao inatokana na maumbile ya kambare. Visabishi hivyo vya athari vinaonyeshwa katika baa grafu ifuatayo:




**Visababishi vya athari**

**17. KANGAJA SIMLE, MCHUZI KITOWEO**


Katika methali hii, kangaja ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 28 sawa na asilimia 70 walisema kuwa methali hii ina athari chanya kwao huku washiriki 12 sawa na asilimia 30 wakisema kuwa methali hii yenye kumtumia kangaja ina athari hasi kwao. Pai chati ifuatayo inaeleza hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki 5 sawa na asilimia 12.5 walisema athari yao inasabaishwa na tabia ya kangaja, washiriki 30 sawa na asilimia 75 walisema athari yao inasabishwa na sifa za kangaja huku washiriki 5 sawa na asilimia 12.5 wakisema kuwa maumbile ya kangaja, ndiyo sababu ya athari yao.

Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii.





**Visababishi vya athari**

Hivyo basi, sifa za kangaja ndizo hufanya jamii kuathiriwa kwa wingi. Sifa za kangaja tumezifafanua katika sura ya tatu.


### 18. KIBOKO ALIYEPASHA HABARI HAPASUI MTUMBWI

Kiboko ndiye kiumbe wa majini aliyeteuliwa na kutumiwa kwenye methali hii. Asilimia 82.5 yaani washiriki 33 walisema kuwa wanapata athari chanya kutokana na matumizi ya kiboko katika methali hii huku asilimia 17.5 ambao ni washiriki 7 wakisema wanapata athari hasi. Pai chati ifuatayo inafafanua hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Washiriki 22 sawa na asilimia 55 walisema kuwa athari yao inasabishwa na tabia za kiboko, washiriki 3 sawa na asilimia 7.5 wakisema athari yao inasabishwa na sifa za kiboko nao washiriki 15 sawa na asilimia 37.5 wakisema athari yao inasababishwa na maumbile ya kiboko. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii




**Visababishi vya athari**


## 19. KILICHOMPATA NGWENA NA KIBOKO NI HICHO

Ngwena na kiboko ndio viumbe wa majini walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 8 sawa na asilimia 20 waliona methali hii kuwa na athari chanya kwao, huku washiriki 32 sawa na asilimia 80 wakiona methali hii kuwa na athari hasi. Pai chati ifuatayo inaonyesha hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Washiriki 24 sawa na asilimia 60 walisema athari ilitokana na tabia ya viumbe hao wawili (ngwena na kiboko). Washiriki 8 sawa na asilimia 20 walisema athari yao ilitokana na sifa za ngwena na kiboko huku washiriki wengine 8 sawa na asilimia 20 wakisema athari yao ilitokana na maumbile ya ngwena na kiboko. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Visababishi vya athari**


## 20. KITATANGE HUTIA CHAFI LEMANI

Katika methali hii, Kitatange na chafi ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa. Asilimia 45 sawa na washiriki 18 walisema kuwa viumbe hawa wana athari chanya kwao, huku asilimia 55 sawa na washiriki 22 wakisema kuwa matumizi ya msamiati huu yanaleta athari hasi kwao. Hebu tutazame pai chati ifuatayo:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Katika kueleza visabishi vya athari, asilimia 72.5 walisema inatokana na tabia ya viumbe hao, asilimia 12.5 ya washiriki walisema kuwa athari yao inatokana na sifa za viumbe hao huku asilimia 15 wakisema kuwa athari yao inatokana na maumbile ya viumbe hao. Kazi hii inajitokeza katika baa grafu ifuatayo.





**Visababishi vya athari**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu athari hasi inatokana na tabia ya viumbe hawa kwa asilimia kubwa, chafi humfuata kitatange na mwishowe kujipata katika mtego (lema) yaani matatizo.


**21. KUMLA NGURU SI KAZI, KAZI KUMTOA MAGAMBA**

Katika methali hii inayomrejelea nguru, asilimia 52.5 sawa na washiriki 21 walisema kuwa methali zenyewe zinawapa athari chanya huku asilimia 47.5 ambayo ni washiriki 19 wakisema kuwa matumizi ya nguru yanaleta athari hasi kwao. Matokeo hayo yako katika pai chati ifuatayo:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Washiriki 4 sawa na asilimia 10 walisema  athari yao hutokana na tabia ya nguru, asilimia 10 ambao pia ni washiriki 4 walisema athari yao ilitokana na sifa za nguru nao washiriki 32 ambao ni asilimia 80 walisema kuwa athari yao ilitokana na maumbikle ya nguru. Hebu tutazame baa grafu ifuatao:




**Visababishi vya athari**


**22. KUVUA NUMBI SI KAZI, KAZI MAGAWIANI**

Katika methali hii asilimia 75 ambao ni washiriki 30 walisema kuwa methali hii ina athari chanya kwao, huku asilimia 25 sawa na washiriki 10 wakisema kuwa methali hii inawapa athari hasi, kama inavyobainika katika pai chati ifuatayo.




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Kutokana na matokeo haya wanajamii wengi wanaichukulia methali hii kuwa na athari chanya huku robo yao wakichukulia kuwa na athari hasi. Asilimia 10 ambao ni washiriki 4 walijibu kuwa athari yao ilisababishwa na tabia ya numbi,washiriki 10 sawa na asilimia 25 wakasema ni sifa za numbi hukuwashiriki 26 sawa na asilimia 65 wakijibu kuwa athari yao inatokana na maumbile ya numbi. Hebu tutazame baa grafu ifuatayo:





**Visababishi vya athari**

## 23. MBIO ZA KASA SI MBIO LAKINI HUMFIKISHA AENDAPO


Katika methali hii kasa, ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa. Katika methali hii asilimia 52.5 yaani washiriki 21 walijibu kuwa methali hii ina athari chanya kwao huku asilimia 47.5 yaani washiriki 19 wakisema ina athari hasi.

Pai chati ifuatayo inaeleza hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Asilimia 27.5 ambao ni washiriki 11 walijibu kuwa athari yao ilitokana na tabia ya kasa, asilimia 20 sawa na washiriki 8 wakisema kuwa athari yao ilitokana na sifa za kasa, hukuwashiriki 21 sawa na asilimia 52.5 wakisema athari yao ilitokana na maumbile ya kasa. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii.




**Visababishi vya athari**

**24. PONO MMOJA AKIOZA HUOZA NA SHAZILE**


Katika methali pono ndiye aliyeteuliwa na kutumiwa. Washiriki 15 sawa na asilimia 32.5 ya washiriki waliojaza hojaji walisema kuwa msamiati huu una athari chanya hukuwashiriki 25 sawa na asilimia 67.5 wakijaza kuwa na athari hasi kutokana na matumizi ya msamiati huu. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Asilimia 22.5 sawa na washiriki 9 walisema kuwa athari yao ilitokana na tabia ya pono, asilimia 30 ambao ni washiriki 12 walisema kuwa athari yao imesababishwa na sifa za pono hukuwashiriki 19 sawa na asilimia 47.5 ya washiriki wakisema kuwa athari yao ilisabishwa na maumbile ya pono.


Kutokana na matokeo haya inabainika wazi kuwa wanajamii wana chukulizi tofauti kutokana na msamiati uliotumika katika methali hii. Baa chati ifuatayo inaonyesha visababishi vya athari.




**Visababishi vya athari**


25. **PWEZA KAMWAMBIA NGISI, TUSIFANYE MAJILISI, MAJI YAKIPWA TUKISI**

Katika methali hii, pweza na ngisi ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa. Washiriki 30 sawa na asilimia 75 ya washiriki walisema kuwa methali hii ina athari chanya kwao, hukuwengine 10 sawa na asilimia 25 ya washiriki wakisema kuwa methali hii ina athari hasi kwao. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Asilimia 22.5 ambao ni washiriki 9 walisema kuwa athari yao ilitokana na tabia ya viumbe hao walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii, asilimia 27.5 sawa na washiriki 11 wakijibu kuwa athari yao inatokana na sifa za viumbe hawa, huku asilimia 50 ambao ni washiriki 20 wakisema kuwa athari yao ilitokana na maumbile ya viumbe hao wawili ambayo yanafanana kwa kiasi kikubwa. Baa grafu ifuatayo inaonyesha visababishi vya athari katika methali hii:





**Visababishi vya athari**

Matokeo haya yanaonyesha kuwa maumbile ya viumbe hawa wawili yamechangia kwa wingi athari ambazo wanajamii wanapata kutokana na matumizi ya methali hii.

### 26. SHUKA YA MASKINI NDIYO ITANDIWAYO DAGAA


Katika methali hii dagaa ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa. Asilimia 12.5 ambayo ni sawa na washiriki 5 walijaza kuwa methali hii ambayo imetumia msamiati huu inawapa athari chanya huku asilimia 87.5 ambao ni washiriki 35 wakisema kuwa methali hii inasababisha athari hasi kwao. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Tabia ya dagaa kwa mujibu wa washiriki 2 sawa na asilimia 5 huwasababishia athari, sifa za dagaa zinasababisha athari kwa asilimia 20 sawa na washiriki 8 huku maumbile ya dagaa yakiwasabishia washiriki 30 athari sawa na asilimia 75.


Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Visababishi vya athari**


## 27. TAA HAACHI MWIBAWE

Taa ndiye kiumbe wa majini aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Asilimia 60 sawa na washiriki 24 waliojaza hojaji walisema kuwa methali hii ina athari chanya kwao huku asilimia 40 ambao ni washiriki 16 wakisema kuwa matumizi ya methali hii yana athari hasi kwao. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Katika kueleza visababishi vya athari, asilimia 20 ambao ni washiriki 8 walisema kuwa athari yao inatokana na tabia ya taa, asilimia 20 wengine ambao ni washiriki 8pia wakisema athari yao inatokana na sifa za taa, ilhali washiriki 24 sawa na 60% wakisema athari yao ilisababishwa na maumbile ya taa. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii:





**Visababishi vya athari**

Kutokana na matokeo haya, tunaona kuwa asilimia ishirini ya wanajamii wanaathiriwa na tabia na sifa za taa mtawalia huku idadi kubwa ya wanajamii ambayo ni asilimia sitini wakiathiriwa na maumbile ya taa.

### 28. UKIKAA NA SIMBA, VAA NGOZI YA MAMBA


Simba na mamba ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Washiriki 22 sawa na asilimia 55 ya washiriki walijaza kuwa matumizi ya methali yenye kutumia msamiati huu ina athari chanya kwao huku asilimiia 45 sawa na washiriki 18 wakisema kuwa methali yenye kutumia msamiati huu ina athari hasi kwao.

Pai chati ifuatayo inaonyesha athari za methali yenye kutumia msamiati huu kwa jamii




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki 10 sawa na asilimia 25 ya washiriki walisema kuwa athari yao ilisababishwa na tabia za viumbe hawa, asilimia 60 ambao ni washiriki 24 wakisema kuwa athari yao imesababishwa na sifa za simba na mamba hukuwashiriki 6 sawa na asilimia 15 ya jumla ya washiriki wakisema kuwa athari yao ilisababiswa na maumbile ya simba na mamba. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii.





**Visababishi vya athari**

Kutokana na matokeo haya ni wazi kuwa wanajamii wengi wanaelewa kuhusu sifa za simba na mamba za kutunukiwa uongozi wa nchi kavu na majini mtawalia. Tabia za simba na mamba kuwa wao ni hatari na ulaji wao wa nyama inafuatana hatimaye na maumbile ya simba na mamba ambayo hutisha.


**29. UMEKUWA NGUVA HUHIMILI KISHINDO**

Nguva ndiye kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Asilimia 17.5 ambayo ni washiriki 7 ya waliojaza hojaji walisema kuwa msamiati katika methali hii unawapa athari chanya huku washiriki 33 sawa na asilimia 87.5 wakijaza kuwa msamiati uliotumika una athari hasi kwao. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Asilimia 25 sawa na washiriki 10 walisema kuwa athari yao ilisababishwa na tabia ya nguva, na washiriki 11 sawa na asilimia 27.5 nao walijibu kuwa athari yao ilitokana na sifa za nguva, huku asilimia 47.5 ambao ni washiriki 19 wakisema kuwa athari yao ilisababishwa na maumbile ya nguva. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii .




**Visababishi vya athari**


### 30. UMEONA WAPI MNANDI KUJENGA NYUMBA MACHWEONI

Mnandi ndiye ndege aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali hii. Kwa mujibu wa washiriki 12 sawa na asilimia 30 walipata athari chanya kutokana na matumizi ya msamiati uliotumika katika methali hii, huku washiriki 28 sawa na asilimia 70 wakipata athari hasi. Hebu tutazame hali hii katika pai chati ifuatayo:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**


Asilimia 77.5 ambao ni washiriki 31 walijibu kuwa athari yao ilitokana na tabia ya mnandi, asilimai 7.5 ambao ni washiriki 3 wakasema kuwa athari yao ilisababishwa na sifa za mnandi huku asilimia 15 yaani washiriki 6 wakijibu kuwa athari yao ilitokana na maumbile ya mnandi. Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Visababishi vya athari**

### 31. USIKU KIZA MANGAZIMBWE MTUMBUU HUWA PAPA


Katika methali hii mtumbuu na papa ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa. Katika utafiti wetu washiriki 9 sawa na asilimia 22.5 ya washiriki walikuwa na athari chanya kutokana na matumizi ya viumbe hawa katika methali hii huku asilimia 77.5 yaani washiriki 31 wakiwa na athari hasi kutokana na matumizi ya viumbe hawa katika hii methali. Pai chati ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki 15 sawa na asilimia 37.5 walisema kuwa athari yao ilitokana na tabia za viumbe hawa . washiriki 7 sawa na asilimia 17.5 wakasema athari yao ilitokana na sifa za viumbe hawa huku washiriki wengine 18 sawa na asilimia 45 wakisema kuwa athari yao ilitokana na maumbile ya viumbe hawa.


Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii.




**Visababishi vya athari**

**32. ZOBE NA MSUWELE WOTE NI WAMOJA**

Katika methali hii ambayo zobe na msuwele ndio viumbe walioteuliwa na kutumiwa, washiriki 28 sawa na asilimia 70 walisema kuwa methali hii inawapa athari chanya huku wengine 12 sawa na asilimia 30 wakisema kuwa methali hii inawapa athari hasi. Pai chati ifuatayo inaeleza hali hii:





**Athari katika matumizi ya msamiati katika methali hii**

Washiriki 8 sawa na asilimia 20 walijibu kuwa athari yao ilitokana na tabia za zobe na msuwele, washiriki wengine 5 sawa na asilimia 12.5 wakisema athari yao ilitokana na sifa za zobe na

msuwele huku wengine 28 sawa na asilimia 70 wakisema kuwa athari yao ilitokana na maumbile ya zobe na msuwele.

Baa grafu ifuatayo inaonyesha hali hii:




**Visababishi vya athari**

Kutokana na matokeo haya katika methali hii athari kwa jamii kwa kiwangokikubwa husababishwa na maumbile ya viumbe hawa.

## 4.5 UAMILIFU WA METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI


Katika sehemu hii tutaangazia uamilifu wa methali zinazorejelea viumbe wa majini ili kutekeleza majukumu fulani mahsusi katika jamii. Uamilifu wa methali hizi tuliupata kutoka kwa matokeo ya hojaji, ambayo ilishirikisha walimu na wafanyakazi wa shule za msingi na upili za Naikaraa, tarafa ya Masai Mara katika kaunti ya Narok. Methali 32 zilitumika kwenye hojaji kisha matokeo yake kuchanganuliwa katika majedwali.

### 4.5.1 KURAHISISHA MAWASILIANO

Washiriki walisema kuwa methali huweza kutumiwa ili kurahisisha mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake, au mwandishi na msomaji wake. Kwa mujibu wa washiriki, methali 16 zina uamilifu wa kurahisisha mawasiliano. Methali hizo ni asilimia 50 ya jumla ya methali zilizotumika katika utafiti. Jedwali lifuatalo linaonyesha methali hizo pamoja na idadi ya washiriki ambao walijaza kuwa methali hizo zina uamilifu wa kurahisisha mawasiliano.

| **Methali zenye uamilifu huu wa kurahisisha mawasiliano** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 1 |
| 2. Chura akitupwa majini hafi. | 2 |
| 3. Dunia mwendo wa ngisi. | 2 |
| 4. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 1 |
| 5. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 1 |
| 6. Kambare mkunje angali mbichi. | 2 |
| 7. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 1 |
| 8. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho | 2 |
| 9. Kitatange hutia chichi lemani. | 1 |
| 10. Kumla nguru si kazi, kazi kumtoa magamba. | 1 |
| 11. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni | 3 |
| 12. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo | 2 |
| 13. Taa haachi mwibawe | 2 |
| 14. Umekuwa nguva huhimili kishindo | 1 |
| 15. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani | 1 |
| 16. Zobe na msuwele ni wamoja | 5 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **16** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kurahisisha mawasiliano kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**


### 4.5.2 KUBADILI MADA

Kati ya methali 32, washiriki walichagua methali 24 ambazo ni sawa na silimia 75% kuwa zina uamilifu wa kubadili mada katika mazungumzo. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo:

| **Methali zenye uamilifu huu wa kubadili mada** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 1 |
| 2. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 2 |
| 3. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 2 |
| 4. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 1 |
| 5. Chura akitupwa majini hafi. | 5 |
| 6. Dunia mwendo wa ngisi. | 2 |
| 7. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 2 |
| 8. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 8 |

| | |
|---|---|
| 9. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 5 |
| 10. Kambare mkunje angali mbichi. | 1 |
| 11. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 1 |
| 12. Kitatange hutia chafi lemani. | 3 |
| 13. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 1 |
| 14. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 1 |
| 15. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 1 |
| 16. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 2 |
| 17. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 2 |
| 18. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 3 |
| 19. Taa haachi mwibawe. | 2 |
| 20. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 1 |
| 21. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 2 |
| 22. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 3 |
| 23. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | 1 |
| 24. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 4 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **24** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kubadili mada kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**


### 4.5.3 KUTENGA KUNDI FULANI KATIKA MAWASILIANO

Methali 14 ambazo ni sawa na asilimia 43.8 ya jumla ya methali katika hojaji zina uamilifu wa kutenga kundi fulani katika mazungumzo. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo.

| **Methali zenye uamilifu huu wa kutenga kundi fulani katika mawasiliano** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 1 |
| 2. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 7 |
| 3. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 1 |
| 4. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 1 |
| 5. Kangaja simle,mchuzi kitoweo. | 2 |
| 6. Kitatange hutia chafi lemani. | 3 |
| 7. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 1 |
| 8. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 1 |

| | |
|---|---|
| 9. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 1 |
| 10. Pweza kamwambia ngisi, 'tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi' | 1 |
| 11. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 9 |
| 12. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 1 |
| 13. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 1 |
| 14. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 2 |
| **15. Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **14** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kutenga kundi kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**

### 4.5.4 KUONYA


Kwa mujibu wa washiriki waliojaza hojaji, methali 31 sawa na asilimia 96.9 zinaouamilifu wa kuonya. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo.

| Methali zenye uamilifu huu wa kuonya | Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 27 |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | 12 |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 9 |

| | |
|---|---|
| 4. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 3 |
| 5. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 25 |
| 6. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 2 |
| 7. Chura akitupwa majini hafi. | 3 |
| 8. Dunia mwendo wa ngisi. | 12 |
| 9. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 10 |
| 10. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 10 |
| 11. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 6 |
| 12. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 12 |
| 13. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 6 |
| 14. Kambare mkunje angali mbichi. | 7 |
| 15. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 5 |
| 16. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 10 |
| 17. Kitatange hutia chafi lemani. | 9 |
| 18. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 7 |
| 19. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 2 |
| 20. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 2 |
| 21. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 1 |
| 22. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 8 |
| 23. Pweza kamwambia ngisi, ‘tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi’ | 3 |
| 24. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 4 |
| 25. Taa haachi mwibawe. | 1 |
| 26. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 15 |
| 27. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 6 |

| | |
|---|---|
| 28. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 5 |
| 29. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | 7 |
| 30. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 5 |
| 31. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 2 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **31** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kuonya kwa mujibu wa wanajamii.





**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**

### 4.5.5 KUBURUDISHA NA KUPUMBAZA

Washiriki pia walijibu kuwa methali hutumika ili kuburudisha na kupumbaza, ambapo methali 4 sawa na asilimia 12.5 ziliteuliwa na washiriki hao kuwa zina uamilifu wa kuburudisha na kupumbaza. Methali hizo ziko katika jewali lifuatalo:

| | |
|---|---|
| 1. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 5 |
| 2. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 8 |
| 3. Pweza kamwambia ngisi, 'tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi' | 24 |
| 4. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba | 10 |
| **5. Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **4** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kuburudisha na kupumbaza kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**


### 4.5.6 KUFUNZA NA KUASA

Washiriki walitaja methali zote 32 sawa na asilimia 100 kuwa zina uamilifu wa kufunza. Jedwali lifuatalo linaonyesha methali hizo:

| Methali zenye uamilifu huu kufunza na kuasa | Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 1 |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | 4 |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 14 |
| 4. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 14 |
| 5. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 7 |
| 6. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 2 |
| 7. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 15 |
| 8. Chura akitupwa majini hafi. | 8 |
| 9. Dunia mwendo wa ngisi. | 10 |
| 10. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 8 |
| 11. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 8 |
| 12. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 7 |
| 13. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 8 |
| 14. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 5 |
| 15. Kambare mkunje angali mbichi. | 17 |
| 16. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 12 |
| 17. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 11 |
| 18. Kitatange hutia chafi lemani. | 6 |
| 19. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 18 |
| 20. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 11 |
| 21. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 6 |
| 22. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 13 |

| | |
|---|---|
| 23. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 12 |
| 24. Pweza kamwambia ngisi, 'tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi' | 8 |
| 25. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 10 |
| 26. Taa haachi mwibawe. | 9 |
| 27. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 10 |
| 28. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 5 |
| 29. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 6 |
| 30. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | 16 |
| 31. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 10 |
| 32. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 8 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **32** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kufunza na kuasa kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**


### 4.5.7 KUTIA MOYO

Methali hutumiwa na wanajamii kwa lengo la kumtia mtu moyo. Methali 27 sawa na asilimia 84.4 za methali kwenye hojaji zina uamilifu wa jukumu la kutia moyo. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo:

| **Methali zenye uamilifu huu kutia moyo** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 1 |
| 2. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 4 |
| 3. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 7 |
| 4. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 7 |
| 5. Chombo cha samaki hakiachi kununuka vumba. | 6 |
| 6. Chura akitupwa majini hafi. | 10 |
| 7. Dunia mwendo wa ngisi. | 2 |
| 8. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 2 |
| 9. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 7 |
| 10. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 2 |
| 11. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 4 |
| 12. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 3 |
| 13. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 6 |
| 14. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 1 |
| 15. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 5 |
| 16. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 8 |
| 17. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 16 |
| 18. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 4 |
| 19. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 4 |

| | |
|---|---|
| 20. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 9 |
| 21. Taa haachi mwibawe. | 11 |
| 22. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 1 |
| 23. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 3 |
| 24. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 2 |
| 25. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | 4 |
| 26. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 2 |
| 27. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 20 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **27** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kutia moyo kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**


### 4.5.8 KUKASHIFU

Methali 24 sawa na asilimia 75 ya jumla ya methali katika hojaji zina uamilifu wa kukashifu inapotumika katika mawasiliano. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo.

| **Methali zenye uamilifu huu wa kukashifu** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 4 |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | 1 |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 3 |
| 4. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 1 |
| 5. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 12 |
| 6. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 1 |
| 7. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 11 |
| 8. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 5 |
| 9. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 3 |
| 10. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 1 |
| 11. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 3 |
| 12. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 7 |
| 13. Kitatange hutia chafi lemani. | 3 |
| 14. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 2 |
| 15. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 2 |
| 16. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 1 |
| 17. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 2 |
| 18. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 2 |
| 19. Pweza kamwambia ngisi, ‘tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi’ | 2 |
| 20. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 1 |
| 21. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 1 |

| | |
|---|---|
| 22. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 12 |
| 23. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 14 |
| 24. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 5 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **24** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kukashifu kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**

### 4.5.9 KUTAHADHARISHA


Methali hutumiwa na wanajamii kwa lengo la kutahadharisha. Methali 29 sawa na asilimia 90.6 za methali kwenye hojaji zina uamilifu wa jukumu la kutahadharisha. Methali hizo ziko katika jedwali lifuatalo:

| Methali zenye uamilifu huu wa kutahadharisha | Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 1 |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | 15 |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 7 |
| 4. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 2 |

| | |
|---|---|
| 5. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 6 |
| 6. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 1 |
| 7. Chura akitupwa majini hafi. | 4 |
| 8. Dunia mwendo wa ngisi. | 9 |
| 9. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 2 |
| 10. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 3 |
| 11. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 7 |
| 12. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 3 |
| 13. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 10 |
| 14. Kambare mkunje angali mbichi. | 2 |
| 15. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 2 |
| 16. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 5 |
| 17. Kitatange hutia chafi lemani. | 10 |
| 18. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 1 |
| 19. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 5 |
| 20. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 4 |
| 21. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 1 |
| 22. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 3 |
| 23. Taa haachi mwibawe. | 7 |
| 24. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 7 |
| 25. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 5 |
| 26. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 1 |
| 27. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa | 5 |

| | |
|---|---|
| papa. | |
| 28. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 2 |
| 29. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 1 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **29** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kutahadharisha kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**

### 4.5.10 KUSHAURI


Methali 32 sawa na asilimia 100 katika hojaji yetu zina uamilifu wa kushauri kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo.

| **Methali zenye uamilifu huu wa kushauri** | **Idadi ya washiriki waliojaza uamilifu huu wa methali** |
|---|---|
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | 5 |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | 9 |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | 2 |
| 4. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | 5 |

| | |
|---|---|
| 5. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | 9 |
| 6. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | 7 |
| 7. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba. | 12 |
| 8. Chura akitupwa majini hafi. | 6 |
| 9. Dunia mwendo wa ngisi. | 4 |
| 10. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | 5 |
| 11. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | 4 |
| 12. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | 5 |
| 13. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | 9 |
| 14. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | 6 |
| 15. Kambare mkunje angali mbichi. | 8 |
| 16. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | 9 |
| 17. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | 4 |
| 18. Kitatange hutia chafi lemani. | 5 |
| 19. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | 5 |
| 20. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | 7 |
| 21. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | 10 |
| 22. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo. | 12 |
| 23. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | 7 |
| 24. Pweza kamwambia ngisi, ‘tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi’ | 5 |
| 25. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | 2 |
| 26. Taa haachi mwibawe. | 7 |
| 27. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | 4 |

| | |
|---|---|
| 28. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | 4 |
| 29. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | 7 |
| 30. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | 4 |
| 31. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani. | 8 |
| 32. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | 2 |
| **Jumla ya methali zilizo na uamilifu huu** | **32** |

Pai chati ifuatayo inaonyesha asilimia ya methali ambazo zina uamilifu wa kushauri kwa mujibu wa wanajamii.




**Asilimia ya methali zenye jukumu hili**

## 4.6 HITIMISHO

Katika sura hii ya nne tumeangazia athari kwa jamii pamoja na uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii. Tumeanza kwa kuangazia athari kwa jamii ambapo methali zenye kutumia msamiati wa viumbe wa majini hutumika. Katika uchanganuzi wetu wa data tumebaini kuwa methali zenye kutumia msamiati wa viumbe wa majini una athari chanya au hasi kwa mwanajamii kutegememea mazingira aliyomo.

Katika sehemu ya pili ya sura hii, tumeangazia uamilifu wa methali husika katika jamii, ambapo tumeeleza uamilifu wa methali pamoja na kuorodhesha methali zinazoleta uamilifu huo kwa mujibu wa wanajamii walioshiriki katika kujaza wa hojaji. Katika sehemu hii, tumebaini ya kwamba methali yoyote ile ina uamilifu wa majukumu mengi katika jamii, kutegemea mazingira ya msikilizaji.

Kutokana na athari pamoja na uamilifu wa majukumu tofautitofauti kwa wanajamii katika methali zenye kutumia msamiati ule ule, inabainika wazi hapa kuwa msikilizaji ni muhimu sana katika mchakato wa mawasiliano kwa kuwa athari pamoja na uamilifu wa majukumu unaoana barabara na dhana za utambuzi, mawasiliano na uelewa katika nadharia ya mahusiano.

Data yetu katika sura hii tumeiwasilisha kwa njia ya ufafanuzi, majedwali na takwimu kwa kutumia pai chati na baa grafu.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO, CHANGAMOTO ZA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

### 5.0 UTANGULIZI

Hii ndiyo sura ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu. Katika sura hii tumenuia kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Nadharia tete zetu tumezibainisha kama zimeoana na matokeo ya utafiti wetu au la. Hatimaye tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa siku za usoni.

### 5.1 MUHTASARI

Sura ya kwanza imehusu utangulizi wa utafiti wetu. Katika sura hiyo, tumezungumzia usuli wa mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, msingi wa nadharia, pamoja na upeo na mipaka ya utafiti wetu. Hali kadhalika tumeangazia yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu ya utafiti pamoja na mbinu za utafiti ambazo tumetumia.

Katika sura ya pili tumeeleza dhana muhimu katika utafiti wetu. Tumetoa maelezo kuhusu dhana za 'isimujamii' na 'jamii' na pia methali kwa jumla, kisha tukajikita katika methali za Kiswahili ili kujenga msingi wa utafiti wetu. Hatimaye tumetoa maelezo kuhusu lugha ya Kiswahili na nafasi yake katika taifa la Kenya. Kwa kufanya hivi, tumeonyesha pia nafasi ya methali za Kiswahili, kipengele ambacho ni sehemu ya lugha ya Kiswahili.

Katika sura ya tatu tumefafanua methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tumeangazia msamiati uliotumika katika uundaji wa methali husika, huku tukiangazia sifa, tabia namaumbile ya viumbe walioteuliwa na kutumiwa katika methali husika. Kwa kuangazia sifa, tabia na maumbile ya viumbe hao, tumejaribu kuonyesha uhusiano wa mazingira na viumbe hao, na mchango yao katika ufanisi wa methali hizo. Tumebaini kuwa viumbe wa majini walioteuliwa na kutumiwa katika methali mahsusi hawakuteuliwa tu, bali tabia, sifa na maumbile ya viumbe hao yalitiliwa maanani kabla na wakati wa kuteuliwa na kutumiwa katika methali hizo husika.

Katika sura ya nne tumeangazia athari kwa jamii pamoja na uamilifu wa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini katika jamii. Tumeanza kwa kuangazia athari kwa jamii ambapo methali zinazotumia msamiati wa viumbe wa majini hutumika. Katika uchanganuzi wetu wa data

tumebaini kuwa methali zenye kutumia msamiati wa viumbe wa majini una athari chanya au hasi kwa mwanajamii kutegememea mazingira aliyomo.

Katika sehemu ya pili ya sura ya nne, tumeangazia uamilifu wa methali husika katika jamii, ambapo tumeeleza uamilifu wa methali pamoja na kuorodhesha methali zinazoleta uamilifu huo kwa mujibu wa wanajamii walioshiriki katika kujaza hojaji. Katika sehemu hii, tumebaini ya kwamba methali yoyote ile ina uamilifu wa majukumu mengi katika jamii, kutegemea mazingira ya msikilizaji.

Kutokana na athari pamoja na uamilifu wa majukumu tofautitofauti kwa wanajamii katika methali zenye kutumia msamiati ule ule, tumebaini wazi hapa kuwa msikilizaji ni muhimu sana katika mchakato wa mawasiliano, kwa kuwa athari pamoja na uamilifu wa majukumu unaoana barabara na dhana za utambuzi, mawasiliano na uelewa katika nadharia ya mahusiano.

**5.2 HITIMISHO**

Katika utafiti wetu, tumekuwa na nadharia tete tatu ambazo tulizitambua. Nadharia tete yetu ya kwanza ilidai kuwa kunao viumbe wenye tabia,sifa na maumbile mahsusi ambao kwa mujibu wa wanajamii hutumika katika methali za Kiswahili, na kwamba tabia,sifa na maumbileya viumbe hao zinafaa kwa matumizi ya methali mahsusi katika jamii ya Waswahili.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa viumbe wenye tabia,sifa na maumbilemahsusi kwa mujibu wa wanajamii hutumika katika methali za Kiswahili na kwambatabia,sifa na maumbile ya viumbe hao zinafaa kwa matumizi ya methali mahsusi katika jamii ya Waswahili. Hivyo basi, nadharia tete hii ni ya kweli.

Nadharia tete yetu ya pili ni ile iliyodai kuwa athari zinazotokana na matumizi ya msamiati wa Kiswahili unaohusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini zinaonekana.Uchanganuzi wetu umeonyesha kuwa matumizi ya msamiati wa Kiswahili unaohusu methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini una athari kwa wanajamii, athari

zenyewe zikiwa chanya au hasi  na husababishwa na kutumiwa katika methali hizo husika. Nadharia tete hii ni ya kweli vilevile.

Katika nadharia tete yetu ya tatu ambapo tulisema kuwa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini huwa na uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu fulani katika mazingira mahsusi. Matokeo ya uchanganuzi wetu ni kuwa methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini huwa na uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu fulani katika mazingira mahsusi; hivyo basi nadharia tete hii ni ya kweli.

## 5.3 CHANGAMOTO ZA UTAFITI

Katika utafiti wetu tulikumbana na changamoto kadhaa. Baadhi ya washiriki tulionuia kuwapa hojaji kujaza walikataa. Sababu waliyoitoa ni kuwa lugha ya Kiswahili hawaifahamu vizuri.

Baadhi ya washiriki tuliowapa hojaji kutujazia hawakuturejeshea, na tulipowauliza wengine walisema hawakuzijaza huku wengine wakituambia kuwa hawakujua walikoziweka. Wengine walijaza hojaji sehemu fulani na sehemu nyingine waliziacha wazi. Hii ilitulazimu tuchanganue data tuliyoipata kutoka kwa washiriki waliojaza hojaji kikamilifu.

## 5.4 MAPENDEKEZO

Katika utafiti wetu, tulibanwa na upeo na mipaka yetu kwa kuwa taalamu ya methali ni pana na ina mambo mengi ya kutafitiwa katika ujumla wake. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa methali zina uamilifu wa majukumu pamoja na athari kwa wanajamii. Mapendekezo yetu ni kama yafuatayo:-

Katika utafiti wetu tulijikita katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tungependekea watafiti wachunguze methali katika makundi mengine ya methali ili kupata uelewa wa kina kuhusiana na athari na uamilifu wa methali hizo katika jamii.

Katika utafiti wetu wa kule nyanjani, tulitumia mbinu ya hojaji. Hojaji ilituwezesha kupata data tuliyoihitaji kutoka kwa kundi moja la jamii, wale wanaofahamu kusoma na kuandika. Hivyo basi hatukupata data kutoka kwa wanajamii ambao hawafahamu kusoma na kuandika.

Tungependekeza utafiti ambao matumizi ya mbinu ya mahojiano itatumika ili kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wanajami wote kwa jumla.

Utafiti wetu ulijikita katika kipengele cha methali peke yake. Hata hivyo pana uhusiano na mwingiliano mkubwa kati ya methali na vipengele vingine vya fasihi simulizi kama vile vitendawili. Tungependekeza watafiti wa baadaye wazamie eneo hili ili kuonyesha kufanana na kutofautiana kwa athari zinazotokana na mwingiliano wa vipengele hivyo viwili.

Utafiti wetu ulijikita katika methali za Kiswahili peke yake. Tungependekeza wasomi wa baadaye walinganishe methali za Kiswahili na methali za lugha nyingine za Kiafrika kwa kuangazia suala la mazingira katika  uteuzi wa msamiati uliotumika katika methali za jamii hizo, kufanana na kutofautiana kwa msamiati huo pamoja na athari kwa jamii zinazotokana na matumizi ya methali zenye msamiati huo kiuamilifu.

# MAREJELEO:


Abudu, M. (1974) *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi*. California: Foundation Books.

Andambi, A. na Murono, E. (2005) *Muundo Mpya wa Methali za kiswahili.* Nairobi: MvuleAfrica Publishers.

Arege, T. na Nyanje, M. (2011) *Kamusi Fafanuzi ya Methali. Nairobi:* Target Publications Limited.

Binyanya, M. R. (2014) Sajili ya Maafisa wa Polisi: Tathmini ya MatumiziYa Lugha ya Kiswahilikatika kituo cha Polisi cha Central, Nairobi.Tasnifu ya Uzamili (M.A.)ambayo haijachapishwa, ChuoKikuu chaNairobi.

Blakemore, S. (1987) *Semantic Constraints on Relevance.* Oxford: Blackwell.

Blass, R (2007a) *"Manipulation in the Speeches of Writings of Hitler and NSDAD."* Seminar notes presented at Nairobi Evangelical Graduate School of Theology and SIL Africa Area. Nairobi.

Cambridge *(2003) Adavanced Learners Dictionary*. Cambridge: Cambridge University Press

Finnegan, R. (1983) *Oral Literature in Africa.* Oxford: Open Book Publishers.

Giles, H. (1987) *Speech Style and Social Evaluation. London:* Academic Press INC

Grice, P. (1975) [In: *Syntax and Semantics*, Vol. 3, Speech Acts, ed. by Peter Cole and Jerry L. *Morgan*.] New York: Academic Press. Available at: https//www.amazon.com/Syntax-Semantics

Habwe, J. na wengine (2010) *Darubini ya Isimujamii.* Nairobi: Phoenix Publishers

Iribemwangi, P.I. na Mukhwana A. (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers

Joon, Y.C. (1992)Methali Kama Falsafa ya Maisha; uhakiki linganishi wa methali za Kikorea na za Kiswahili, Tasnifu ya Uzamili (M.A.) ambayo haijachapishwa, ChuoKikuu cha Nairobi.

Karama, S. na Saidi, S. (1983) *Maelezo ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: Sasa Sema Publishers.

King'ei K. (1982)Uhakiki wa "Nthimo"(methali) za Kikamba, kwa Kufuatisha Misingi ya Methali za Kiswahili,Tasnifu ya Uzamili (M.A)ambayo haijachapishwa, ChuoKikuu cha Nairobi.

------------- na Ndalu, A. E. (1989) *Kamusi ya Methali za kiswahili.*Nairobi: East African Publishers

Kipury, N. (1983) *Oral Literature of the Maasai.* Nairobi: Heinmann Educational Books (E.A) Limited.

Mang'eni, L. (2008) An Analysis of Political Language in Kenya: A Pragmatic Analysis of the Use of "Change" and "Majimbo" as Concept During the 2007 General Elections. Tasnifu ya Uzamili (M.A.) ambayo haijachapishwa, ChuoKikuu cha Nairobi.

Mekacha, D. K.(2011) *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili.* Dar es salaam: Osaka University of Foreign Studies

Mlacha, S. (1995) *Dhima ya Methali Katika Malezi.* Dar-es-Salaam: TUKI

Oxford (2005) *Oxford Dictionary.* Oxford: Oxford University Press.

Mugenda, O. na Mugenda, (2003) *Reseach Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: ACTS Press.

Mukhwana, A. (1990) Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili Kenya. Tasnifu ya Uzamili (M.A.) ambayo haijachapishwa, ChuoKikuu cha Nairobi.

Sankan, S. S. (1971) *The Maasai.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Scheven, A. (1981) *Swahili Proverbs.* Washington: University Press of America, INC

Sperber D. na Wilson,D. (1995) *Relevance Theory.* Oxford: Blackwell.

Sperber D. na Wilson,D. (2004)*Relevance Theoryin the Handbook of Pragmatics*. Horn R. & Ward Gregory. Oxford: Blackwell.

TUKI (2001) *Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza.* Dar-es-Salaam: TUKI.

------- (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar-es-Salaam: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2001)*Kamusi ya Methali.*Series: *Lulu za Lugha 2*Nairobi: Longman

Whiteley, W.H (1974) *Language in Kenya*. Nairobi Oxford University Press

Wilson, D. (2003)“Relevance and Lexical Pragmatics”*[in Italian Journal of Linguistics/ Rivista di Linguistica15.2: 273-291(2003)*, SpecialIssue on Pragmatics and the Lexicon].

https//www.researchgate.net/...Wilson/.../0046352456ecac3cb2000000.pdf

## KIAMBATISHO "A"

## HOJAJI

Jina langu ni Paul Sito. Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, idara ya Kiswahili. Nafanya utafiti kuhusu athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati. Ili kuweza kufanikisha lengo langu hili la utafiti, nakusihi unijazie hojaji hii. Habari itakayopatikana kutoka kwa hojaji hii inakusudiwa kutumiwa katika utafiti huu peke yake na daima itabakia kuwa siri.

SEHEMU YA A.

Jina :………………………………………………………………. (Si lazima)

Tumia alama √ katika jibu lako.

Umri: miaka (20-25) miaka (26-30)

miaka (31-35) miaka (36-40)

miaka (41-45) miaka (45-50)

miaka (51 na zaidi)

Kituo chako cha kufanyia kazi:

A. Shule ya msingi [ ]

B. Shule ya upili [ ]

SEHEMU YA B.

1. Je, kwa maoni yako mazingira huathiri uteuzi wa msamiati?

A. ndio [ ]

B. la [ ]

2. Msamiati unaoteuliwa na kutumiwa katika mazingira mahsusi hukusudiwa kuwa na athari gani kwa mwanajamii au wanajamii?

A. Athari chanya [ ]

B. Athari hasi [ ]

C. Athari chanya au hasi [ ]

SEHEMU YA C.

Ili kuweza kurejelea mazingira na athari zake katika uteuzi wa msamiati, tujikite katika methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Methali zenyewe zinapotumiwa katika jamii, hukusudiwa kuwa na uamilifu fulani. Ili kufanikisha lengo hili tutazingatia :

a. tabia ya kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali husika.

b. sifa za kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali husika.

c. maumbile ya kiumbe aliyeteuliwa na kutumiwa katika methali husika.

Katika jedwali lifuatalo, jaza nafasi zilizoachwa kama inavyostahili kwa kufuata maagizo.

| **Methali** | **Athari (tumia alama ya √ katika jibu lako)** | | **Athari yenyewe husababishwa na nini? Chagua kutoka: a, b, au c hapo juu.** | **Uamilifu wa methali husika katika jamii ni upi?** |
|---|---|---|---|---|
| | **chanya** | **hasi** | | |
| 1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni. | | | | |
| 2. Anayetaka kufa na ale bunju. | | | | |
| 3. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo. | | | | |
| 4. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba. | | | | |
| 5. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge. | | | | |
| 6. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza. | | | | |
| 7. Chombo cha samaki hakiachi kununka vumba. | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. Chura akitupwa majini hafi. | | | | |
| 9. Dagaa amemponza ndobe | | | | |
| 10. Dunia mwendo wa ngisi. | | | | |
| 11. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje? | | | | |
| 12. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi. | | | | |
| 13. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini? | | | | |
| 14. Kaa akiinua gando mambo yamekatika. | | | | |
| 15. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa. | | | | |
| 16. Kambare mkunje angali mbichi. | | | | |
| 17. Kangaja simle, mchuzi kitoweo. | | | | |
| 18. Kiboko aliyepasha habari hapasui mtumbwi. | | | | |
| 19. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho. | | | | |
| 20. Kitatange hutia chafi lemani. | | | | |
| 21. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba. | | | | |
| 22. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni. | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 23. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo. | | | | |
| 24. Pono mmoja akioza huoza na shazile. | | | | |
| 25. Pweza kamwambia ngisi, ‘tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi’ | | | | |
| 26. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa. | | | | |
| 27. Taa haachi mwibawe. | | | | |
| 28. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba. | | | | |
| 29. Umekuwa nguva huhimili kishindo? | | | | |
| 30. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni? | | | | |
| 31. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa. | | | | |
| 32. Zobe na msuwele wote ni wamoja. | | | | |

Shukurani kubwa kwa muda wako. Data hii itanifaa pakubwa katika utafiti huu.

## KIAMBATISHO "B"

## DATA YA UCHANGANUZI

**METHALI ZA KISWAHILI ZINAZOREJELEA VIUMBE WA MAJINI**

1. Alaye kitu cha mamba asifike mtoni.
2. Ana nchi yake simba ana maji yake mamba.
3. Anayetaka kufa na ale bunju.
4. Atakaye maji mtoni asimtukane mamba.
5. Aavumaye baharini papa kumbe wengine wapo.
6. Binadamu ni ngamba hawakosi la kuamba.
7. Chafi kandani mwako ni chafi-kiyenge.
8. Chafi rasilmali yake utumbo.
9. Choko choko kamchokoe pweza, binadamu hutamweza.
10. Chombo cha samaki hakiachi kunuka vumba.
11. Chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba.
12. Chura akitupwa majini hafi.
13. Chura hupenda maji lakini si maji moto.
14. Chura huweza kumwua tembo.
15. Chura humzuia maji ndovu akiyatamani.
16. Dagaa amemponza ndobe.
17. Dunia mwendo wa ngisi.
18. Ewe mtuje, kwamba wali tafi ungalikuwaje?
19. Hasira za mkizi tijara (furaha) ya mvuvi.
20. Huna mshipi, huna ngwe kuomoa tenga ni nini?
21. Kaa akiinua gando mambo yamekatika.
22. Kaa mkuu ng'ombe wa maji akiinua gando mwelemeze nanda.
23. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa.
24. Kambare mkunje angali mbichi.
25. Kangaja simle, mchuzi kitoweo.
26. Kasirani ya mkizi ni furaha kwa mwenye tando.

27. Kiboko aliyepasha habari hapasui mtumbwi.
28. Kila mvuvi wa pweza tutaonana mwambani.
29. Kilichompata ngwena na kiboko ni hicho.
30. Kitatange hutia chafi lemani.
31. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumwosha.
32. Kumla nguru si kazi, kazi ni kumtoa magamba.
33. Kuvua nguru si kazi, kazi ni kumwosha.
34. Kuvua numbi si kazi, kazi magawioni.
35. Maji marefu mwulize chura.
36. Mamba hutoka majini na kulamba umande.
37. Maskini hajui kula na mkwasi, akianza kula samaki huanza kichwani.
38. Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendapo.
39. Mchagua samaki hupata aliyechina.
40. Mtafitafi hula samaki (nswi) mtulivu hula nyama.
41. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo.
42. Nguvu ya mamba ni maji.
43. Ngwena na mwenzake (mwingine) hawapatani.
44. Nyama wote wangawako, mkuza pezini papa.
45. Pono mmoja akioza huoza na shazile.
46. Pweza kamwambia ngisi, ‘tusifanye majilisi, maji yakipwa tukisi’
47. Samaki akilia machozi yake hupelekwa na maji.
48. Samaki huanza kuoza kichwani.
49. Samaki mkunje angali mbichi.
50. Samaki mmoja akioza, huoza wote.
51. Samaki mmoja akioza ni mtungo pia.
52. Samaki wote hunuka walimshuku kambare.
53. Shuka ya maskini ndiyo itandiwayo dagaa.
54. Taa haachi mwibawe.
55. Ukikaa na simba, vaa ngozi ya mamba.
56. Ulimwengu umemshinda kaa endaye upande upande.

57. Umekuwa nguva huhimili kishindo?
58. Umeona wapi mnandi kujenga nyumba machweoni?
59. Ungenda juu kiboko makazi yako pwani.
60. Usiku kiza mangazimbwe mtumbuu huwa papa.
61. Uso wa samaki hausikii viungo.
62. Wavu utakaonasa samaki wengi huanza mapema.
63. Wavuvi wa pweza hujuana mwambani.
64. Zobe na msuwele wote ni wamoja.